ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria

		na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa

		na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini

30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tisa - Tarehe 19 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya mwaka 2017/2018.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 37

Usimamizi wa Zaka na Sadaka

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana moja kati ya majukumu yake makuu ni kusimamia zaka na sadaka. Na kwa sababu zaka ni haki ya kisheria kwa kila muislam ambazo enzi za Bwana Mtume (S.A.W) ilikuwa ni lazima kutoa zaka kwani ni haki ambayo imeainishwa kutolewa kwa kiwango maalum kwa mwaka tofauti na inavyotendeka hivi sasa mtu kutoa zaka anavyotaka na kwamba hamna mtu au taasisi ya kusimamia utoaji wa zaka.

(a) Je, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina mpango gani wa kusimamia na kuhakikisha kwamba watu wenye uwezo wanatoa zaka kama inavyotakiwa.

(b) Je, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina utaratibu gani wa kukusanya zaka kwa kila mwaka na kuzigawa kwa maskini na mayatima na wote wenye haki ya kupata zaka hizo kuliko kuwaachia watu kugawa zaka hizo wao wenyewe ambapo kwa sasa inaonekana kwamba zaka na sadaka nyingi huwa haziwafikii walengwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora) - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 37 kama ifuatavyo:
Mhe. Spika, ni kweli moja ya majukumu ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni kusimamia maswali mazima ya zaka na sadaka ambazo ni katika haki za kisheria. Zaka ni nguzo miongoni mwa nguzo tano za uislam ambayo ni lazima kutolewa na muislam aliyekamilisha masharti yake, masharti hayo ni kuwa muislam, kuwa huru na mali kufikia kiwango na kupitiwa na mwaka (kwa baadhi ya mali). Kwa mujibu wa sheria za sasa kamisheni haina uwezo wa kumlazimisha mtu kutoa zaka au kumlazimisha mtu kupeleka zaka yake sehemu maalum. Aidha, mtu anakuwa na uwezo wa kugawa zaka yeye mwenyewe na akipenda kuiletea kamisheni zaka yake au kwa watu anaowahisi wataigawa zaka kwa mujibu wa sheria na kuwalenga wale wanaostahiki.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria Nam. 2 ya mwaka 2007 kifungu cha 60 (1) Kamisheni ina uwezo wa kuratibu, ukusanyaji na ugawaji wa zaka kwa kuhakikisha kwamba umma kwa jumla unaelewa vya kutosha kuhusu mambo yanayohusiana na zaka. Katika kulifanikisha hili kamisheni imeandaa muongozo wa zaka unaoelimisha na pia inaelimisha kupitia tovuti www.wakf.go.tz , vipindi vya redio na TV, ziara za kimafunzo kwenye vyuo vikuu na maskuli, kufanya semina katika sehemu za kazi, makala ya gazeti na vipeperushi kwa wanaofika kamisheni.

(b) Mhe. Spika, mtu anayewajibika na yuko tayari kutoa zaka anasaidiwa kutekekeza wajibu wake huo ipasavyo, fedha na mali za zaka zinazopokelewa zinazimamiwa na kutolewa ipasavyo kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa. Fedha za zaka zinazopatikana huwa zinasimamiwa na kugaiwa kama utaratibu uliokuja ndani ya *Qur-an* nao ni wa kuzigawa fedha hizo kwa watu wa aina nane.

Mhe. Spika, katika kuraghibisha na kuelimisha watu kuleta zaka zao, kamisheni ikishapokea zaka hizo huzigawa kwa mafungu yaliyotajwa katika *Qur-an* na maeneo ambayo zaka husika imekusanywa. Kwa mwaka 1438 sawa na 2017 kamisheni ilikusanya na kugawa fedha na bidhaa zenye thamani ya sh. 396,885,000/= ugavi ulizingatia mafungu na maeneo yaliyotajwa ndani ya *Qur-an.*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa ruhusa ya kumuuliza Mhe.Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa mujibu wa Sheria Nam. 2 kifungu (60) (1)

imeipa mamlaka kamisheni ya kuratibu namna bora ya kukusanya zaka na kwasababu kwenye jibu lako umesema kwamba mwaka 1438 zaka zilizokusanywa milioni 300.

a) Je. wewe unahisi kiwango hiki kilichokusanywa ndio kiwango sahihi ambacho kilitakiwa kukusanywa na kugaiwa kwa walengwa kama kamisheni ilivyo na wajibu wa kuratibu.

b) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kwa sasa ipo haja ya kuwa na kanuni bora ambayo itaelekeza namna bora ya kukusanya sadaka na zaka na kuzigawa kwa maskini kulikoni kwa hivi sasa kwamba hakuna kanuni ambayo ndio muongozo wa utekelezaji wa masuala hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali la nyongeza Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo:

a) Kuhusu kiwango halisi kama tulivyosema mwanzo zaka ni sadaka ambayo mtu anatoa akijaaliwa na kamisheni inapokea kwa hiyo huwezi kusema kiwango hiki kidogo au kikubwa lakini chochote kinachotolewa inakuwa ni kiwango halisi kwa wakati ule kwa sababu ndicho watu walichojaaliwa kukitoa.

b) Kamisheni imeona umuhimu wa kuweka kanuni bora ndio maana kuna sheria lakini kuna miongozo mbali mbali na makundi mbali mbali ambayo yanahitaji kutolewa zaka kwa wakati ule zinapopatikana, na ndio maana kamisheni inasimamia kutoa zile zaka kutokana na miongozo

iliyokuwemo ndani ya sheria na miongozo ambayo ipo ndani ya kamisheni.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kwa kuniona kuweza kunipa swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kujibu swali hili la zaka ambalo lipo kwenye meza yetu.

Mhe. Spika, mimi naomba nimuulize swali la nyongeza kwanza nimshukuru kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa lakini nimuulize kwamba zaka ipo kwa mujibu wa sheria kama ambavyo umesema na ndio maana malalamiko haya yamekuja kutokana na kwamba wale walengwa ambao wamekusudiwa kuzipata zaka hizi haziwafikii.

Je, huoni upo umuhimu wa wizara kusimamia ipasavyo juu ya mgawanyo huu wa zaka ili kuweza kuwafikia wale walengwa ambao wamekusudiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, siwezi kusema kwamba zaka haziwafikii waliokusudiwa kwa sababu kwa mujibu wa muongozo wa Kamisheni ya Wakfu kwamba zaka zile zinakwenda kwa makundi ya watu ambao wameainishwa, kuna mayatima, wasiokuwa na uwezo na makundi mengine. Katika hili kamisheni inasimamia ipasavyo kufanya kazi zake kwa mujibu wa miongozo na sheria ambayo ipo. Sasa labda nikuombe Mhe. Mwakilishi kama unaona kwamba kuna sehemu ambayo zaka inakwenda kinyume na utaratibu ni vyema basi ukaisaidia wizara kutuletea taarifa kwamba zaka imegaiwa sehemu ambayo sio ili tuweze

kufanyakazi ya kufuatilia na kuona ukweli halisi wa jambo lenyewe. Ahsante sana.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri, ustadh swali moja tu la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa tumeambiwa tukumbushane na ukumbusho unawafaa waumini. Je, ni mara ngapi watendaji wako wamewaita matajiri wa nchi hii ili kuwakumbusha wajibu wao huu unaolingana na zaka.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Said Omar Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema katika swali mama kamisheni kupitia vipindi mbali mbali vya redio, TV, lakini magazeti na makala mbali mbali mara zote inatoa elimu kwa kukumbusha umuhimu wa waislam kutoa zaka. Lakini ni wajibu wetu sisi watoaji kwamba kila mtu akubali kutakidi kila alichokuwa nacho ndani na kukitolea zaka. Lakini naomba niseme kwamba kamisheni inaendelea kusimamia na inaendelea kutoa elimu mara kadhaa katika kuwakumbusha waislam suala hili. Lakini pia niongeze kusema hata ndani ya misikiti yetu mara nyingi ukisikiliza hotuba za Ijumaa unaona kabisa jinsi mashekhe wanavyotoa elimu kwa kuwakumbusha Waislamu umuhimu wa kutoa zaka.

Nam. 65

Muongozo wa Kuwatumia Ng'ombe kubeba Mizigo

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika jitihada zake za kuwapatia haki za kila kitu kinachoishi kama haki za binaadam na haki za wanyama. Katika jitihada hizo nimeona suala la ng'ombe wanaofanywa madereva wa gari za ng'ombe kushamiri na kuonekana ni usafiri wa mizigo, lakini suala hili katika miaka ya nyuma halikuruhusiwa. Sijui kisheria au kidini au haki za wanyama lipo vipi kwa watu wanaowatumia ng'ombe hao.

(a) Je, kumtumia ng'ombe kwenye gari la ng'ombe na kubeba mizigo ni ruhusa.

(b) Je, ipo haki ya kuwabebesha ng'ombe mizigo kama gari za mizigo.

(c) Je, ng'ombe kukatazwa asitiwe kwenye gari hapo zamani ni sheria au haki za wanyama au kidini.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, **k**wa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake Nam. 65 kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, matumizi ya wanyama katika kazi mbali mbali zikiwemo za kilimo, ubebaji wa mizigo, usafiri na huduma nyenginezo yameruhusiwa kwa kuzingatia uwezo wa mnyama husika. Wanyama ambao wanatumika zaidi ni pamoja na ng'ombe, punda, farasi na ngamia.

b) Mhe. Spika, **wa**nyama hao wanaruhusiwa kutumiwa kwa kazi isipokuwa wabebeshwe mizigo kwa mujibu wa uwezo wao, wapate muda wa

kupumzika, pia wapewe chakula na maji ya kutosha pamoja na huduma nyengine za kinga na tiba kila inapohitajika.

c) Mhe. Spika, **k**wa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mifugo Nam. 11 ya mwaka 1999 ng'ombe wameruhusiwa kutumika kwenye magari ya ng'ombe. Aidha, sheria hiyo inalinda haki za wanyama na kukataza utesaji wa wanyama na kutoa maelekezo ya matumizi bora ya wanyama hao.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wote kufuata utaratibu mzuri wa utumiaji wa wanyama kazi na kulinda haki za wanyama kama ilivyoelekezwa katika sheria na vitabu vya dini.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa baadhi ya wanyama ninawaona wanabeba mizigo kwenye migongo na kwenye mapolo, lakini sasa ng'ombe anabebeshwa gari anakuwa dereva kwa muda mrefu. Sasa huyu nyama yake wakati wa kuchinjwa au akishakuchinjwa kiafya inakuwaje inakidhi haja maana anakuwa ametunisha msuli kipindi kirefu.

b) Huyu mnyama kama ng'ombe ni tofauti na punda, punda haliwi akishafika umri wake anauliwa tu au anakufa mwenyewe. Lakini huyu ng'ombe hatuoni kwamba tunampa adhabu mbili ya kumbebesha halafu tuje tumchinje.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said kama hivi ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, kwanza lazima tukubali kwamba mnyama kwa bahati mbaya hasemi na ingekuwa anasema kwa mizigo anayopakiwa kwa kweli haistahiki hata kidogo tunahitaji sisi kama binaadam kuwa na huruma. Wakati mwengine unamkuta ng'ombe amepakiwa mizigo halafu na mwenye ng'ombe amempanda juu yake. Sasa ukitizama kilo za ng'ombe kama ni 150 halafu mwenye ng'ombe ana kilo 70 halafu ana mzigo wa kilo zaidi ya 100 kwa kweli tunamuonea sana ng'ombe. Kwa hiyo, kwanza nasema upakiaji na utumiaji wa wanyama pamoja na kuwa wameruhusiwa hata ndani ya dini lakini inahitaji kama binadamu kuangalia kwa sababu wenzetu wanyama wetu hawana akili wala hisia kama sisi.

b) Ni kweli nyama ya ng'ombe ambaye amechukua mizigo muda mrefu inakuwa ngumu, sasa ule ni utashi wa mwenyewe mlaji akiona nyama ngumu haipendi wengine wanapenda nyama ngumu wanakula. Lakini nasema ni utashi wa mlaji mwenyewe akiona nyama inafaa kula atakula kama haifai ataacha.

Lakini Mheshimiwa suala la punda ni kweli kabisa punda yeye akishatua mizigo akishafikia umri ama anakufa au anaachwa tu anakuwa kwenye nyumba. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na

Uvuvi kwa ruhusa yako naomba kumuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe.Waziri ametwambia kwamba kuna wanyama hutwishwa mzigo kuliko kilo zake alizojaaliwa nazo na huwa ni athari mbaya juu ya uhai wake.

a) Je, kwa kuwa wizara inashughulika na wanyama wameweka sheria gani kwa anayekutwa na kosa kama hilo ili ashtakiwe.

b) Mhe. Waziri ametwambia kwamba nyama unaweza kuchagua yoyote unayoitaka wewe kama nyama ngumu au laini. Lakini swali langu lipo hapa ng'ombe tunategemea wanachinjwa katika machinjio maalum mlaji hajui wapi ng'ombe huyo alipochinjwa na hamjui kama alikuwa wa gari ama huyu alikuwa wa kawaida. Wana utaratibu gani wa kuwawekea alama ya maelezo huyu ng'ombe wa gari au huyu ng'ombe wa kawaida ili tunusurike na hayo matatizo yake.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:

a) Kwanza Mhe. Spika, ni kweli pamoja na kwamba ipo sheria lakini kwa bahati mbaya hatujaweza kusimamia vizuri kuona kwamba huyu ng'ombe ametwikwa mzigo nje ya uwezo wake. Kwa kweli ufuatiliaji wa sheria hii haujakuwa mzuri hata kidogo na ndio maana nikasema inategemea sana sisi binaadam kuhisi tu kwamba huyu ni mnyama ana uwezo fulani wa kuchukua mzigo na anakusaidia kubeba mizigo hakuna sababu ya kumbebesha

mizigo mingi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa sasa hivi sina kumbukumbu za sheria iliyotumika kuweza kuwaadhibu wale wanyama ambao wamepakiwa mizigo ya ziada.

b) Kuhusu kutambua nyama ngumu na nyama laini katika machinjio ng'ombe wanachinjwa katika sehemu mbali mbali na yule anayepeleka ng'ombe ndie anayeweza kusema kwamba ng'ombe wangu anafaa au ana sifa gani. Lakini kwa bahati nzuri ng'ombe ambae amepakiwa mizigo hapa kwenye shingo yake huwa kuna alama inaonekana kabisa kama ng'ombe huyu ni ng'ombe wa mizigo na unaweza ukamu-i*dentify* kuwa ni wa mizigo. Sasa kwa bahati mbaya hatujakuwa na utaratibu wa kusema kama huyu ng'ombe wa mizigo achinjwe kwa sababu hakuna sheria hiyo sasa hivi inayozuia ng'ombe ambaye anapakiwa mizigo kuwa asichinjwe. Lakini nasema ni wazo zuri labda tulizingatie na kwa sababu tuna upungufu wa nyama basi mnyama akichinjwa watu wanakula bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini katika sisi binaadam kuna wengine si waaminifu hutokezea mpaka kuchinja ng'ombe wafu na kupeleka katika mabucha.

Je, kuna utaratibu gani wa kuweza kutoa vibali vya uhakika kwamba ng'ombe huyu amepitia katika chinjio ili kuhakikisha kwamba walaji wanakula nyama iliyo bora na safi kabisa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali hili. Ni kweli kumekuwa na tatizo moja kubwa sana kwanza watu kuiba wanyama na kuwachinja halafu kuwapeleka kwenye maduka, lakini tumegundua hata wanyama wafu watu wamekwenda kuwapeleka wafu wakachinjwa halafu wakapelekwa watu wakala. Ni kweli kabisa kuna tatizo hilo la msingi na tunahitajika sote kuwa waaminifu, waadilifu kwamba mnyama anayeliwa, aliwe mnyama aliyekuwa halali, aliyekuwa anatakiwa atimize masharti yote.

Mhe. Spika, tunao utaratibu wa madaktari ambao wanawapima wanyama wakifika pale kwenye machinjio ili kutoa ithibati kwamba ng'ombe huyu amechinjwa na yuko katika hali salama. Vile vile ni wajibu wa masheha kule wanakotoka lazima aseme ng'ombe huyu ametoka sehemu fulani na kuna kibali cha kutoka pahala hapo. Hayo ndio mambo yatatusaidia kuweza kudhibiti uchinjaji wa nyama ambayo haiko katika hali inayostahiki. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 47

Viwango vya Ufaulu kwa Wanafunzi Kujiunga na Chuo cha Ualimu

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa lengo la serikali ni kutoa elimu bora ili vijana wetu pamoja na taifa liweze kusonga mbele na kwa sababu chimbuko la kupata elimu bora ni kuwa na walimu bora waliofaulu vizuri kuanzia ngazi ya *'O' level*.

(a) Je, ni kiwango gani cha ufaulu kinachohitajika cha *'O' level* (*form IV*) kwa mwanafunzi anayeomba kujiunga na chuo cha ualimu.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kupeleka na kukamilisha vifaa vya maabara katika skuli ambazo zina upungufu wa vifaa vya maabara jambo ambalo ni changamoto kubwa ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanafaulu vizuri masomo ya sayansi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa elimu bora itapatikana kutokana na kuwa na walimu bora waliofaulu vizuri masomo yao ya ngazi ya elimu ya sekondari *'O' level* na ngazi za elimu ya juu ambao watajiunga na mafunzo ya ualimu katika Vyuo vya Ualimu au Vyuo Vikuu.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:

a) Sifa za kujiunga na mafunzo ya ualimu katika ngazi ya cheti cha ualimu ni kama hivi ifuatavyo:

i) Muombaji wa mafunzo ya ualimu cheti cha maandalizi na msingi lazima awe amefaulu masomo ya elimu ya sekondari na kupata alama angalau kuanzia D tano (5) zikiwemo D mbili za sayansi.

ii) Muombaji wa mafunzo ya diploma ya elimu ya msingi ya sayansi lazima awe amefaulu katika kiwango cha C masomo (3) ikiwemo angalau somo moja (1) la sayansi, au awe amefaulu masomo mawili kwa kiwango cha C masomo mawili (2) na D tatu (3) yakiwemo masomo mawili ya sayansi na cheti cha ualimu.

b) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imenunua na kusambaza katika skuli zake zote vifaa vya maabara mara mbili kwa mwaka. Vifaa hivyo vinasambazwa hasa katika skuli zinazotarajiwa kufanya mitihani ya taifa ya kidato cha nne na kidato cha sita. Katika mwaka 2018/2019, wizara imepanga kuongeza fungu la fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara ili iweze kuzipatia skuli vifaa vingi zaidi na kuziwezesha skuli kuwapa wanafunzi mazoezi mengi ya vitendo. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na majibu yake mazuri nampongeza sana kwa majibu ya ufasaha ambayo yamenipa uelewa.

a) Kwa kuwa umesema wizara inanunua vifaa vya maabara mara mbili na kuvisambaza katika skuli zetu kwa mwaka. Mimi nilitaka nijue ni idadi gani ya fedha zimetumika kwa ajili ya hivyo vifaa kwa mwaka huu unaoishia 2018 ambao sasa tupo katika mwezi wa Februari kwa sababu zipo baadhi ya skuli nina uhakika nazo kama hazina hivyo vifaa.

b) Je, ni skuli ngapi za sekondari ambazo zina maabara za kiwango bora na cha kisasa kwa Unguja na Pemba na ambazo zina walimu wenye uwezo wa hali ya juu wa kutumia vifaa hivyo vya maabara vilivyoletwa ili kuweza kupandisha kiwango cha elimu cha watoto wetu. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu 2017/2018 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imetumia milioni 512,924,000 kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara, na vifaa hivi baada ya kununuliwa vimeshasambazwa katika skuli mbali mbali za sekondari za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kuhusu hali ya maabara lazima tukiri kwamba kwa sasa hakuna maabara hata moja ambayo ina msimamizi wa maabara, na hili tunaelewa kwamba na upungufu na taratibu za kuwatafuta watu hawa zitafanywa ili kuona kila maabara ina mtaalam wake wa maabara ambayo itasaidia sana kutoa mafunzo ya vitendo. Kwa sasa maabara hizi zinasimamiwa na walimu wenyewe wa masomo. Kwa hivyo, walimu wa masomo wanapata kazi mbili kubwa kabisa kuipanga maabara yenyewe, halafu na kusomesha. Kwa hivyo, hili jawabu nadhani tumemjibu kama tulivyoeleza hapo mwanzo.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri yenye kufurahisha. Kwa kuwa mzigo wa kusomesha mwanafunzi ni mzigo wa taifa. Je, ana mpango gani alau wa kalili kuzisaidia skuli binafsi kuwapa hivi vifaa vya maabara kusudi kupatikana wataalam zaidi watakaotumikia nchi yetu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina mpango wa kuzigaia skuli binafsi vifaa hivi kwa vile skuli hizi kimsingi zipo katika mfumo zaidi wa kufanya biashara. Kwa hivyo, wao wenyewe wanalazimika kununua vifaa vyao kwa mujibu wa uwezo wao.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Naibu Waziri umekiri kwamba suala la maabara ni muhimu sana katika skuli zetu za Unguja na Pemba. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuliboresha suala hili katika skuli zetu za Unguja na Pemba ili wanafunzi waweze kupata taaluma inayostahiki katika maskuli yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, hivi karibuni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Idara yake ya Elimu ya Sekondari ilifanya utafiti wa kina ili kujua hali halisi za maabara yetu, kujua vifaa halisi vilivyopo katika maabara zetu za skuli, kujua wasimamizi waliopo na kujua skuli gani ina vifaa vya maabara na havitumiki, na kujua skuli gani hawana na kadhalika. Baada ya utafiti huo idara imependekeza mikakati mbali mbali ikiwa ni pamoja na hili ambalo nimesema mwanzo kuwapata wataalam wa maabara *(lab technicians)*. Hilo ni moja.

Pili, kutokana na upungufu uliobainika katika utafiti huo ndio tumesema kwamba mwaka wa fedha ujao wizara itaongeza fungu hili.

Tatu, pia wizara imepanga mpango wa kutoa mafunzo ya ziada kwa ajili ya usimamizi wa maabara na katika Mradi wa Kuimarisha Elimu *(ESP)* pia suala hili la maabara limeimarishwa. Kwa hivyo, hiyo ni baadhi ya mikakati ambayo wizara itachukua kuimarisha. Ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini ndani ya majibu yake alisema serikali haina mpango wa kutoa vifaa vya maabara katika skuli binafsi kwa sababu kubwa wanafanya biashara. Lakini Wizara yake hiyo hiyo ya Elimu tumeshuhudia wanatoa vitabu katika skuli binafsi. Ni kwa nini wasifikirie na suala hili la vifaa vya maabara likawa limo katika mpango kama ambavyo vile vitabu vya kufundishia wanatoa katika skuli binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, vifaa vya maabara na vitabu ni mambo mawili tofauti kidogo. Hata hivyo, wizara inatoa vitabu nakala chache sana, nakala tano tano kwa kila skuli ni chache sana, kama ni mfano wa kuwaonesha. Kwa hivyo, hatuwezi kulinganisha gharama hizi na gharama za maabara, lakini kimsingi hasa kwamba wao wana nafasi zaidi ya kutumia vyanzo vyao vya fedha vya kununua vifaa vyao. Baadhi ya mambo ambayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunawasaidia skuli binafsi ni pamoja na kuwapatia baadhi ya nyaraka zetu, lakini pia tumewaruhusu kwa kupatiwa vitabu kama watakuwa na uwezo kuweza kuvichapisha na kutumia katika skuli zao. Ni skuli chache ambazo kuna mkataba maalum huwa tunasaidia baadhi ya vifaa, lakini ni chache mno nadhani ni moja.

Kwa mfano, Al-Ihsan tunasaidiana kidogo baadhi ya vifaa pamoja na JKU. Ahsante sana.

Nam. 20

Ujenzi wa Mabweni katika Skuli za Sekondari

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika kuleta maendeleo ya elimu na ufaulu wa wanafunzi katika masomo yao. Lakini kuna changamoto kwa mfano, katika Skuli ya Madungu Sekondari ambayo inachukua wanafunzi takriban kutoka maeneo mengi ya Pemba, skuli hiyo haina mabweni ya kulala wanafunzi hao. Wanafunzi wa skuli hiyo hukodiwa nyumba za jirani kitu ambacho sio sahihi sana.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa kujenga mabweni katika skuli za sekondari na skuli zote kubwa ambazo hazina mabweni nchini ili wanafunzi wakae pamoja na kuweza kudurusu masomo yao katika kujitayarisha na mitihani.

(b) Katika skuli ya Madungu Sekondari zipo nyumba karibu na skuli hiyo ambazo wanafunzi huzitumia kama mabweni, Je, nyumba hizo ni za serikali au ni za watu binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 lenye vipengele (a) na (b) kwanza napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:

Skuli ya Sekondari ya Madungu ni moja katika skuli mpya iliyojengwa kupitia mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi.

Skuli hiyo haikukusudiwa kuwa ni ya bweni bali ni skuli ya kutwa. Skuli hiyo imekusudiwa kupokea wanafunzi wa sekondari kutoka maeneo ya mji wa Chake Chake ambao watasoma na kurejea majumbani mwao. Kama kuna wanafunzi wanaotoka katika mitaa ya mbali ya mji wa Chake Chake hawakupaswa kusoma katika skuli hiyo na wizara iko tayari kuwahamishia katika skuli za sekondari za karibu na maeneo wanayoishi. Hata hivyo, kwa siku za karibuni kumekuwa na mtazamo wa baadhi ya skuli ikiwemo Skuli ya Sekondari ya Madungu kuwaweka baadhi ya wanafunzi wake katika nyumba za kuazima kwa lengo la kuwasaidia zaidi kimasomo. Hata hivyo, kuanzisha bweni la wanafunzi kwa kukodi nyumba ya mtu binafsi si utaratibu bora wa kuendesha dakhalia na pia kunakosa udhibiti mzuri wa wanafunzi. Hivyo, wanafunzi hawa hawapo katika mazingira mazuri ya kiusalama katika nyumba kama hizo.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:

a) Serikali inaona umuhimu wa kuwa na skuli za bweni katika baadhi ya skuli na maeneo, lakini sio katika kila skuli hasa za maeneo ya miji. Kwa mwaka 2017/2018, serikali imeanzisha skuli ya bweni katika Skuli ya Sekondari ya Mohammed Juma Pindua Mkoani, Mkanyageni na kupokea wanafunzi wa sekondari katika maeneo mbali mbali ya Pemba. Pia, skuli za *Fidel Castro*, Utaani na Kengeja zimeendelea kutoa huduma za dakhalia kwa wanafunzi waliopangiwa kusoma katika skuli hizo.

b) Nyumba iliyogeuzwa kuwa ni bweni la wanafunzi karibu ya Skuli ya Sekondari ya Madungu ni nyumba ya mtu binafsi. Bweni hilo limefanywa kwa makubaliano binafsi kati ya skuli na mwenye nyumba. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa ufafanuzi wake lakini niulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa amesema kwamba kukodi mabweni ya binafsi au sehemu ambazo zinakuwa ni nyumba za kukodi sio utaratibu mzuri, lakini suala hili sasa hivi limeonekana kwamba skuli yoyote ikikaribia mitihani lazima walimu wanawaweka kambi kwa ajili ya kuongeza nguvu za kuweza kufanya mitihani yao vizuri zaidi. Na ni lazima watoto walale pamoja ili waweze kukaa na walimu na ku-*solve* mitihani yao. Je, waziri haoni sasa umeshafikia muda na kubadilisha program ya kuweka madakhalia katika maeneo ili kukidhi haja hii.

b) Kama skuli ile ambayo iko pale Madungu, pana skuli ya Shamiani ziko skuli karibu tano pale mpaka Pondeani na zote zina *form IV.* Huoni kuwa imeshafika wakati kwa Chake Chake kuwajengea dakhalia kwa sababu skuli zimekuwa nyingi na wanafunzi wamekuwa wengi na wanafunzi wengine wanatoka Pujini, wengine wanatoka Tundaua ambako hakuna skuli hizo na lazima walale mjini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaona ipo haja ya kuweka dakhalia lakini si kila eneo wala si kila skuli kuwa na dakhalia yake. Dakhalia zitajengwa pale ambapo pataonekana kwamba pana haja ya kujenga dakhalia. Kuwepo kwa skuli nyingi za sekondari karibu na wananchi maana yake kwamba

imekusudiwa wanafunzi waweze kusoma katika maeneo hayo na baadae kuweza kurudi nyumbani. Kwa hivyo, kwa sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina mpango wa kujenga dakhalia kila penye skuli. Lakini hizi dakhalia zilizopo zitaendelea kuimarishwa na nyengine ambazo itaonekana inafaa itaweza kujengwa hapo baadae baada ya utaratibu mzima huu wa dakhalia kufanyiwa upembuzi yakinifu na ukionekana kwamba una tija fulani au una manufaa fulani serikali itayarejesha.

Mhe. Spika, kuhusu kujenga dakhalia Chake Chake, Chake Chake inayo dakhalia *Fidel Castro*, kwa hivyo ni kwamba baadhi ya wanafunzi na wapo sasa hivi katika *Fidel Castro* wanaishi dakhalia ile. Lakini Chake Chake mjini serikali kwa sasa haina mpango wa kujenga dakhalia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri lakini naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Swali kama hilo hilo la Chake Chake la Madungu linafanana na skuli ya Mpendae, kwa sababu skuli ya Mpendae tunaishukuru serikali wametujengea skuli mpya, ya kisasa yenye kila aina ya hadhi na vijana wa pale wanaweka kambi baadhi ya siku lakini pana maeneo yamejengwa kwa kuwahifadhi katika wakati ule mgumu wa kambi. Je, serikali ina mpango gani kumaliza majengo yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake. Kama ni majengo yanayohusiana na dakhalia, majengo yale yalikuwemo katika mradi mkubwa ambao ulitayarishwa hapo awali. Ilipofika wakati wa utekelezaji ikawa fedha zilizotengwa hazitoshi tena kuweza kuzipatia skuli zile dakhalia na iliposhindwa kufanya hivyo tukaona kwamba kile kilichopatikana kijengwe, na tukajenga skuli zile na si Mpendae peke yake na nyenginezo pia. Kwa hivyo, pale ambapo serikali itapata uwezo basi itaendeleza ujenzi wa dakhalia katika skuli zile

ambazo zilikuwa na mpango wa kujengwa dakhalia lakini pesa hazikutosha kwa wakati huo.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alikiri kwamba kuna nyumba ya mtu binafsi ambayo inatumika kama bweni la watoto pale skuli ya Madungu.

a) Je, wizara yake imechukua hatua gani katika kuhakikisha nyumba hiyo haipo katika eneo la skuli.

b) Ni hatua gani zilizochukuliwa baada ya kubaini kwamba wanafunzi wanakaa pahali ambapo si salama kwa usalama wao na si jengo la serikali. Ni hatua gani wizara yake itachukua kuhakikisha kwamba wanafunzi wale hawatokaa tena katika nyumba hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi. Ni kwamba jengo liliopo pale ni jengo la mtu binafsi na majengo ya binafsi katika maeneo mbali mbali ya skuli yako mengi, si Madungu peke yake. Kwa maana hiyo, sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itajaribu kuzungumza na wale ambao wamejenga katika maeneo ya skuli kuweza kuondoka hasa, wale ambao wamejenga kinyume na taratibu tutawataka maeneo hayo waondoke. Mwanzo tutazungumza nao kwa busara na hekima na baadae ikibidi tunaweza kutumia sheria zilizoko ili kuweza kuwahamisha watu hao.

Kuhusu kambi amezungumza vizuri mwakilishi mmoja. Kimsingi kambi si kitu halali katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini imefika wakati tukapima lipi bora zaidi kuziruhusu kwa masharti maalum ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wako salama, wanapatiwa ulinzi wa kutosha ili vijana wetu wapate fursa

ya kudurusu au kuziondoa moja kwa moja. Wizara ikatumia busara na hekima ikaona kwamba ni vyema baadhi yake zikaendelea kwa masharti. Kwa hivyo, kambi zote zilizopo sasa hivi zipo kwa masharti maalum, lakini si kwamba wizara inafurahia jambo lile.

Hata Skuli ya Madungu kuna *matron* wanne wanaofanya ulinzi pale, pana walinzi wa UMAWA wanaosaidia ulinzi pale. Lakini pamoja na hayo yote bado hatujaridhia moja kwa moja bado tunatoa masharti katika kufungua kambi hizi. Tunafanya hivyo kwa sababu tunahisi kambi zina tija zaidi kielimu, wakati tunajiandaa kurudisha dakhalia baadhi ya sehemu tunazivumilia kambi kwa muda. Ahsante sana.

Nam. 27

Kufanyiwa Matengenezo Barabara ya Mtambile – Kangani na Kengeja - Muwambe

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Aliuliza:

Njia za Mkoa wa Kusini Pemba zimejengwa ili kuwarahisishia wananchi usafiri na kufanya shughuli za kimaendeleo ili kujikwamua na hali ngumu ya umaskini. Hata hivyo, njia hizi kwa sasa zimeharibika vibaya hususan barabara ya Mtambile – Kangani na Kengeja – Muwambe.

(a) Je, Mhe. Waziri unalijua hili.

(b) Ni lini ulifanya ziara katika maeneo haya ili kusikiliza kilio cha wakaazi wa eneo hili.

(c) Ni lini hasa njia hizi zitafanyiwa matengenezo makubwa ili ziweze kupitika kwa urahisi na kupunguza kilio cha wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumuarifu Mhe. Mwakilishi kuwa nalifahamu vizuri suala hili

(b) Katika barabara hizo tayari nimeshafanya ziara mara nyingi na hivi karibuni tu nilikuwepo huko Pemba kwa ajili ya kuzikagua barabara hizo na kukutana na wananchi.

(c) Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Idara ya *UUB* Pemba inafanya maandalizi ya kuziba mashimo kwenye barabara hizo ili ziweze kupitika kwa urahisi wakati serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya kuzipandishia barabara hizo. Vile vile wizara kwa sasa inaendelea kufanya utafiti ili kubaini ni sababu gani zilizosababisha kupata athari kwa barabara hizo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri mimi ningependa kumuuliza swali moja. Ni lini maandalizi hayo yataanza kuhusu barabara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo. Kama nilivyosema hapo mwanzo barabara zile zimeathirika na sisi tunaendelea na utafiti wa kuweza kujua nini chanzo ambacho kimesababisha mpaka barabara zile ziharibike. Lakini vile vile kabla ya hapo kuna baadhi ya barabara ambazo anazijua Mheshimiwa kama vile

Mtambile-Mwambe na Mtambile-Kangani tulianza kuzitia viraka sasa hivi tupo katika barabara ya Mkoani-Chake Chake na barabara ya kutoka Maili Tano mpaka Konde tunaendelea kutia viraka, tukitoka kule tutaendelea kuzitia barabara zile viraka ili zipitike wakati wowote huku tunajitayarisha tutakapopata fedha kwa ajili ya kuzipandishia barabara zile. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara hizi hususan ya Mtambile-Muwambe zimejengwa kwa muda mrefu na wakati zilipokuwa zinajengwa watu waliharibiwa vipando vyao na kwa muda mkubwa sana bado hawajalipwa. Je, Mhe. Waziri watu hawa watalipwa lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo. Ni kweli barabara hizi tunadaiwa fidia za vipando na tupo katika mpango kuhakikisha kwamba kama tulivyowalipa wengine basi zile fedha ambazo wastani wa takribani shilingi 100 milioni basi na wao tunazilipa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba anakiri kuwa baadhi ya barabara zilizoko Pemba zina mashimo. Lakini Mhe. Waziri wafanyakazi wa kitengo cha Barabara Pemba wanafidia yao wanadai tangu Mei zilipotokea mvua kubwa zile, lakini sasa mashimo haya yanatarajiwa kuzibwa na hao hao wafanyakazi na anakiri kwamba pesa zile zimetoka lakini mpaka leo hawajazipata.

Je, ni lini wafanyakazi wale watapata pesa zao ambazo ni haki yao ili kuhakikisha kuziba hivyo viraka kuwa madhubuti zaidi na kuacha kuja kutuondosha njiani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Ni juzi tu hapa niliulizwa swali hili na Mheshimiwa mmoja katika Baraza la Wawakilishi na nikamjibu nitalifuatilia hili mpaka nihakikishe kwamba wale wanalipwa. Napenda kutoa taarifa kwamba hivi sasa wameshaanza kulipwa na wataendelea kulipwa mpaka zile pesa zao zote zimalize, kwani kazi waliyoifanya ni kubwa sana katika kuzinusuru zile barabara na sisi lazima tuwalipe haki yao. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mheshimiwa kwa sababu ya umuhimu wake nitaongeza kidogo, naanza na Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi kwanza niipongeze serikali kwa jitihada zake za kutujengea barabara nzito na nzuri ambazo tunategemea ni usalama wa maisha yetu na kuokoa fedha zetu. Lakini swali langu liko hapa, kwa mfano barabara yangu ya Kwarara, barabara nzuri lakini kingo za barabarani hamna inaanza kumong'onyoka siku za mvua ni hatari tutaikosa mapema. Kwa hivyo, namuomba Mheshimiwa hili je, ana mpango gani wa kuifanyia utaratibu wa kuijengea kingo pembeni na kuweka matuta ya usalama kwa ajili ya watu wetu.

Pili, kwa kuwa barabara zina umuhimu sana wa usafirishaji wa bidhaa mbali mbali kwa mnfao barabara ya Tunguu kutoka Kwa Bi. Khole mpaka Makunduchi, hivi sasa zina mashimo mengi ni hatari kwa ajili ya wasafiri na kwamba wanatoa huduma mbali mbali kwa ajili ya wananchi wetu. Wizara ina mpango gani wa kuweka viraka katika barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Tunakiri kwamba zile kingo zina umuhimu wa kutaka kuhamiwa kabla ya mvua za masika hazijaja zikaleta athari. kwa hivyo suala lake tutalichukua na tutalifanyia kazi.

Kuhusu barabara anayosema ni kweli sisi tunakiri barabara nyingi kutokana na mvua kubwa zina mashimo, lakini akitembelea sasa hivi aende aangalie Pete na sehemu nyengine, aangalie Bububu, Mwachealale barabara inayokwenda mpaka Kitope na nyengine zote hivi sasa tumeshaanza kuziba mashimo. Na tutaendelea kuziba mashimo mpaka tunahakikisha kwamba zile barabara zitapitika wakati wowote wakati ile barabara ambayo hivi sasa iko katika tathmini ya kutaka kujua namna gani ile barabara gharama zake tupate kuijenga na tumetenga shilingi 500 milioni kwa barabara ile. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa kuuliza swali zuri sana ambalo linagusa wananchi wangu. Mhe. Spika, mimi swali langu dogo tu, kwa kuwa miaka nenda na miaka rudi barabara ya Koani kwenda Jumbi imekuwa ina changamoto sana hasa kwa upande wa serikali baada ya yule *contractor* aliyekuwa amepewa kushindwa kutimiza majukumu yake pamoja na mkataba. Sasa kwa kuwa mvua za masika zinakuja na barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa maeneo yale pamoja na upande wa huku Jumbi.

Je, wizara yake inajipangaje kuhakikisha kwamba zile kero zinazowakuta wananchi katika kipindi hiki zitaondoshwa ili

tuweze kuvuka kwa salama mpaka pale ambapo wataweza kukamilisha utaratibu wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake kama ifuatavyo. Barabara ile anayosema ni miongoni mwa barabara tatu ambazo zilikuwa zijengwe na Dishapria**,** lakini kutokana na matatizo tumemaliza barabara ya Jendele mpaka Unguja Ukuu na barabara hii ya Koani - Jumbi. Hivi sasa tumeshatangaza *tender* na wakati wowote zabuni baada ya kufanikiwa tutamtangaza kwa ajili ya ujenzi. Kwa hivyo, mimi namuomba awe na stahamala kwa sababu tayari tupo katika mchakato wa kuhakikisha kwamba ile barabara inajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Spika, nakushukuru maana nilikuwa nimeshavunjika moyo, naomba niulize swali la nyongeza lenye (a) na (b) kwa Mhe. Naibu Waziri.

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa alitoa ahadi kwa wamiliki wa *Double Tree by Hilton* Nungwi tulipokutana nao kwamba *as soon as possible* atawarekebishia barabara yao kwa njia ya kifusi au kutia rojo la lami. Sasa barabara ile kwa kuwa muda mrefu imeshakaa na wameshaona wamedanganywa. Ni lini sasa atatoa kauli atakwenda kuirekebisha barabara ile ya Nungwi.

(b) Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kutia saini kwa barabara ya Bububu hadi Chaani kwenda Mkokotoni na barabara ile takriban itachukua mwaka mmoja na miezi miwili kumalizika. Hadi hivi ninavyosema Mhe. Spika, barabara ya Chaani haipitiki ina mashimo mengi na mavumbi ambayo yanaathiri watu macho, pumu na vifua. Ni lini sasa barabara ile ya Chaani

itatiwa rojo la lami hadi itakapotiwa lami kamili ili kuepusha madhara yale na njia kupitika kwa salama. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwaklishi maswali yake mawili yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kuhusu barabara ya Nungwi barabara za ndani zote ziko chini ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lakini kama tulivyokutana na wale wawekezaji tukashauriana kama tunavyofanya barabara nyengine, tumewataka wakae pamoja na sisi pamoja na Mwakilishi wake ili kuhakikisha namna gani tutaitengeneza. Lakini nataka kusema hapa kwamba, tuna vifaa vichache na sasa hivi bado tupo Mgonjoni na kifaa chetu ia kimeharibika kwa upande ule. Kwa hivyo naomba watustahamilie watakapokuwa tayari tutakuwa nao pamoja.

Kuhusu barabara anayosema hivi sasa yeye ni shuhuda kwamba vifaa vimeshaanza kuwasili Gamba pale na wakati wowote ile barabara itaanza kazi. Kwa hivyo, namuomba awe na moyo wa ustahamilivu kama wananchi walivyosubiri kipindi chote katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza Ilani ya Uchaguzi na tunatoa ahadi basi na hii barabara nayo watafurahia matunda kama walivyofurahia barabara nyengine. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 29

Vyanzo vya Kiutalii kwa Wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja

Mhe. Simai Mohammed Said - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Spika, nianze kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kumpongeza leo kwa majibu mazuri Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Baada ya hapo naomba swali langu Nam. 20 katika orodha ya kazi ya siku ya leo lijibiwe. Ahsante sana.

Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Kusini hasa katika vijiji vya Uzi, Uzi Ng'ambwa, Unguja Ukuu Kaebona, Tindini, Kaepwani, Kikungwi pamoja na Bungi wamezungukwa na visiwa vidogo vingi kwa upande wa Magharibi.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa kuwashajihisha wananchi katika matumizi ya visiwa hivyo kutoka uvuvi na kuanzisha michezo ya bahari ili kujiongezea kipato.

(b) Ni kwa nini serikali haiwatafutii wananchi hao mradi wa hoteli katika visiwa hivyo ambao utawasaidia katika maendeleo ya ajira pamoja na elimu kutokana na mapato hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, serikali kupitia Kamisheni ya Utalii imekuwa ikiandaa vipindi mbali mbali vyenye nia ya kuwaelimisha wananchi kuhusu fursa zilizokuwepo katika sekta ya utalii na namna wanavyoweza wakafaidika nazo.

Mhe. Spika, serikali kupitia mradi wa matokeo kwa ustawi imeweka mpango wa kuvitumia visiwa vilivyo karibu na vijiji vya Uzi, Uzi Ng'ambwa, Unguja Ukuu Kaebona, Tindini, Kaepwani na Kikungwi kwa ajili ya shughuli za utalii. Utekelezaji wa mpango huo utasaidia kuongeza ajira kwa wananchi walio karibu na maeneo hayo.

(b) Mhe. Spika, serikali kupitia mradi wa maabara ya utalii ulifanya utafiti wa kuangalia namna bora ya matumizi ya visiwa kiutalii. Ripoti hiyo ilishauri kuwa na matumizi tofauti kulingana na jinsi kisiwa kilivyo, ripoti hiyo imewasilishwa serikalini kwa kupatiwa mwongozo. Hivyo basi, serikali itaangalia matumizi yaliyopendekezwa katika visiwa vilivyo karibu na maeneo hayo na kuwashauri wananchi wa maeneo hayo ipasavyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

(a) Lakini Mhe. Spika, kwa kuwa miaka nenda miaka rudi kumekuwa na mwamko mdogo sana wa Wazanzibari hasa katika vijiji vyetu tofauti kuingia kwenye ubia hasa kwa kutumia ile Sheria ya *Public Private Partnership* ili kuanza miradi tofauti katika maeneo tofauti. Sasa je, Mhe. Waziri atakuwa yupo tayari kwenda na mimi kwa wananchi hasa katika Kamati ya Maendeleo ya Unguja Ukuu ili kuanza mchakato wa wananchi hawa kwenye maeneo ya Kisiwa cha Uzi, Unguja Ukuu Kaebona, Tindini pamoja na Kikungwi waweze kupatiwa kisiwa kwa ajili ya maendeleo.

(b) Kwa kuwa rasilimali ya visiwa vyetu hivi tulivyojaaliwa navyo Zanzibar ni rasilimali kubwa, lakini bado haijatumika vizuri. Lakini visiwa kama Chumbe pamoja na Misali na Mnemba vimetutilia sifa kubwa sana, lakini kisiwa cha *Prison Island* au Changuu hadi leo ukiangalia mapato yanayopatikana bado ni madogo. Je, serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba kisiwa cha *Prison Island* kinarudishwa serikalini ili wananchi wa Zanzibar waweze kufaidika na rasilimali hii. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, nipo tayari kufuatana naye kwenda Unguja Ukuu na kukutana na kamati za maeneo hayo ili kuona kwamba tunawapatia visiwa kiutalii.

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa amesema serikali kuna kisiwa kile cha Changuu kwamba kina mapato madogo. Nimuombe sana Mhe. Mwakilishi kwamba nia ya serikali na malengo ambayo imejiwekea ni kuingiza mapato mengi kupitia sekta ya utalii. Nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba kama anaona mapato ni madogo yanayoingia katika serikali kupitia utalii, nimtoe wasiwasi tu, bado tutaendelea kufanya kazi tutashirikiana kwa pamoja kwa kuwa yeye ni mdau wetu na anatembea sehemu mbali mbali, kwa hivyo tutashajihisha zaidi kuona na kisiwa kile kinazidi kuingiza mapato serikalini. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu lenye kifngu (a) na (b). Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini katika majibu yake amesema wizara ilifanya utafiti.

(a) Nilitaka kujua utafiti huo ulifanywa na nani kama wizara au kampuni, kama kampuni ni kampuni ipi.

(b) Miongoni mwa mapendekezo ambayo yalikwenda serikalini, ni mapendekezo yepi ambayo yatawafaidisha wananchi wa maeneo hayo miongoni mwa hayo ambayo yalikwenda serikalini. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, utafiti huu kama nilivyoeleza katika swali mama Kamisheni yetu ya Utalii ndio ambayo inafanya tafiti hizi kwa masuala ya kiutalii, na ndio maana nimesema kwamba kuna maabara ya utalii.

(b) Mapendekezo ambayo yamependekezwa na yamepelekwa serikalini ni kama suala la mwanzo nilivyomjibu kwamba, mapendekezo haya ni kuvifanyia utafiti visiwa hivi vya Uzi au na visiwa vyengine ambavyo tunavyo Zanzibar kuona kwamba vinafanyiwa kazi kiutalii. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Spika, nimsifu Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

(a) Mhe. Spika, lakini nimuulize Mhe. Naibu Waziri kidogo kwamba Zanzibar ina visiwa vidogo vidogo vingi vinavyokaliwa na watu na watu hao wana tamaduni mbali mbali. Je, Mhe. Naibu Waziri alishawahi kuvitembelea visiwa hivi na akajua tamaduni zao, ili baadhi ya tamaduni tuweze kuzitumia katika maendeleo yetu.

(b) Kama ataweza kuzitafutia tamaduni zile maana yake kuzijengea uwezo haoni kwamba atakuwa amevipandisha hadhi vile visiwa kujulikana pamoja na kupata mapato.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake swali lake lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kwanza naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba bado sijafanya ziara ya visiwa ambavyo vipo katika Zanzibar. Nimuahidi Mhe. Mwakilishi hili nalichukua na nitafanya ziara ya visiwa ambavyo ametutaka tufanye ziara na kuona maendeleo ya visiwa vile.

(b) Mhe. Spika, naona kwamba serikali ina umuhimu wa kuweka tamaduni katika Sekta ya Utalii na visiwa vile ili kuona tamaduni zile zinatumika vizuri ipasavyo kwa Sekta ya Utalii. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa maswali yamemalizika naomba kutoa matangazo ya wageni waliopo.

Wageni waliopo wa mwanzo ni wageni wa Mhe. Naibu Spika (Mhe. Mgeni Hassan Juma), wageni wenyewe ni Mhe. Saada Mkuya (Mbunge wa Jimbo la Welezo) karibu sana Mheshimiwa katika Baraza la Wawakilishi. Mgeni wa pili ni Ndg. Salma Moh'd Seif (Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa *VICOBA*. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mhe. Waziri Maudline Cyrus Castico Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto hawa ni wanaharakati wa Jumuiya za Maendeleo ya Jamii na wageni wenyewe ni kama hivi ifuatavyo:

Ndg. Joseph Emmanuel, Ndg. Kamtate Ishao, Ndg. Mary Mremi, Ndg. Leya Gadi, Ndg. Mangi Issack, Ndg. Emmanuel Kejo na Ndg. Asifiwe Mwamkenja, karibuni sana Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wageni wa Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Mwakilishi wa Kijitoupele hawa ni viongozi wa Wadi ya Jimbo la Kijitoupele. Wa kwanza ni kutoka Jimbo la Kijitoupele ni Ndg.

Shaaban Ali Saleh (Mwenyekiti), Ndg. Shaaban Mwinyi Kondo (Katibu), Ndg. Mwanaharusi Ali Abdulrahman (Katibu Mwenezi), Ndg. Rashid Vuai Vuai (Mwenyekiti wa Wazazi) na Ndg. Abdulhakim Hamad (Mwenyekiti wa Vijana). (*Makofi*)

Kutoka Wadi wa Kijitoupele ni Ndg. Mashavu Akui Khamis (Mwenyekiti), Ndg. Moh'd Issa Kidali (Katibu), Ndg. Mwanakheri Ali Pandu (Katibu Mwenyezi). (*Makofi*)

Kutoka Wadi wa Meli Nne Ndg. Maulid Ali Suleiman (Mwenyekiti), Ndg. Juma Zubeir Sultan (Katibu), Ndg. Mgeni Haroun Ali (Katibu Muenezi). Karibuni sana, karibuni katika Baraza la Wawakilishi. Ahsanteni. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Spika: Ahsante kuhusu utaratibu na nina watu wawili kwanza nianze na Mhe. Mohamed Said Mohamed halafu nitakuja na Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kuniona. Lakini nimesimama kwa kanuni ya 42 fasili ya 9 (d).

Mhe. Spika, sihitaji kuisoma kanuni hiyo ni kanuni maarufu sana. Lakini jambo ambalo nataka kulizungumza hapa jana usiku na leo asubuhi katika vitongoji vya Zanzibar na maeneo yake yamekosa petroli. Nataka kulizungumza suala hilo kama utaniruhusu naomba niendelee. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tumekosa petroli katika viunga vya Zanzibar na maeneo mengine kutoka jana usiku mpaka leo asubuhi katika vituo kadhaa vya petroli. Tulikuwa tunaomba hatutaki kanuni hii tuijadili lakini naomba tamko la serikali. Je, kuna upungufu wa mafuta ili kuwaondolea shaka wananchi au tunataka kuongeza bei

wakati tumeficha mafuta yale. Tulikuwa tunataka tamko la serikali juu ya jambo hilo muhimu sana kwa ustawi wa taifa letu. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante. Naam Mhe. Waziri bahati nzuri ana maelezo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu mtoa hoja kwamba mimi kama Waziri husika wa Taasisi ya *ZURA* lakini kwa suala hili alilosema kwa bahati mbaya sana mpaka sasa hivi sina taarifa nalo yoyote. Lakini kama hali iko hivyo basi aniachie nifuatilie halafu basi nitaweza kusema kile ambacho kipo. Lakini nilikuwa nyumbani mapumzikoni sijapata taarifa yoyote. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nimesimama kwa kanuni ya 45 sijui kama utaniruhusu nisome maelezo binafsi ya Mjumbe.

Mjumbe yoyote anaweza kwa kubali cha Spika kutoa maelezo yake binafsi katika wakati unaofaa kufuatia mpangilio wa shughuli ambazo umewekwa kwa kanuni ya 27 (k) mambo yanayohusu haki, fursa, kinga ya Wajumbe (27) kwa ruhusa yako.

Nataka kuweka *hansard* sawa. Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei) juzi Ijumaa nilikuwa sipo mimi nilienda kusali baadae Baraza likaakhirishwa kuna mambo matatu aliyazungumza. Nataka kuweka sawa alisema nimetumia lugha ya matusi na bahati nimekuja na kamusi jipya hili la 2010 la Kiswahili. Lugha yenyewe alisema neno 'bure' nataka kumpa taarifa akatafute kamusi hili ukurasa wa 36 maana yake nini alisema neno tusi na *hansard* yake ninayo kama utaniruhusu kuisoma Mhe. Spika, nayo niisome.

Mhe. Spika: Endelea kidogo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Neno bure limetafsiriwa ukurasa wa 36 maana yake:

(1) Huduma inayotolewa bila ya malipo
(2) Bila kosa au hatia ya sababu.

Neno la pili alilosema nimetumia lugha ambayo si nzuri 'soza' ukurasa wa 375 akaangalie kamusi hii si maneno yangu kamusi jipya la mwaka 2010. Nataka kumpa darasa kidogo au elimu maana yake nini?

Ni kitendo cha kuchukua au kumaliza kitu ndio maana ya soza. Sasa hilo tusi sijui kalipata wapi na Mhe. Spika, kitu cha mwanzo wazee wangu nyinyi mnanifundisha adabu kumheshimu mkubwa na mdogo.

La tatu maliza akaangalie ukurasa wa 220 unasema kamusi jipya kabisa la mwaka 2010. Maana yake nini Mhe. Spika. Limetafsiriwa katika ukurasa wa 220 maana yake ni kuhitimisha kitendo au kuhitimisha chochote bila kubakiza. Maneno ya hayo sio matusi wala kejeli. Kwa hiyo, nimwambie Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwamba maneno hayo si matusi wala kejeli.

Kwa hiyo nimwambie Mheshimiwa asije kusimamisha gari ambayo haijui mwendo wake itakuja kumtoa meno. Alichokifanya Mheshimiwa anataka kutugombanisha kati ya watu wa Unguja na wa Pemba. Mhe. Subeit Khamis Faki alikuwa akikaa kiti hiki siku zote anachangia ki-Pemba humu ndani. Sasa sijui hili kosa kalipata wapi. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nataka kuweka *hansard* sawa kuwa hakuna neno tusi.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimeweka *hansard.*

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa kwa kuweka sawa. Naomba sasa nimwite Mhe. Naibu Spika ili tuweze kuendelea na shuguli. Mhe. Naibu Spika, karibu uje uchukue nafasi.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii katika Kufuatilia Utendaji wa Shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kutoa Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii katika kufuatilia utendaji wa shughuli za serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa utukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika Mkutano huu wa Tisa wa Baraza la Tisa kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, naendelea kukushukuru na kukupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti, pamoja na wasaidizi wako kwa namna mnavyoliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha demokrasia katika chombo hichi muhimu cha wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 100 (14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2016 inayoelekeza Utaratibu wa Kazi za Kamati za Kudumu ambayo pia inaweka masharti ya kila Kamati kuwasilisha Ripoti ya Shughuli zake mbele ya Baraza lako Tukufu katika Mkutano kama huu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106 (1) ya

Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2016 na majukumu yake ni kama yale yaliyokwisha kuelezwa na Kamati zilizotangulia lakini Kamati hii inafanyakazi na Wizara mbili zifuatazo:-

1) Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo; na

2) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, hivi sasa niko tayari kuelezea muhtasari wa Ripoti ya Kamati yetu na napenda sana kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe waiangalie vizuri taarifa nzima ya ripoti yetu ambayo nakala zake zimesambazwa kwenu nyote. Kama kawaida ripoti yetu imegawika katika sehemu kuu tatu (3) ambapo sehemu ya kwanza inaelezea utangulizi na maelezo ya jumla ya kamati, sehemu ya pili uchambuzi wa kazi za kamati na sehemu ya tatu ni hitimisho na shukrani.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kamati inatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa kanuni, kamati ilitumia utaratibu ufuatao;-

1. Kufanya vikao na wizara pamoja na taasisi zilizo chini ya wizara husika ili kutoa taarifa juu jambo au suala mahsusi ambalo kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa watendaji wa taasisi hizo.
2. Kufanya ziara za ukaguzi katika miradi ya maendeleo, sehemu za kazi na sehemu nyengine ambazo kwa namna moja ama nyengine zinahusika na utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika.
3. Kufanya mikutano na wadau kwa lengo la kupokea maoni juu ya masuala mbali mbali ambayo kamati ilikuwa inayafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati kwa kushirikiana na wizara husika pia ilipata fursa ya kutembelea Mikoa ya Dar es Salaam na Tanga kwa nyakati tofauti ili kujifunza kwa vitendo na hatimae kuweza kuishauri serikali ipasavyo kuhusiana na Sekta za Utalii,

Utamaduni na Mambo ya Kale, Usalama na Afya Kazini, Maendeleo ya Wanawake na Watoto pamoja na Ushirika na Ajira.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti yetu maelezo yanayohusu Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo yanapatikana kuanzia ukurasa wa 4 hadi 25 ambapo inaonesha kwamba utekelezaji halisi hadi kufikia Disemba 31, 2017 (nusu mwaka) ni kuwa makisio ya mapato kwa taasisi zilizoruhusiwa kutumia mapato ni asilimia 107. Kwa upande wa mapato yanayoingizwa hazina ni asilimia 71**.** Kamati inatoa pongezi za dhati kwa wizara kwa hatua hii hadi kuvuka lengo na kuzihimiza taasisi ambazo mapato yake yanakwenda hazina kuongeza juhudi, ili kukusanya zaidi na hatimae lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

Sekta ya Habari

Mhe. Mwenyekiti, **,** Sekta ya Habari kwa ujumla wake bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi, ili hatimae iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kuhabarisha, kuelimisha na kuiburudisha jamii. Licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na watumishi waliomo kwenye Sekta ya Habari, kamati imebaini kwamba bado utendaji wao wa kazi umekuwa unakumbwa na vikwazo kadhaa katika kufanikisha majukumu yao kwa ufanisi ikiwemo mazingira magumu ya kufanyia kazi, uhaba wa vitendea kazi vya kisasa, wataalam, mafunzo katika maeneo yao ya kazi na maslahi yasiyoendana na ukubwa wa majukumu yao kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inalipongeza Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) na Serikali kwa ujumla kwa kupata mitambo mipya ya kisasa pamoja na ukarabati mkubwa wa studio za redio

na *Karume House*. Uchambuzi kamili kuhusiana na *ZBC* unapatikana katika ukurasa wa 6 - 8.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inatambua kwamba majukumu makuu ya shirika hili ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Mbali ya majukumu hayo, shirika ni mdomo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kuiweka karibu na wananchi kwa mustakabali wa nchi hii. Kwa mantiki hiyo, kamati inaitaka *ZBC* ijitambue kwamba ni vyombo vya utangazaji vya Taifa ambapo bado wananchi wengi wanapenda kuangalia na kuisikiliza. Hivyo basi, pamoja na ushindani wa vyombo vya habari uliokuwepo, *ZBC* inapaswa kuendeleza "*tone"* yaani lafudhi yake ambayo imekuwa ikiendeleza hadhi yake kwa muda mrefu sasa pamoja na matumizi ya lugha kwa ufasaha.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kuna baadhi ya watangazaji bado usomaji na utangazaji wao hauridhishi kwa kudododosa dodosa baadhi ya maneno. Pia, kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko kadhaa yanayohusiana na nyimbo, vipindi na baadhi ya maudhui yanayooneshwa au kusikilikana kwamba hayana au hayatufunzi maadili mazuri kwa utamaduni wa Mzanzibari na Tanzania kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo kamati haikuridhika nayo na changamoto kuhusiana na *ZBC* ni pamoja na hali ya utunzaji na usafi wa vifaa vipya pamoja na ujenzi wa jengo jipya Pemba. Aidha, mwenendo wa ajira hasa *ZBC TV* ambapo huwaajiri wafanyakazi wapya na kuwaacha vijana wanaowatuma kwa kujitolea kwa kipindi kirefu pamoja na kutokuwalipa posho ipasavyo na kwa wakati wafanyakazi wanaohudhuria katika Mikutano ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaiagiza *ZBC* kuweka mpango maalum wa kuwapa mafunzo watangazaji wake, ili kupunguza tabia ya kukosea kosea na kudododosa kwa baadhi ya watangazaji wake

pamoja na kusawazisha deni la malimbikizo ya mafao ya wafanyakazi wake Unguja na Pemba na kuhakikisha kwamba inawalipa posho ipasavyo na kwa wakati wafanyakazi wanaohudhuria katika Mikutano ya Baraza la Wawakilishi.

Shirika la Magazeti ya Serikali

Mhe. Mwenyekiti, maelezo kuhusiana na Shirika la Magazeti ya Serikali yanapatikana katika ukurasa wa 8 -11 ambapo kamati yangu imebaini kwamba shirika limefanikiwa kubadili muonekano wa gazeti na kuwa na mvuto zaidi pamoja na kuongeza kurasa kutoka kurasa 16 hadi 24.

Mhe. Mwenyekiti, kutokuwa na uhakika wa idadi ya nakala za uchapaji, gazeti kushindwa kufika Dar es Salaam na Mikoani kwa wakati, kufa kwa soko la Zanzibar Leo Tanzania Bara, kukosekana kwa matangazo ya biashara kutoka Tanzania Bara, ni miongoni mwa changamoto na mambo ambayo kamati haikuridhika nayo kuhusiana na shirika hili ambayo mengi yamekuja baada ya uamuzi wa kuchapisha gazeti hili hapa Zanzibar. Mhe. Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe waziangalie vizuri changamoto hizi katika ukurasa wa 9.

Mhe.Mwenyekiti, **k**amati inaliagiza Shirika la Magazeti ya Serikali liimarishe Kitengo chake cha Biashara, Masoko na Matangazo ili kuhakikisha kuwa soko la Zanzibar linaimarika Tanzania nzima. Aidha, shirika lihakikishe gazeti lake la Zanziabar Leo linaongeza zaidi habari za michezo hasa mwenendo wa Ligi Kuu ya Zanzibar na Ligi Kuu ya Muungano ambapo Simba inaongoza mpira wa miguu ikiwa ni njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba gazeti linanunuliwa kwa wingi hapa nchini kwetu.

Idara ya Habari Maelezo

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitembelea Makao Makuu ya Idara ya Habari Maelezo Rahaleo ambapo pamoja na utekelezaji wake wa makujumu ya kila siku, kamati haikuridhishwa na kukosekana kwa mfumo bora wa utunzaji wa kumbukumbu za picha na vielelezo vyengine muhimu kuhusiana na viongozi wetu wa Kitaifa. Aidha, kamati imebaini kwamba utendaji wa idara hii unasuasua na hatimae kuonekana kwamba majukumu ya idara hii yanafanywa na watu ama taasisi nyengine. Vile vile kutokuwa na ushirikiano na mfumo bora wa mashirikiano na vyombo vya habari vya watu binafsi nayo ni changamoto nyengine inayoikabili idara hii.

Mhe.Mwenyekiti, kamati inaishauri idara kufikiria kuweka na kufanyakazi mabango ya kielektroniki katika maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu, ili kusambaza zaidi taarifa mbali mbali zinazohusu serikali na jamii kwa ujumla. Aidha, kamati inadhani ni jambo la busara kwa idara kuweka ubao mkubwa wa picha na matangazo (*display board*) katika Ofisi za Baraza la Wawakilishi Chukwani kama ilivyokuwa hapo kabla huko Kikwajuni.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na Tume ya Utangazaji na taasisi nyengine zinazosimamiwa maelezo yake yanapatikana katika ukurasa 13 - 16. Kamati ilipata fursa ya kukutana na wamiliki wa vyombo vyote vya habari hapa Zanzibar pamoja na kutembelea baadhi ya vituo binafsi vya Matangazo ya Redio, Redio Jamii na Televisheni ambapo kwa ujumla kamati imegundua kwamba katika vyombo vya habari vya watu binafsi kumekuwa na ufanisi wa kazi na vimejipanga vizuri. Hivyo, kamati ina wasiwasi kwamba kutokana na mwenendo uliopo hivi sasa, vyombo vya serikali vinaweza kukimbiwa na wasikilizaji na watazamaji wetu.

Mhe. Mwenyekiti**,** gharama kubwa za umeme pamoja na mlolongo wa kodi, baadhi ya wakati kutokushirikishwa vyombo vya habari vya binafsi katika shughuli nyingi za serikali zikiwemo

ziara za viongozi wakuu wa serikali, ni miongono mwa changamoto zilizolalamikiwa wakati kamati ilipofika katika sehemu zao za kazi. Aidha, Mhe. Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa sana na wamiliki wa baadhi ya ving'amuzi ambao huwakosesha wateja wao kuona Televisheni ya Taifa ya Zanzibar *(ZBC TV*) mara tu baada ya kumalizika kwa muda wa malipo ya kila mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, **k**amati inaiagiza Tume ya Utangazaji iwasiliane na taasisi husika ili kuhakikisha kwamba waandishi wa habari kutoka vyombo binafsi na wao wanashirikishwa katika ziara za kikazi za viongozi wakuu wa kitaifa japo kwa zamu pale hali inaporuhusu.

SEKTA YA UTALII

Mhe. Mwenyekiti, **m**aelezo yanayohusiana na Seka ya Utalii yatapatikana kuanzia ukurasa wa 17 - 20 ndani ya ripoti yetu. Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imegundua mapungufu kadhaa ambayo yanaleta changamoto kubwa katika sekta nzima ya utalii. Takriban hoteli zote zinakabiliwa na tatizo la miundo mbinu ikiwemo tatizo kubwa la ubovu wa barabara, maji safi na umeme usiokuwa wa uhakika, kukosekana kwa takwimu sahihi za wageni wanaoingia nchini kwa shughuli za kitalii nalo limetajwa kuwa ni tatizo linachangia upotevu wa mapato.

Mgogoro wa wananchi wa Paje na Warusha Vishada vya Michezo ya Baharini (KITE)

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilifanya ziara maalum ya kuwatembelea wananchi wa kijiji cha Paje ambao wanalalamikia kutokupata sehemu ya malipo kutokana na shughuli za urushaji wa vishada vya baharini inayofanywa na wawekezaji na wanamichezo wa mchezo huo. Hali hii inatokana na kuwa wananchi wa Paje

wameacha kufanya shughuli zao za kiuchumi walizokuwa wakizifanya baharini ikiwemo kusokota kamba (vyau). Kwa wale watu waliokuwa hawavijui vyau ni sehemu watu wanazika makumbi yao wanapata usumba ndio vinaitwa vyau kwa watu wa pwani tunaishi tunajua, utafutaji wa pweza (bwachi) na upandaji wa mwani, ili kupisha mchezo huo ikiwa ni njia moja wapo kuunga mkono shughuli za kuendeleza utalii hapa nchini. Hata hivyo, wananchi wa Paje hivi sasa wanalalamika kwamba hawafaidiki na chochote kwa muda mrefu sasa huku warusha vishada wakiendelea kutononoka kutokana na mapato hayo ambapo hujipatia dola 20 kwa kurusha kishada kimoja kwa saa moja, mapato ambayo hayana kodi yoyote inayoingia serikalini. Mhe. Mwenyekiti, kamati inadhani hali hii ikiachiwa kuendelea inaweza kuzusha mgogoro mkubwa hapo baadae na kuleta athari mbaya kwa wanakijiji, wageni na serikali kwa ujumla. Ombi letu la kamati wakae pamoja ili kuliondoa tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuijengea uwezo kamati hasa katika masuala ya utalii wa ndani Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Wizara iliandaa ziara ya kujifunza katika Bodi ya Utalii Tanzania *(Tanzania Tourism Board – {TTB})* Dar es Salaam, Hifadhi ya Taifa Saadani Tanga, Mapango ya Amboni - Tanga. Kwa kweli ziara ilikuwa ya mafanikio kwani iliwawezesha wajumbe kufahamu jinsi wenzetu wanavyofanya na walivyojipanga kuendeleza sekta hii. Kamati imejifunza mengi kutokana na ziara hizo ikiwemo:-

- Umuhimu mkubwa wa kuimarisha utalii wa ndani kwani una nafasi nzuri ya kuongeza pato la Taifa.
- Umuhimu wa Kamisheni ya Utalii kuwasiliana na Wizara ya Elimu, ili kuangalia uwezekano wa kuwepo kwa mtaala wa utalii na hatimae kufundishwa katika skuli za msingi kama wanavyofanya kwa baadhi ya dkuli huko Tanga.

- Kuanzisha ushirikiano wa Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar na Hifadhi ya Saadani kwa kubadilishana watalii kwa lengo la kuzitangaza kiutalii pande zote mbili.
- Kuendeleza uhifadhi wa uoto wa ssili pamoja na viumbe hai katika hifadhi zetu ikiwemo misitu na magofu yetu tuliyokuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti**,** ukosefu wa nishati ya mafuta ya petroli mwishoni mwa mwezi wa Disemba mwaka jana kulipelekea usafiri wa barabarani kuwa mgumu katika kipindi hicho na kulipelekea athari kubwa za kijamii na kiuchumi. Baadhi ya watalii waliakhirisha safari zao za kuja Zanzibar na wengine waliokwisha kutangulia walibadilisha ratiba zao za ndani na kusababisha hasara kubwa ya mapato ambayo tulikuwa tunayategemea katika nchi yetu. Baadhi ya wageni walikosa ndege na kuakhirisha safari baada ya gari walizokuwa wakitegemea kuwachukua kutoka hoteli hadi Uwanja wa Ndege kukosa mafuta na kusababisha hasara kwa ma-*agent* wao. Mhe. Mwenyekiti, kamati ina wasiwasi kwa nini tatizo kama hili litokee katika mwezi wa Disemba, ingawa leo limeanza tena maeneo mbali mbali katika Unguja yetu hii tuliyokuwa nayo, mwezi ambao sote tunafahamu kwamba wageni wengi huwa wanatembelea Zanzibar kwa mapumziko ya *christmas* na mwaka mpya. Kamati inaishauri derikali kuitafakari kwa kina kadhia hii kwa nini itokee wakati kama huo.
Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa maagizo ya kamati kwa kamisheni hii ni kwamba ihakikishe Sheria ya Utalii Nam. *7* ya mwaka 2012 inayoweka masharti ya kuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijiji ambapo kila mwekezaji anapaswa kuchangia asilimia moja (1%) ya mapato yake inatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Utamaduni, kamati hairidhiki na matumizi yasiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili na filamu zisizo na maadili kama ripoti yetu tulivyofafanua ukurasa wa 21-23.

Aidha, kamati haikuridhika kabisa na kusuasua kwa ujenzi wa jengo la Beit el Ajaib ambayo ni roho ya historia ya Mji Mkongwe na Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, **k**amati kwa mara nyengine tena inaendelea kutoa pongezi zake za dhati kwa Timu ya Taifa ya Mchezo wa Mpira wa Miguu Zanzibar (*Zanzibar Heroes*) baada ya kufanikiwa kushinda na hatimae kupata nafasi ya Makamu Bingwa katika shirikisho la soka *Senior Challenge Cup* mwaka 2017 yaliyofanyika nchini Kenya ambayo yaliandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika Mashariki na Kati *(CECAFA).* Aidha, Timu ya Mpira wa Ufukweni (*Zanzibar Sand Heroes*) nayo imefanikiwa kupata ushindi wa kwanza katika mashindano ya *Copa Beach Soccer* yaliyofanyika Dar es Salaam. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa timu zetu hizi kutokana na mafanikio na ushindi huo mkubwa ambao umeiletea sifa kubwa nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na pongezi hizo kamati inalia na ufinyu wa bajeti inayotengwa katika sekta hii**, w**izara na serikali kwa ujumla inafahamu kwamba timu zetu zinashiriki mashindano ya kimataifa kila mwaka wakati hivi sasa hali ya fedha za michezo zinazotengwa ni kidogo na hazikidhi mahitaji ya kuvisaidia vilabu vinavyoshiriki michezo ndani na nje ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na bajeti ndogo inayotengewa Baraza la Michezo, watendaji wa Baraza hilo wanabakia kuwa ombaomba hasa kwa wafanyabiashara hadi kufikia hatua ya mfanyabiashara mmoja fulani kuisaidia *BTMZ* wakati wa mashindano ya *Senior Challenge Cup, 2017* na baadae kulazimisha atangazwe ndani ya Baraza la Wawakilishi kitu ambacho ni kinyume na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, **k**amati inamalizia uchambuzi wa wizara hii kwa kuiagiza kuongeza bajeti katika Sekta ya Michezo, ili kuimarisha vilabu na wanamichezo wetu hasa wale wanaoshiriki katika mashindano ya Kimataifa na kujiepusha na mtindo wa kuwa ombaomba.

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, **m**aelezo kuhusiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto yanapatikana kuanzia ukurasa wa 24 – 43 ambapo kamati inatambua kwamba majukumu makubwa ya wizara hii ni kuratibu program za uwezeshaji wananchi kiuchumi, kuimarisha Vyama vya Ushirika pamoja na kushajihisha haki na usawa wa kijinsia. Vile vile, kamati inatambua shughuli za kuratibu na utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali ambazo nazo zinatekelezwa na wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kamati iliarifiwa kwamba kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, iliidhinishiwa jumla ya shilingi 14,456,640,000 kwa ajili ya utekelezaji wa program na majukumu ya wizara. Pia wizara ilikadiriwa kukusanya Tsh. 891,078,000 na hadi kufikia Disemba 31, 2017 ilikusanya Tsh. 399,712,750 sawa na asilimia 45**.** Kamati hairidhiki na kiwango hiki cha mapato na inaitaka wizara kuongeza juhudi na bidii ya kazi na hatimae kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kama lilivyokusudiwa.

SEKTA YA KAZI

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Kazi ni miongoni mwa sekta muhimu ya wizara hii ambayo inatekeleza majukumu yake kupitia Idara ya Ajira, Kamisheni ya Kazi pamoja na Idara ya Usalama na Afya Kazini. Kamati yetu ilitembelea sehemu mbali mbali za kazi

kuangalia utekelezaji wa majukumu na sheria zinazohusiana na sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, **k**amati yetu imebaini kwamba Maafisa wa Ukaguzi kazi na Usalama wa Afya Kazini hawafuatilii majukumu yao hasa katika Sekta Binafsi, pia kuna baadhi ya maafisa wa Ukaguzi Kazi na Usalama wa Afya Kazini wamekuwa wakituhumiwa kwa ubadhirifu kwa kuwashawishi waajiri kutotekeleza sheria za kazi ikiwemo malipo ya kima cha chini kwa kuwakandamiza wazalendo na kuwapendelea wageni. Kamati pia inaishauri kamisheni iwachunguze vizuri baadhi ya Maafisa wa Kamisheni ya Kazi kutokana na tuhuma za kuwa wasaliti na kuwashawishi baadhi ya waajiri wasitekeleze sheria za kazi pamoja na maagizo yanayotolewa na serikali.

SEKTA YA UWEZESHAJI

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza kwa dhati uamuzi wa serikali wa kuanzisha Idara ya Maendeleo ya Ushirika, Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Mfuko wa Uwezeshaji lengo ikiwa ni kuratibu, kutoa mikopo pamoja na misaada kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla ikiwa ni mtu mmoja mmoja au waliojikusanya kwa pamoja kwa kuunda vikundi vya ushirika na hatimae kuwaondolea umaskini. Hata hivyo, Mhe.Mwenyekiti, kamati haijaridhika na utekelezaji wa azma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imepata fursa ya wananchi mbali mbali waliowezeshwa pamoja na vyama mbali mbali vya Ushirika Pemba, Unguja na Tanga ili kuona ni jinsi gani wananchi wanajikita katika kufanya shughuli mbali mbali za kujiletea maendeleo baada ya uwezeshwaji huo.

Mhe. Mwenyekiti, katika ziara hizo, kamati imebaini kwamba bado wananchi wanahamasika na wana mwamko wa kujiendeleza

na baadhi yao wamefanikiwa katika vikundi vyao. Kamati inachukua fursa hii kukipongeza kwa dhati kabisa Kikundi cha Ushirika wa Kilimo cha Ndimu cha Juhudi Zetu Bwejuu - Dongwe**,** kikundi hiki Mhe. Mwenyekiti, kinapaswa kupigiwa mfano kwa mafanikio makubwa waliyoyapata baada ya kuwezeshwa na wizara. (Maelezo kamili juu ya kikundi hiki yanapatikana katika ukurasa wa 31 wa ripoti yetu hii). Lakini pia Mhe. Mwanyekiti, tunampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wao wote kwa ushiriki wao mzuri katika shughuli zote tulizokwenda bila ya kuchoka.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo ya baadhi ya vikundi kamati yetu inasikitika kwamba hakuna takwimu sahihi za idadi ya vyama au mtu mmoja mmoja waliowezeshwa na Mifuko mbali mbali ya Uwezeshaji (Mfuko wa Kujitegemea, Mfuko wa AK/JK na Mfuko wa Uwezeshaji) ambayo wameweza kufanikiwa kutoka hali ngumu ya umaskini na kuweza kujitegemea yaani *From Zero to Hero.* Aidha, ukosefu wa soko, ukosefu wa mfumo wa usindikaji wa bidhaa na bei kubwa ya pembejeo za kilimo nazo ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili Sekta hii ya Uwezeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, kamati inaiagiza wizara ishirikiane na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ili kuangalia uwezekano wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa mazao au kutafuta mwekezaji au wawekezaji ama kuingia ubia ili kuyahami mazao ya wakulima wetu hasa ndimu na mambo mengineyo.

SEKTA YA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba unanistahamilia na kunivumilia kutumia muda zaidi kuizungumzia sekta hii kutokana na hali halisi ilivyo hivi sasa kutokana na kadhia ya udhalilishaji

wa wanawake na watoto hapa nchini. Maelezo kamili juu ya sekta hii yanapatikana katika ukurasa wa 34 - 43. Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe waiangalie kwa dhati nao watoe changamoto zao hasa tukizingatia kwamba tunaishukuru serikali kwa kupitisha mswada muhimu ambao tukimaliza Baraza hili Mhe. Rais wetu atautia saini uanze kazi juu ya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za kuwaendeleza wanawake na watoto pamoja na program ya kukuza muitikio wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, lakini kamati inashangaa tatizo la ukosefu wa usafiri katika idara hii. Aidha, kamati inasikitishwa sana kwa kukosekana kwa mfumo bora wa ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji kuanzia shehia hadi taifa.

UDHALILISHAJI WA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaendelea kusononeshwa na kusikitishwa juu ya kushamiri vitendo vya ukatili, udhalilishaji wa wanawake na watoto , mapenzi ya jinsia moja na matumizi ya dawa za kulevya katika jamii yetu. Kamati inaamini kwamba vitendo hivi vimeshamiri katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, hivyo sote kwa pamoja tuunganishe nguvu zetu kuvipiga vita na hatimae kuvitokomeza kabisa vitendo hivi. Hivyo, kamati hairidhiki kabisa na baadhi ya watendaji wanaohusika na kushughulikia vitendo vya udhalilishaji wakiwemo Maafisa wa Idara ya Wanawake na Watoto, watendaji wa Jeshi la Polisi, Madaktari na Watendaji wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama wanaoshughulikia kadhia hii.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi za kitaifa za kupambana na vitendo vya udhalilishaji, vitendo hivyo bado vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku Unguja na Pemba, na kwa kuona uzito wa jambo hili, kamati iliweka utaratibu maalum wa

kufuatilia mwenendo wa vitendo hivi katika jamii, Idara ya Maendeleo ya Wanawake pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika muda wote wa mizunguko ya kamati. Mhe. Mwenyekiti, takwimu kamili za kesi hizo zinaonekana katika ukurasa wa 36 na 37 wa ripoti yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza sana juhudi zinazochukuliwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kufanya mikakati ya makusudi ya kuzishughulikia kesi za udhalilishaji kwa operesheni maalum. Kamati imearifiwa kwamba afisi hiyo imo katika matayarisho ya ufunguaji wa kesi za udhalilishaji awamu ya tatu. Zoezi hili linategemewa kuanza mwezi huu tuliokuwa nao wa Februari ambapo jumla ya majalada 290 yanashughulikiwa na wanasheria wa afisi hiyo kwa hatua za mwisho.

Changamoto katika Kesi za Udhalilishaji

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kamati kutembelea Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na sehemu kadhaa kufuatilia kesi hizo, kamati imebaini kwamba kumekuwa na changamoto kadhaa zinazokwamisha kesi za udhalilishaji hapa Zanzibar. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

1) Uwepo wa maombi mengi ya ufutishaji wa kesi za udhalilishaji kutoka kwa wanajamii. Wanajamii wanakwamisha kutokana na kuwa karibu na kesi hizo.
2)
3) Baadhi ya watendewa wa makosa ya udhalilishaji umri wao ni mdogo sana na wanashindwa kujieleza polisi au kutoa ushahidi mahkamani.

4) Kuwepo kwa kasoro katika baadhi ya hati za uchunguzi wa kidaktari (PF3) kwa watendewa na kupelekea kukosekana kwa ushahidi.

5) Kukosekana kwa umahiri wa kutoa ushahidi kwa baadhi ya mashahidi (mashahidi vigeugeu na wakaidi) huwa hawatoi uhakika wa ushahidi wao.

6) Kukosekana kwa maadili kwa baadhi wa watendaji wanaosimamia haki jinai kuwa sio waaminifu baadhi yao wanawarudisha nyuma na wanawakosesha haki isipatikane.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Mhe. Mwenyekiti, ili kuvidhibiti na kuvitokomeza kabisa vitendo hivi, kamati inatoa maoni na ushauri wake kama ifuatavyo:-

1. **Taasisi za Kudhibiti Jamii *(Social Control*) zitimize wajibu wake:**

    - Familia zihimize malezi na maadili mema.
    - Taasisi za Kijamii (Shule na Madrasa) zijitahidi kutayarisha raia wema baadae.
    - Dini zetu ziendelee kutilia mkazo kukataza maovu yasiendelee katika maeneo yetu ya jamii.
    - Kutungwa, kutumika na utekelezaji wa sheria bora zitakazoweza kuwadhibiti ipasavyo watenda maovu hao. Kwa hivyo, naishukuru serikali tumepitisha mswada na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu haitofika mwezi mmoja au miwili Mhe. Rais kwa umuhimu wa hili atatia saini.
    - Watendaji Haki Jinai (*Criminal Justice*) wawe weledi na waadilifu, kwani wakiwa waadilifu mafanikio yatapatikana
2. Kamati inashauri kuangaliwa upya na hatimae kuikata kabisa misingi ya udhalilishaji na vitendo viovu kama tulivyoainisha katika ukurasa wa 40 wa ripoti yetu.

3. Serikali ihakikishe kwamba inaweka watendaji wenye uweledi na wanaofuata maadili ya kazi zao katika sehemu zote za huduma hii.

4. Kuandaliwa kwa mafunzo maalum kwa madaktari kuhusu namna ya kufanya uchunguzi kwa watendewa wa makosa ya udhalilishaji na taarifa zinazostahiki kujazwa vizuri katika PF3.

5. Kukataa maombi yote ya wanajamii yanayokusudia kufutisha kesi za udhalilishaji. Tunaomba haya yakataliwe ili kunusuru jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati kamati ikiwa katika hatua za mwisho za kukamilisha ripoti yake, serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilikuwa tayari imeandaa Mswada wa Sheria ya Adhabu na Sheria ya Mwenendo wa Jinai, miswada ambayo tayari imeshapitishwa na Baraza lako tukufu katika Mkutano huu wa Tisa unaoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, imefurahishwa na kupongeza kwa dhati dhamira ya serikali kuja na miswada hiyo, kwani kamati inaamini kwamba itasaidia kupunguza au kuondoa kabisa wimbi la vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto hasa katika Sehemu ya Kumi na Tatu ya Sheria ya Adhabu ambayo inahusika na Makosa Dhidi ya Maadili ikiwemo kubaka, adhabu ya kubaka kwa kundi, **k**ujaribu kubaka, kutorosha mwanamke, kutorosha watoto wa kike na kiume, kuwezesha ukahaba. Yaani hii kuwezesha ukahaba wanaoendeleza kuwarubuni wakawaweka pamoja makahaba na mengineyo.

Aidha, kamati inapongeza na kuunga mkono Sehemu ya Kumi na Nne inayozungumzia makosa yanayohusiana na ndoa na mahusiano ya kifamilia ikiwemo ndoa ya hadaa, kufunga ndoa

kinyume na sheria, ukatili kwa watoto, kutelekeza mtoto au mtu mwenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Mwenendo wa Jinai, kamati inaunga mkono utaratibu wa kiupelelezi na mahkama ulioainishwa ikiwa ni pamoja na kuziongezea uwezo Mahkama za Wilaya na Mikoa pamoja na kutowapa dhamana watendaji wa makosa hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inamalizia sehemu yake ya pili ya ripoti yake kwa kuitaka wizara hii kwa kushirikiana na kukaa pamoja na Serikali za Mitaa, Jeshi la Polisi, Madaktari, Afisi ya *DPP* na Mahkama, ili kuandaa mkakati wa pamoja wa kushughulikia ipasavyo na kwa ufanisi zaidi kesi zote zinazohusika na udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi inamalizia ripoti yake kwa kuwapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa wizara zote mbili zinazosimamiwa na kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia kamati yetu kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba na kikanuni.

Aidha, kamati inatoa shukrani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi, pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia kamati yetu wakati wote ilipokuwa Kisiwani Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Vile vile, kamati inatambua, kuthamini na kumshukuru Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP*) pamoja na watendaji wake wote Unguja na Pemba, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Mkuu wa Wilaya ya Kati, pamoja na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mchango wao mkubwa wa

kufanikisha majukumu ya kamati hii wakati ikifuatalia kadhia ya udhalilishaji hapa nchini.

Kamati pia inatoa pongezi za dhati na maalum kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga pamoja na Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Tanzania Bara kwa mashirikiano yao ya dhati kwa kuwa bega kwa bega na kamati yetu, wakati ilipokuwa katika ziara za kimafunzo huko Tanga na Dar es Salaam. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa weledi na umahiri mkubwa waliouonesha wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yetu hadi kufanikisha kukamilika kwa ripoti hii. Wajumbe wamefanya kazi nzuri kuhakikisha kamati inaisimamia vyema serikali kwa mujibu wa katiba yetu na maslahi ya Taifa zima. Napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (SHIHATA)	Mwenyekiti
2.Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma	Makamu Mwenyekiti
3.Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mjumbe
4.Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
5.Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
6.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7.Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, pia na kwa umuhimu mkubwa kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndg. Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati, Ndg. Ramadhan Khamis Masoud pamoja na wafanyakazi wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema kamati kutekeleza majukumu yake bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa umuhimu wa kipekee napenda kuwapongeza sana Ndg. Himid Haji Choko na Ndg. Mussa Issa Mussa ambao ni makatibu wa kamati yetu. Kwa kweli makatibu wetu hawa wamejitahidi sana katika kuratibu vikao vya kamati yetu hadi kufikia leo hii na kuwasilisha ripoti yetu. Aidha, kamati yangu inathamini na kupongeza sana mchango wa Ndg. Amina Abeid Hemed ambaye ni mkalimani wa lugha ya alama katika kamati hii.

Aidha, kamati inatoa pongezi za dhati kwa wafanyakazi wote wa vyombo vya habari vya serikali na watu binafsi kwa kazi nzuri na mashirikiano waliyotupa Unguja, Pemba na Tanzania Bara. Wameonesha dhahiri kwamba wao wanajali maendeleo kila tunalolibaini zuri huwa wanalitoa bila ya matatizo, tunawapongeza kwa dhati suala hilo.
Mhe. Mwenyekiti, pia nimesimama hapa kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele, niwapongeze viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi, jimbo, wadi, matawi hadi shina kwa kuniamini, pamoja na wananchi wote wa jimbo hilo kuwa mimi ni mwakilishi wao nawasemea changamoto zao, nachukua ushauri kwao na kuleta hapa kwa maslahi ya jimbo letu na nchi yetu kwa jumla. Najua unapokuwa mwakilishi Mhe. Mwenyekiti, husemei jimbo unasemea Zanzibar nzima kwa faida na maendeo ya nchi yetu.

Mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa usikilizaji mzuri wa Waheshimiwa Wajumbe wakati wote wa uwasilishwaji wa hotuba hii. Nawaomba waichangie kwa ajili ya kuiboresha na kuongeza ufanisi wa utendaji katika wizara hizo na serikali kwa ujumla. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele ambaye pia ni

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Mhe. Mjumbe wa kwanza kuchangia katika ripoti yetu hii Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf wa Jimbo la Chaani, atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahman Rahiym*. Mhe. Mwenyekiti, nakupongeza sana kwa kunipatia nafasi leo hii kuwa mtu wa mwanzo kwa sababu Mwenyekiti mwenyewe mjomba kila siku anaishika namba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesimama hapa kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi. Kwanza niipongeze kamati kwa ujumla kwa kuweka taarifa makini na ya uwazi kabisa, pamoja na changamoto zenye ukweli ambazo wamezifanyia kazi. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana mwenyekiti pamoja na wajumbe wote wa kamati hii kwa kufanya kazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza kwenye wizara moja hadi moja. Nitaanza na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuchangia. Nimeamini kwamba kweli mtu anaweza akakabidhiwa wizara akawa sio mwenye *qualification* za hali ya juu kwenye masuala yale, lakini akawa mtendaji bora na makini na akaiweza wizara. Leo naweza kusema kwamba nathibitisha kiasi kikubwa Waziri wa Wizara hii ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo anafanyakazi kama mtu ambaye ni profesa wa mambo haya ya utalii, kazi ya utalii Zanzibar inakuwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilikaa na wageni tofauti wakaniambia Nadir serikali tumesikia ina- *target* ya wageni laki tano *within* 2020, lakini inaonekana sasa imeshafika kila sehemu wageni wa

kutosha. Vile vile niipongeze wizara nzima kwa sababu najua waziri peke yake hawezi kufanyakazi hii bila ya kusaidiwa na watendaji wake, pamoja na wenye mashirika ya *Tour Operators* ambao wanasaidia nchi, pamoja na mabalozi na watu wengine binafsi wenye kuweza kufanya *marketing* kwa kupitia Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumza mambo machache kwenye wizara hii halafu nitakwenda wizara inayofuata. Kwanza nimwambie Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kupitia wizara nzima, ili aweze zaidi kazi zake ziende vizuri na utalii Zanzibar uwe wenye sifa, kwanza ahakikishe anasimama vizuri na wizara japo mbili kwenda tatu, ikiwemo Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Utalii bila miundombinu mizuri *at the end* utakuja kusemwa tu na utakuwa ni mbaya, kwa sababu haiwezekani mgeni anatoka *airport* anakwenda zake Nungwi, Kiwengwa, Makunduchi au Paje njia zimejaa mashimo, hazina alama na haziko kwenye kiwango zitaleta madhara kwa wageni. Na wengi wanaokuja pengine ni wagonjwa wa migongo, watu wazima hawawezi kuhimili mikiki ya mashimo na gari zinavyokwenda mbio na mara zinapasuka mpira na kusababisha ajali.

Kwa hivyo, ningekuomba zaidi ili usifelishwe kwenye mambo ya utalii kama unavyokwenda sasa hivi, hakikisha kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwenye mambo ya miundo mbinu hususan njia zinazoingia kwenye mahoteli makubwa zitiwe vifusi. Sasa hivi njia ya Nungwi kuendea *Double Tree By Hilton, Smiles Beach Hotel* na nyenginezo hakuingiliki na gari ndogo, kama huna *four wheel* kule hujapita. Sio kule tu mashamba mengi, ningeomba wizara husika mbili. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa sababu ni wizara mama, lakini kupitia wizara ya vikosi inayo mambo yake kwa kupitia taasisi zake za halmashauri ijitahidi nayo kwenye njia ndogo

ndogo ikafanye japo njia za vifusi na mambo mengine mambo yakakaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala hilo hilo la utalii, Zanzibar kwenye mahoteli karibu mengi wananunua maji, fedha wanazokwenda kununua maji ni nyingi sana. Kwa hivyo, ningeomba miundo mbinu ya maji iboreshwe sana kwa wananchi pamoja na mahoteli ili utalii wetu uwe mzuri, wenye mahoteli wasipate matatizo kwa sababu wanalipa kodi kubwa na *expenditure* zao ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la utalii vile vile suala la ulinzi ni muhimu, ningemuomba Mhe. Waziri akaongea na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, au yeye mwenyewe kwa kupitia wizara yake akaunda timu maalum zinazotembelea baharini ambazo zitaweza kukamata watu wanaosumbua wageni na kufanya mambo ya uhalifu hapa mjini na sehemu nyenginezo. Hii itasaidia kuweka ulinzi wa hali ya juu kwa wageni na watalii wetu katika masuala ya ulinzi na italeta heshima na mambo mazuri kwenye suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba suala la Beit el Ajaib tulipatie ufumbuzi wake na tupate habari zake, maana yake wengine tunasikia kwamba serikali ndio inayojenga, wengine tunasikia Serikali ya Oman ndio inayotaka kujenga, ukweli haujulikani. Jengo lile katika Zanzibar ndio namba moja ambalo liko kwenye kivutio cha utalii na ni jengo ambalo lina historia kubwa na nzuri. Kwa hivyo, ningeomba jengo lile lifanyiwe marekebisho haraka iwezekanavyo, ili hali yetu ya utalii iendelee kuwa nzuri kwenye upande wa historia, pamoja na majengo yote ambayo tunayo nchini katika hali iliyokuwa mbaya basi yawekwe katika hali iliyokuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeshauri tena kwa Mhe. Waziri kwenye mwezi wa Agosti huko tuna *World Cup* inafanyika

Russia, lakini 2022 itafanyika Qatar. Kwa hivyo, tungeomba wizara yako muanze kujipanga jinsi ya kwenda kujitangazia kule nchini kwa upande wa Zanzibar, ikiwa kuweka mabango au kuweka kiofisi ili watu katika mizunguko ile mkapata kutangazia Zanzibar kwa sababu dunia nzima itakuwepo pale. Hii inatokana na sio kwenye *World Cup area* tu, pia katika ma-*airport* ya wenzetu au katika sehemu za wenzetu nendeni kama ikiwezekana zungumzeni na mabalozi ili mkaitangaze nchi zaidi. Lakini pia *target* ni sehemu zipi ambazo Zanzibar wateja wake bado hawaji kwa wingi Uzbekistan, Azerbaijan na Kazakhstan, na nchi nyenginezo ambazo Brunei wananchi wake matajiri bado Zanzibar bado hawafiki kwa wingi. Tungeomba utangazie kwa njia hizo ili mambo yaende vizuri.

Lakini nikupongeze vile vile kwa ndege nyingi ambazo zinakuja sasa hivi Zanzibar za *direct live chatter* zile zinazokuja kuleta wageni. Nikupongeze sana uendeleee kuongea na wanaoleta ndege walete nyingi zaidi, na nasikia umefanya maarifa hivi karibuni ndege ya Uturuki itatua mara tano Zanzibar *within* mwezi sita, wa saba. Umeongea nao ninavyosikia na nina uhakika nimesikia kwamba mwezi wa sita kwa mwenendo wako kwamba itatua Zanzibar mara tano *Tariq Share Line.* Lakini ushauri wangu mwengine ningekuomba ukatafuta angalau watu watano, sita kwa kumuomba Mhe. Rais mkaweka basi watu. Kuwateua Mabalozi wa heshima ili kutangazia nchi au wale ambao wamefanya kazi kubwa kuitangazia nchi yetu kwa masuala ya utalii, wapo watu ambao wana uzoefu naamini ukikaa wewe na Mhe. Rais ukimuomba mnaweza kuwateua wakatusaidia kwenye masuala ya *marketing* na masuala ya kuleta utalii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye suala la *ZBC* kwa sababu haya yote ninayoyazungumza kwenye kamati yamo nimeshayasoma nimeona niifunge ni kubwa. Nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweka vifaa vipya kwenye Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo lakini bila ya wafanyakazi wa *ZBC* hata

ikiwekwa mashine ya almasi haitaweza kwenda bila ya watendaji. Mimi ningeomba changamoto iliyomo humu ndani wafanyakazi hawa kwa mujibu wa sheria wanatakiwa walipwe kwa siku *amount* nafikiri sijui kama si hamsini elfu, lakini kinachosikitisha kwamba wizara hii inalipwa fedha taslimu na Baraza la Wawakilishi, lakini pesa zao hawalipwi kwa mujibu wa sheria inavyotakiwa. Wana kazi nzito kama tunavyowaona mbele wanasimama muda mrefu, wanatumia macho yao kupitia darubini kutumurika sisi wanaumia, lakini pesa zao hawalipwi.

Mhe. Mwenyekiti, watendaji wote Baraza la Wawakilishi pamoja na vyombo vya ulinzi wanalipwa pesa zao kwa mujibu wa sheria kila siku wakiondoka. Kwa nini waandishi wa habari hawalipwi wakati tunalipa Baraza la Wawakilishi. Ningeomba basi Baraza la Wawakilishi tuwalipe sisi wenyewe kama tunavyowalipa watu wengine fedha zao ili kuepuka na usumbufu. Kama kuna tatizo basi Mhe. Waziri aje atueleze lakini haipendezi kwamba watu wanafanyakazi pesa zinalipwa halafu wakatwe au waambiwe watapewa siku nyengine, ni mambo ya kusikitisha.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mtu anasababisha masuala kama haya basi sisi itabidi tutakuja kumtaja tu humu ndani, mambo anayoyafanya kwamba si mazuri na hii ni dhulma, mtu afanye kazi kwa mujibu wa haki alipwe asikae akalipwa nusu, akalipwa robo pesa yake, alipwe kwa mujibu alivyoahidiwa alipwe pesa zake. Ningeomba Ofisi ya Baraza la Wawakilishi isimamie suala la watu hawa kulipwa pesa zao kwa mujibu wa *time* zinavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *Zanzibar Heroes* niwapongeze sana ningemuomba Mhe. Waziri niliahidi hapa mimi mwenyewe kwamba tutakuja kukutana nao kuwapongeza, kukaa nao pamoja na kula nao chakula cha mchana ili kubadilishana mawazo. Ni lini sasa Mhe. Waziri atakuja kutwambia kabla Baraza hili kufungwa tutakuja kula nao. Mimi nilisikia Jumamosi ile iliyopita, naomba

kabla ya kufungwa Baraza la Wawakilishi ikiwa Ijumaa hii hapa ya kesho kutwa au Jumamosi basi tuje kukaa nao hapa ndani tubadilishane nao mawazo, tule nao kama tulivyoahidi tutimize ahadi yetu kama alivyotimiza Mhe. Rais kwa kuwa fedha tumeshazilipa za kuwasaidia chakula tuliweka pembeni. Sasa ningeomba Mhe. Waziri ulisimamie kabla kufunga Baraza hili tuje tukae nao pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nina nia ya kuunda Kamati Teule kwenye wizara inayofuata. Mhe. Mwenyekiti, naenda kwenye Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na Wizara nzima nao wanafanyakazi nzuri lakini kuna mambo machache, nina nia ya kuunda Kamati Teule kupitia Kanuni ya 111. Hapa kuna suala la ajira na mambo ya nje. Kamati imebaini kwamba hadi kufikia tarehe 30 Disemba, 2017 idara kwa kushirikiana na wakala binafsi wa ajira Balozi za Tanzania zilioko nchini, wamekwenda wamefanikiwa kupata ajira 620. Mhe. Mwenyekiti, nchi zilizotajwa hapa ni Bahrain, Maldives, Oman, Qatar, Saudi Arabia na Umoja wa Nchi za Kiarabu.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mwenyekiti wa Kamati hii akafanya ziara kwenye hizi nchi kwa kushirikiana na kamati aende akahakikishe vizuri kwa sababu naweza kusema ripoti hii iliyokuwemo humu sio sahihi. Mimi nitatoa mfano nilikuwepo Oman hivi kipindi cha karibuni nilizungumza na Balozi wa Tanzania nchini Oman. Wazanzibari waliopo nchini Oman peke yake ni 9,000 wanaofanya kazi ndani ya Oman au zaidi ya wafanyakazi 9,000 lakini takwimu halisi humu haimo.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru na niipongeze sana Serikali ya Zanzibar kwa ushirikiano mzuri na Serikali ya Oman, pia niipongeze sana Serikali ya Oman na wananchi wake wote ambao wamekubali kuwapokea ndugu zetu wa Zanzibar kuweza kuwaajiri kule na kuwa nao. Hivi nakwambia mfanyakazi wa

chini kule analipwa sh. 410,000/- ya hapa, huyo ni mtendaji wa ndani, tiketi bure, matibabu bure na chakula bure, ukifanya hesabu bilioni 3 na milioni 600 kwa mwezi na mwaka bilioni 45 wanalipwa Wazanzibari wanaofanyakazi ndani tu ya nyumba, sikwambii Wazanzibari ambao wana *post* kubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kuhusiana na ajira. Juzi nimekwenda nimefanya *research* kuna hoteli *Beach Club* hapo Hyatt kuna wafanyakazi 47 ni *restaurant* tu cha kushangaza na kusikitisha Wazanzibari watatu tu ndio walioajiriwa na hapa ndio panapo nia ya kutaka kuunda Kamati Teule niliyoizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha Zanzibar hoteli ina wafanyakazi 400 unaambiwa kuna Wazanzibari 10 tu ndio walioajiriwa ndani. Vijana wamekaa wanakula unga, kuna vijana waliokaa mabarazani, wanadada wamekaa mabarazani, ndugu zetu wamejaaa hawana kazi yoyote wanachanganyikiwa, lakini ajira wanapewa Wakenya, wanapewa watu kutoka India, wanapewa watu kutoka Uingereza na nchi zetu zilizo karibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani kwamba Zanzibar tumezungumza mwanzo wazalendo wapewe *priority* wapewe kazi. Leo kazi wanapewa watu wengine mpaka za kulinda, kazi za kukosha gari, kazi za ulinzi, kazi za kusafisha hawapewi Wazanzibari imekuwaje mambo haya. Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kupitia kanuni ya 111. Moja, Baraza linaweza kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo fulani. Mbili, Kamati Teule itapendekezwa kwa njia ya hoja itakayotolewa na Mjumbe na kuamuliwa na Baraza na taarifa ya hoja hiyo haitajadiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeleta *concern* hii kwa sababu kuna haja sasa ya Zanzibar tukaunda Kamati Teule kupitia kiti chako ili kuweza kusema sasa kuna Wazanzibari wangapi hawajaajiriwa, wangapi wameajiriwa na wangapi ambao wanatoka nje ya nchi wameajiriwa. Wazanzibari kazi hawapewi wanadharauliwa,

wanaambiwa hawawezi kazi wakati kazi wanaweza, wapo vijana shupavu, wanawake shupavu wa kufanyakazi lakini cha kushangaza kazi zile wanapewa wengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kanuni hiyo ya 111, sasa naomba kutoa hoja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kukaa na napongeza uongozi mzima kwa ujumla. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakushukuru sana kwa mchango wako, lakini pamoja na hiyo hoja yako uliyotoa nimekufahamu vizuri sana Mhe. Nadir, unasema unataka kuunda Kamati Teule kupitia Baraza. Mhe. Mjumbe, tumekufahamu kama ipo haja ya kufanya hivyo, basi Baraza litafanya ikiwa ipo haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii, ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu kuichangia ripoti hii Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze pia kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu ambao mimi ndio msemaji wao hapa, mtetezi wao na niweze kutoa mawazo na fikra kuweza kuishauri serikali kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar, kwa kadri na uwezo wangu ninavyofahamu kwa kutumia akili, ubunifu, au njia yoyote ambayo inayostahiki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze pia kwa kumpongeza Mhe . Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kuonesha ushirikiano wa pamoja. Lakini pia nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo hasa katika mafanikio mazuri waliyoonesha wakati wa Tamasha la Sauti za Busara ambapo Zanzibar imepata sifa kubwa na wageni wamekuja. Lakini pia kiutamaduni vikundi vingi ambavyo

vimeweza kushiriki na mimi nikiwa mdau katika uongozi huo basi kwa nafasi hii, ili kuhakikisha kwamba nachukua fursa hii pia kuwapongeza wananchi wa Zanzibar na hasa wale wenyeji wa Mji Mkongwe kwa kufanikisha hili.

Mhe. Mwenyekiti, juzi mtu alinishangaza sana aliponiambia kwamba Zanzibar imetajwa mpaka Hong Kong katika taarifa ya habari kwa mambo mazuri kama haya yanayofanyika nchini kwetu, basi tuseme tu matamasha kama haya sasa sio ya Wazanzibari ni yetu sote na yanatuletea sifa sana. Kwa hivyo, namshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza sana watendaji wa Wizara hizi zote mbili, Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa sababu mambo ni mengi wana vitu vingi, *resources* ni chache lakini wanatumia njia nyingi za ubunifu ili kuweza kufanya yale wanayoyataka.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nitoe ushauri wangu kwa mambo ya ripoti niliyoyasoma au niliyoyasikia na yale ambayo naamini yataweza kuwasaidia. Kwanza katika kupitia ripoti kwenye ukurasa wa 20 nimesikitika kusoma kwamba wakati mafuta yalipoadimika mwaka 2017 naomba niinukuu hii ripoti.

"Baadhi ya kauli zilizotolewa na wageni baadhi ya wakati huo sio nzuri zenye kuwavunja moyo watalii wetu, mfano mzuri ni wakati ule ule wa kadhia ya ukosefu wa petroli, mtendaji mmoja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Mafuta *(ZURA)*, wakati akifanya uchunguzi wa mafuta katika sheli ya Kijangwani alimtolea maneno ya fedheha mtalii kama alivyonukuliwa na mmoja wa watembezaji wa watalii wakati akitoa ushuhuda wake wa kamati. Alisema:

"Next time do not do your holiday in Zanzibar". Maana yake huyu mtendaji wa *ZURA* alimwambia mtalii mara ya pili usije Zanzibar kufanya likizo yako ya mapumziko.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili la lugha sio jambo geni, lakini nimekuwa nikilisema mara nyingi hapa nikichangia hasa kwa watendaji ndani ya serikali yetu. Inawezekana tabia hii wakati mwengine haipo katika *junior officers*, pengine ni wafanyakazi ambao ni *senior* ndani ya serikali wamekuwa na mwenendo wa kutoa maneno au kauli ambazo haziendani. Mimi naomba sana watu ambao wanatoa kauli kama hizi wakati mwengine za makusudi kujionesha kama wao wanaipenda Zanzibar zaidi na kuwaambia wageni wetu ambao tunawategemea katika uchumi wetu basi watandikwe viboko japo 12, waletwe kule Kiinua Miguu ili waanze kujifunza nini cha kusema na nini hakifai.

Mhe. Mwenyekiti, pia lugha kama hizi naomba sana katika maeneo ambayo unapoingia hasa *airport* pamoja na watendaji wa serikali wanapofanya ziara zao katika mahoteli hasa upande wa *labour* wengine upande wa *ZSSF*, wengine upande wa *ZRB*, na wengine wote wanaosimamia wajitahidi sana katika lugha zao pamoja pia na viongozi wa Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri kitu kimoja kwa sababu Mhe. Waziri ndie anayetoa leseni hasa aanze mchakato wa mtendaji yeyote atakayekwenda serikalini anapofika katika hoteli ahitajike kujaza fomu maalum, mimi jina langu hili, sababu ya kwenda pale atasema kaenda kufanya uchunguzi au kuingia. Kwa sababu kuna wakati mwengine inawezekana watu wanachukua *advantage* ya nafasi zao za kazi kwenda kuingilia maeneo na kuwasumbua wawekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo kutolewe fomu maalum, jina la mtendaji ndani ya serikali, sababu ya kwenda pale, angalau tuweze kumjua na kuna utambulisho kwa sababu haya mabuku

yanayowekwa yanakuwa wakati mwengine ni mabuku kwa ajili ya ulinzi na usalama.

Mhe. Mwenyekiti, tuanzishe fomu maalum, haiwezekani kuwa wawekezaji wanalalamika juu ya lugha halafu ndani ya serikali tukae kimya, haiwezekani mtu mmoja akatutia doa wote ndani ya serikali yetu iliyoko madarakani ndani ya Chama cha Mapinduzi. Wazanzibari wote lugha hizi zinaandikwa kwenye mitandao kama hamuoni fuatilieni kwenye *facebook* angalieni kwenye *web-site* zilizoandikwa masuala ya *tourism* yanatajwa wanaandikwa Polisi, *Immigrations,* watendaji kila mmoja wataandikwa humo ndani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo hizi lugha tujitahidini sana na Mhe. Waziri uendelee kuwasemea hasa vijana wetu, siku hizi ukienda pale Forodhani unakuta vijana wanakimbia mbio wanapiga kachu ndani ya bahari na huku wageni wanapita, watoto, waswahili, ili mradi balaa na sehemu yenyewe hairuhusiwi. Wakati mwengine polisi wanafanya ziara za kupita maeneo hayo wageni wapo lakini hawachukuliwi hatua zozote za kisheria. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo maeneo kama hayo yote tuangalie jamani.

Lakini pia nitoe masikitiko yangu kwa sababu haya masikitikiko ni sehemu ya kuchangia. Mwaka jana nilizungumza kwamba lugha ya kusema *low season* iachwe kutumika tuanze kutumia *green session*. Mhe. Waziri utakapokuja hapa mwezi wa tisa utwambie mwaka huu mwezi wa Aprili na Mei ni sehemu ngapi umeweza kufanyia kazi ili tuanze sasa kuita *the green season* katika maeneo haya ambapo wageni wanapungua.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilishauri suala la *visa* kwa ajili ya *East African Residence* wazungu au raia aliyetoka nje ambao tayari wamo ndani ya nchi za Afrika Mashariki kama mtu anafanya kazi katika sehemu ya kampuni kubwa Nairobi, Kampala, Bujumbura au Kigali wawe wanapotaka kuja Tanzania au Zanzibar tuwaondolee *visa fee.* Sisemi wasilipe *visa,* lakini *visa*

tuwatambue wameingia hapa je, katika mchakato huo umefikia wapi. Nilishauri pia katika mwezi mtukufu wa Ramadhan mgeni yeyote atakapoingia *airport* anapewa karatasi ya *do and don't,* mambo ya kufanya unapofika Zanzibar na mambo yaliyokuwa hayastahiki kufanywa yaandikwe kwa lugha zaidi ya nne Kifaransa, Kiingereza, Kijerumani, Kitaliana, Kihispaniola ili mgeni ajue utaratibu wake anapokwenda Mji Mkongwe haya ni maeneo mavazi yako unatakiwa uvae ya stara. Mhe. Mwenyekiti, mwezi mtukufu unakuja umefikia wapi na mwaka tayari umeshapita.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme pia jengo letu la Kamisheni ya Utalii halipo katika hali nzuri, Utalii wa Zanzibar na jengo la kamisheni haliendi sambamba, kutoka hali iliyokuwa nje na mpaka ndani, sihaba hao watendaji hawajafulia maana yake wanapendeza kwa sababu mavazi yao wanavaa nguo zao wenyewe. Lakini ukiangalia jengo ni bovu nafikiri lile jengo hata si mali ya Wizara yenu ni mali ya Shirika la Bima. Sasa lini mtafanya mpango kuwapatia jengo lenye ofisi inayostahiki ili nao pale wajigambe na sisi wenyewe tujigambe.

Mhe. Mwenyekiti, kaangalieni ofisi iliyokuwa ya *TTB* sasa hivi Dar es salaam, ndio iliyokuwa jengo la Ubalozi wa Marekani wa zamani. Kaangalieni Kamisheni ya Utalii ilivyo yaani inasikitisha sana ipo huko nje ya mji, ofisi zote zipo mjini *fine,* si tatizo kuwa nje ya mji, lakini angalu ziwe zina sura na hadhi zinazostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar Leo gazeti la serikali tangu mwezi Mei, 2017 halifiki, serikali nimesema hapa mchapishe magazeti 500 Zanzibar, 2,000 mkachapishe Dar es Salaam mnatuma kwa *email* gazeti zima saa 11:00 jioni. Leo magazeti yote hapa yamekaa yanafungiwa maandazi, aibu gazeti la Zanzibar wenzetu Bara ndugu zetu hawaoni. Kwa hivyo sasa hivi tunafanyaje, hata hayo matangazo ya makampuni yote makubwa yaliyokuwa yanalipiwa kwenye Zanzibar Leo hatupati, *tender,* nini wasome

hawaoni. Zanzibar Leo linaishia hivi sasa kule kwenye makapu na maboksi. Chapisha magazeti 500 Zanzibar kwa wakala wako wa serikali, 1,000 chapisha Dar es Salaam unalipia utauza utapata matangazo, gazeti kama haliingizi pesa halina maana japo ni la serikali litatutia hasara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi nashauri gazeti mchapishe kopi kadhaa Tanzania Bara, kopi kadhaa Zanzibar halafu tuone. Gazeti pia linabadilika kila sura na kila mwaka linakuja tofauti, leo lina manjonjo, sio ukifanya manjonjo mara moja linabaki hivyo hivyo, tuwe tunaona manjonjo tofauti mle ndani. Gazeti ni zuri mimi nashukuru linatoka ni safi lakini manjonjo yaendelee. Gazeti letu ni moja la serikali manjonjo yaendelee kufanywa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda niwapongeze watu wa Shirika la *ZBC* hasa katika kipindi cha usiku cha Taarab Asilia, nafurahi sana nikisikia ile taarab usiku nikiwa nyumbani, nikiwa kwenye gari wanapiga vipindi kama hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia niipongeze sana serikali kwa studio mpya pamoja na wizara na waandishi wetu pia wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini wanajitahidi. Mhe. Mwenyekiti, nimpe taarifa Mhe. Waziri nasikia watu wake wanaosimamia kipindi cha Mawio wameweka huko mkakati kwamba wanasiasa tusitangaziwe vipindi vyetu kwenye Mawio. Sasa waambie watu wako kama wao hawataki kututoa kwenye Mawio, sasa na sisi kwenye bajeti hapa tutakuja kuzuia.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani wananchi wanatoa madukuduku yao kwenye Mawio halafu sisi tusihojiwe kutoa taarifa, *so we need to respond back.* Kwa hivyo, lazima na sisi pia kama tunachapwa kwenye Mawio na wananchi, juzi wananchi wetu wa Kikungwi wamenilalamikia nikahojiwa.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani taarifa yangu iende kwenye Taarifa ya Habari kwenye Mawio isifike mtakuwa mnatuonea sisi wanasiasa. Kwa hivyo, mwambie huyo mhusika wa Mawio na yeye pia ajitayarishe ikiwa ni huko na sisi hapa mawio yake tutakuja kumtandika mwezi wa sita kwenye bajeti tutazuia pesa, hatutaki sisi kuambiwa, sisi ndio Wawakilishi wa Wananchi serikali inakuja hapa kutoa bajeti tunasimamia hizi fedha, haiwezekani sisi mkaweza sasa kutuwekea sehemu gani tusikike, wapi tusisikike, hilo haliwezekani. Sisi ni Wawakilishi wa Wananchi kwa hiyo huyo mtu wa Mawio umwambie huko.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nataka nizungumze suala zima la *Zanzibar Heroes*. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri, Serikali, Rais wetu hasa na Wazanzibari wote kwa jinsi walivyoonesha mapenzi na umoja wakati wa ile michezo ya *CECAFA*. Nikupongeze wewe kama Mhe. Waziri kwa sababu kile kipindi tulikuwa na Mkutano wetu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Dodoma, najua roho yako ilishindwa kwenda huko, lakini ulipiga kotekote au ulikwenda na kurudi nilifurahi sana kukuona kwenye fainali upo uwanjani umependeza ukibeba bendera ya Zanzibar.

Lilikuwa jambo zuri sana nikupongeze sana kwa jambo hilo na uendelee kutumia njia za ubunifu kuhakikisha vijana wetu wa *Zanzibar Heroes* sio baada ya mechi hii kushinda halafu tukawasahau. Nashauri tuwe tunakuona nao kila baada ya miezi miwili mitatu unatembea nao njiani, tuwaone kwenye gari yako Kapteni uko nae karibu, Kocha unatembea tembea nae kwenye chakula cha usiku, wakati mwengine pia unakwenda kuwatembeza katika mahoteli ambayo yapo chini ya himaya yako na wao wakaone wakajifunze. Tunajua wengine wamepatiwa viwanja hapa kujenga basi usimamie kama watahitaji mikopo, u-*facilitate* kuwatafutia mikopo kupitia *PBZ*. Lakini pia wengine kama watataka ajira usimamie katika ajira pia wanazozitafuta kuwe kuna tofauti na waonekane bidii yao na jina walilotuletea

Wazanzibari tunakuwa ni endelevu na kila mmoja apiganie yeye kutaka kuchezea *Zanzibar Heroes*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala zima la *minimum wage* au tutasema iliyotangazwa na Mhe. Waziri mwaka jana kuongeza mapato au fedha kwa ajili ya kima cha chini cha mshahara. Mhe. Mwenyekiti, jambo lolote linapofanyika panakuwa pana changamoto. Mimi nimeshalisema sana sitaki kubishana, sitaki nigombane na Mhe. Waziri na utendaji wake. Naomba nishauri tu katika lile suala ambalo ulilolitoa kutoka shilingi elfu saba ambalo ni katika *skilled and* unsIkilled *labor* ya elfu kumi kwenda mpaka elfu thelathini na shilingi elfu saba mpaka ishirini na tano.

Kama halitenedeki, haliwezekani, halifanyiki linashindwa kupatiwa yaani watu wanashindwa kulipa basi lirudishe lirekebishe hakuna ubaya wowote. Leo haiwezekani nimezungumza kwa mfano watendaji kibao huko ndani wanajenga mtu huwezi kumwambia fundi ukamlipa shilingi elfu thelathini. Kwa hivyo, inawezekana huko watu wanashindwa, sasa kama halitekelezeki haina haja ya kufanya jambo ambalo tunalipeleka, tumejaribu Waziri umekuja na mawazo twende katika mfumo mwengine ujengee utaratibu tu basi. Kwa sababu nimesema hata katika serikali Uwanja wa Mao watu wameshindwa kuwalipa shilingi elfu kumi, sasa hiyo thalathini iko wapi. Ikiwa Serikali ya China imeshaingia mkataba na SMZ kulipa shilingi elfu kumi, elfu ishirini utazipatia wapi. Sasa ina maana hata serikali pia walishindwa kufidia ile *difference* ili ile sheria ifanye kazi na kwa mujibu wa Sheria za Kazi hakuna mtu yeyote au taasisi yoyote yuko *accented.* Kwa hiyo, Mhe. Waziri hata ukija kwangu kuniambia serikali hii italipa kiasi hiki, *private sector* walipe hiki hakuna hicho kitu.

Sheria inabana kama tunakwenda kwenye *private sector* mtu alipwe shilingi elfu thalathini walipwe wote. Sasa ifanyie

marekebisho ni yupi na yupi anaweza akalipwa, yupi hawezi kulipwa. Sasa katika changamoto hii unapoiangalia usilazimishe, njoo chini angalia wapi turekebishe, ina maana inakuwa tunakwenda sambamba kwa pamoja baina ya utendaji kwa sababu humo ndani kuna sekta ya mafuta, kuna sekta ya ujenzi, kuna sekta ya utalii, kuna watu wengine wa chini mazingira yao na majumbani mwao. Kwa hivyo, tunaangalia kwa umoja wetu kila kitu kiende sambamba kwa mujibu wa sheria unayotaka wewe na watu wanachostahiki kiasi gani cha kulipwa.

Mhe. Mwenyekiti, muda wangu bado si unao naona unanitolea macho.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuomba umalizie.

Mhe. Simai Mohammed Said: Naona unanitolea macho sana mara unanitoa nakujua wewe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka nimpongeze sana Katibu Mkuu wa Wizara hii Mhe. Omar Hassan (King) wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, lakini pia Bi. Sabah, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii. Napenda sana umoja wa watendaji unaokuwepo baina ya wizara hii na waziri husika ni mfano mzuri kwa mawaziri wengine, sisemi kama wengine hawana lakini utendaji wao unauona sasa hili ni jambo zuri kabisa. Naomba sana hasa Mhe. Waziri na yeye pia aendelee kuhakikisha kwamba fedha katika utendaji wote katika sekta hii ambayo ni sekta mama ni mtambuka, kwa hivyo tunakuwa tunafaidika kwa pamoja. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza Kamishna wa *Immigration* kwa jinsi siku hizi *Immigration* ukifika *airport* wanakuwa na tabasamu wanacheka, lakini zaidi nguvu ziende katika *point of entries* ili tuwe tunatoa sura nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kumshauri Mhe.Waziri ikiwezekana katika maeneo ya *airport* mpya itakapokwisha basi

kwenye maua ya nje kuwe na milangilangi, mishokishoki, mifenesi ili mgeni akitoka tu nje ya *airport* anapata harufu ya Zanzibar na marashi yake ndio tunayosema.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe sana pamoja na Wajumbe wa Baraza pamoja na watendaji ambao wapo juu wananisikia.

Ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Simai, lakini nilikuwa nakuomba sana usiwe unachangia kwa wasi wasi kwa hofu ya kukutoa. Kama tutakwenda vizuri kwa mujibu wa kanuni zetu basi sifikirii kama nitakutoa. Nakuomba sana jisikie huru changia vizuri usiwe na hofu ya kukutoa.Tukienda vizuri kanuni inafuatwa. Nakushukuru sana.

Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid, atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Abdalla Ali Kombo ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nafurahi na nakushukuru leo kwa kuniona mapema juzi nilikosa lakini leo nipo nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyetuwezesha tukafika hapa tukaweza kuchangia na tukatekeleza majukumu yetu ambayo tumepangiwa kutekeleza. Kwa sababu moja kati ya majukumu yetu sisi ni haya ya kusema tuchangie ili mambo yaende vizuri.

Lakini pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hii. Hii Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii imefanya kazi kubwa na imetuwezesha kutupa

muelekeo wa mambo mazuri ya kuchangia. Kwa hiyo, hatuna haja ya kuzungumza sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze katika ukurasa wa 5 nitakwenda hivyo hivyo kidogo kidogo. Tunazungumzia suala la Sekta ya Habari. Sekta ya Habari Mheshimiwa kamati imeiona kwamba katika kifungu hicho wanasema sekta hii kwa ujumla wake bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili halitaki tochi ni jambo ambalo lipo wazi, ni jambo ambalo kila mmoja wetu analiona na nachukua fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa hili. Wamefanya kazi nzuri Mhe. Waziri na timu yake ya kulibadilisha Shirika la Habari na Utangazaji kwa kutumia sheria waliyonayo.

Lakini pamoja na haya wenzangu wamezungumza mengi na mengi yamezungumzwa ambayo ni changamoto ambazo zinaikabili taasisi hii. Moja ya changamoto aliyoizungumza Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na mimi narudia kuizungumza na naitolea rai na naishauri. Nashauri kwamba ili twende vizuri ni lazima tuweze kuwawezesha vijana wetu ambao muda wote wanakaa hapa kukutumia wanarusha matangazo haya, wanapigwa na baridi, wanavaa makoti, wanafanya nini baadae wanarudi.

Ni wajibu na sisi kurudisha ile hisani waliyokuwa wanafanya, pamoja na kusema kwamba ni wajibu wao lakini sote ni wajibu wetu na sisi wawakilishi tunalipwa nyingi zaidi na siamini kama yupo miongoni mwetu anayeweza kupunguziwa posho akaridhika, hakuna si Waziri, si Mwakilishi, si Katibu, wala si yeyote. Kwa hiyo, ni wajibu wetu na sisi kwamba hawa watumishi wetu wafanyakazi wanaofanyakazi ya kurusha matangazo yetu ya *ZBC* wakapewa.

Ushauri wangu kwa Baraza kwamba ni vyema pesa za hawa zikakatwa akandikiwa waziri *cheque* wakalipwa moja kwa moja isiwe kuna njia ya kuzunguka. Wapewe haki yao na wao wahesabiwe, ikiwa wameamuliwa kupewa shilingi kumi wapewe, thalathini imetajwa wapewe, arubaini wapewe. Kitakachobakia kiende kwenye taasisi husika kuondoa manung'uniko.

Mhe. Mwenyekiti, nimeamua kulisema hili la kwanza kabla ya kuendelea kwa sababu mimi naamini bila ya wao hakuna kitu kitakachoweza kukiona vizuri mpaka wananchi wetu wakapata habari. Leo akisema fundi mitambo huko mambo yameharibika hakuna kitu.

Lakini pia tukija ukurasa wa 6 Majukumu Makuu ya Shirika hili ni kutoa habari na kuielimisha jamii. Leo mimi nilikuwa na kitu kimoja nataka nikizungumze ambacho nakiona watu hawa wana wajibu mkubwa, lakini na moja ambalo kwa sasa linakosekana na nataka kwenye mwezi wa 9 niulize kwenye *library* zetu zile nyimbo za zamani ambazo zilikuwa za asili leo tunaziona zinapigwa kwa mambo mengi mapya mapya. Je, ile *library* ipo? Kama ipo kwa nini haionekani umuhimu wa kuzirejesha zile zikaweza kutunza ile silka yetu ikaweza kutoa taswira nzuri kwa vijana wetu ambao wengi wao leo mambo yale hawayajui, sambamba na kukitangaza Kiswahili cha asili. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, maneno yetu ya Kiswahili ya asili kwa asilimia kubwa sasa yamepotea. Nashauri *ZBC Radio* na *ZBC TV* muandae utaratibu mzuri utakaowezesha maneno yale ya Kiswahili yakaweza kutumika kwa kupata maoni ya wadau wa Kiswahili moja kwa moja kwa kuweka kipindi ambacho mtu ataweza kupiga simu na kutoa maoni yake wale watu wa zamani ambapo vijana wetu wataweza kuyafahamu.

Leo maneno mengi ya Kiswahili vijana wetu hawayafahamu tena yanaanza kupotea kwa kiasi kikubwa. Tufanye utaratibu ambao

utaweza kuyarejesha mambo yale sambamba na hotuba za viongozi wetu. Kwa nini tunasikia hotuba nyingi za kiongozi wetu kama Marehemu Mzee Abeid Amani Karume zinajirejea rejea wakati mzee alianza mwaka 1964 mpaka 1972 alipokufa. Kuna hotuba ngapi zilizohifadhiwa za Marehemu Mzee Karume, hotuba zile zinatakiwa zitolewe ili vijana wetu wafahamu maneno ambayo akiyasema Muasisi wa Taifa hili Marehemu Mzee Karume. (*Makofi*)

Leo hata tukisikia hotuba za Mzee Abeid Amani Karume zinajirejea, mimi niwaulize hatuna nyengine angalau ishirini, thalathini, zikawa zinarejea angalau arubaini ikiwa kila siku asubuhi zinaletwa zile nyengine mpya alizofanya mkutano Kisiwandui, Kidongo Chekundu, alizofanya Chake Chake, alizofanya Mtambwe, alizofanya Konde. Lakini leo hotuba zile za Marehemu Mzee Karume zinajirejea rejea. Mimi naomba sana *ZBC* muwe na utaratibu huo wa kuziingiza hotuba za Mzee Karume katika vipindi angalau dakika tatu au nne kila siku asubuhi vijana wetu wakapata kujua. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo limezungumzwa ambalo sikutaka na mimi niliongezee sana. Lakini naishukuru sana kamati imezungumza katika ukurasa wa 7 kutokulipwa deni la malimbikizo la mfanyakazi Khamis Dadi. Jambo la aibu hili wizara naiomba na nakushaurini mambo kama haya yasifikiwe kuandikwa kwenye kamati. Ni vizuri nyinyi wenyewe mkakaa chini mkazungumza mkamalizia madeni, si vizuri hata kidogo kwa serikali au chombo kikubwa kama hichi kuja kuzungumza deni la mfanyakazi binafsi haipendezi. (*Makofi*)

Ushauri wangu mambo kama haya yasifanywe Mhe. Waziri nakuomba na nakuamini sana kwa utendaji wako kazi ulisimamie na uhakikishe kwamba huyu kama ipo haki yake apewe tena kwa wakati. Tunabeba majukumu hapa lakini mpaka kwa Mwenyezi Mungu kama hatukuweza kulitekeleza hii ni haki yake kwa nini

asilipwe na serikali inatoa pesa kaitumikia serikali kwa nini asipewe haki yake.

Tukienda kwenye ukurasa wa 10 nimeona kuna tatizo la gazeti, mwenzangu Mhe. Simai Mohammed Said kalizungumza sana. Mhe. Mwenyekiti, ipo haja ya kuliona jambo hili na kulifanyia mabadiliko ya haraka kuhakikisha kwamba gazeti letu linapata soko kule Tanzania Bara. Kwa sababu uzalishaji wa nakala mia tano kwa hapa inawezekana ikatosheleza, lakini mia tano kwa Bara au elfu mbili zikawa ni kidogo pindipo tutakapoweza kulitangaza vizuri watu wakalifahamu. Naomba sana na nashauri kwamba kwa hapa suala hili la magazeti lishughulikiwe na liangaliwe kwa upana wake.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nataka niende kwenye ukurasa wa 15 kuhusiana na suala la utalii. Mimi nafurahi na nampongeza sana Mhe. Waziri na timu yake kwa sababu nikikupongeza wewe peke yako bila ya watendaji tutakuwa hatujawafanyia haki, bila ya wao ndio waliokuwezesha wewe na hii wizara ikaweza kufanya kazi vizuri. Lakini tukumbuke kwamba Sekta ya Utalii kwa sasa ni tegemeo namba mbili kwa ajili ya kuingizia serikali mapato ya fedha za kigeni, tunapofika pahala ikawa watu tunaowategemea kuingia ili sisi tukapata fedha za kigeni wanakutana na changamoto jambo hili halipendezi. Mhe. Simai Mohammed Said kalizungumza kwa upana mimi naongezea tu natilia nguvu pale alipomalizia yeye.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema sasa tubadilike tusifanye kazi kwa mazowea, tubadilike tufanye kazi kisasa. Leo tumetoka watalii laki tatu, tulikuwa tunazungumzia laki tatu, mwaka huu tunazungumzia laki nne msimu haujaisha ni matumaini yetu tunaweza kuzidi hapo. Lakini hata wewe Mheshimiwa unapokwenda pahala ukakosa makaribisho mazuri huwezi kwenda tena. Niwaombe sana watendaji wa Kamisheni ya Utalii wasimamie vizuri na wahakikishe kwamba watalii wanapata

huduma sahihi za makaribisho na kila kitu ili na wao wajisikiie wapo nyumbani na wafarijike kwa mara ya pili kuja kutembea. Haipendezi kwa mtu kumwambia kwamba mara ijayo usije tena kufanya *holiday* yako Zanzibar, haipendezi wala si lugha ya kizanzibari, si lugha ya kiungwana, waungwana hawajibizani hivyo. Sisi Wazanzibari ni waungwana na lugha zetu tunazozitumia zote ni za kiungwana. Kwa hiyo, ni wajibu wetu tutumie maneno mazuri ili tuwakaribishe vyema wageni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna changamoto. Mhe. Mwenyekiti, usinitizame kidogo nakuomba juzi sikupata. Sambamba na hayo, kuna tatizo ambalo linatakiwa mliangalie leo wawekezaji wale wamejenga mahoteli lakini kuyafikia mahoteli ni shida, serikali kwa upande wetu tujitahidi kuhakikisha kwamba yale mahoteli tunayafikia kwa kuyatengenezea miundo mbinu ya barabara. Wizara yako na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali na Mitaa na Idara Maalum za SMZ na nyote mnaohusika na mambo haya nawaombeni mtoe kipaumbele cha ujenzi wa zile barabara za ndani zinazofikia yale mahoteli.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf yeye alizungumzia Kamati Teule, mimi sitaki kuzungumzia Kamati Teule lakini naunga mkono suala la Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kufanya utafiti kwamba ni Wazanzibari wangapi ambao wameajiriwa hivi sasa. Nimeshauliza masuala haya sana, ni ukweli usiofichika kwamba nafasi nyingi za ajira hawapewi vijana wetu kwa visingizio tofauti haipendezi, si jambo la busara. Naiomba Wizara ya Kazi kulichukulia suala hili kupitia Idara ya Utumishi ya Kazi kupita hoteli moja moja na makampuni yote kuhakikisha wafanyakazi wazalendo zile nafasi ambazo wanazimudu wanapewa wenyewe. Kwa sababu moja katika sheria yetu ya kuingiza uwekezaji ilikuwa asilimia moja ya mapato ya hoteli yabakie vijijini isaidie vile vijiji vyenye yale mahoteli, leo tujiulize ziko ngapi zinazofanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seid Abeid: Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya najua nimeshawashiwa taa nakuomba kwa heshima kubwa kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia na nawapongeza Wizara kwa kazi zao nzuri. Lakini naomba yale yangu ambayo nimeyatoa myachukue na myafanyie kazi ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said atafuatiwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo na Mhe. Asha Abdalla Mussa ajiandae.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na afya, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya Wanawake, Habari na Utalii, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) na timu yake yote au Wajumbe wake wote kwa uandishi wa kitabu hiki na maelezo ambayo ametoa katika kitabu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nichukue nafasi hii kuwapongeza Mhe. Waziri wa Habari, Utalii Utamaduni na Michezo na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na Manaibu wao, Makatibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Makamishna mbali mbali wa Wizara hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuzungumzia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na sekta zake na nianze na Sekta ya Habari. Sekta hii ni muhimu sana katika kuitangaza nchi yetu kwa mema, mazuri na hali ya uchumi ilivyo. Kwa ujumla watu wa habari wanafanya kazi hiyo kwa uadilifu na umakini lakini bado

zipo kasoro ambazo zinaonekana. Ni matarajio yangu kwamba kamati yetu hii inayoongozwa na Mhe. Ali Suleiman Ali wamefanya kazi nzuri lakini bado katika kipindi kijacho kuna maeneo tutawashauri pia wayaangalie ili wafanye kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Habari hapa Zanzibar imegawika katika sehemu mbili, kuna sekta ya serikali na sekta binafsi. Katika miaka ya nyuma kabla ya miaka ya tisini sekta ya habari ilikuwa ya serikali, lakini sasa imekua na kuwa sekta ya binafsi na serikali. Nianzie na sekta ya serikali hasa kwa *ZBC*. Mhe. Mwenyekiti, kama wenyewe wanavyojiita kwamba wapo katika mabadiliko, mabadiko kwenye televisheni na mabadiliko kwenye redio na tunayaona mabadiliko, ndugu yetu Mkurugenzi Mkuu anajitahidi kuleta vionjo vipya katika kuimarisha utendaji wa shirika hili ambalo la kibiashara, lakini ukiliangalia sana si la biashara ya faida, ni biashara lakini kwa kutoa huduma kwa nchi. Kwa hivyo, ni matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri na timu yake watawaunga mkono ili waweze kufanya kazi kwa uadilifu na kutokumvunja moyo mkurugenzi ili aweze kufanya kazi kwa uhakika.

Ninalotaka kuzungumzia katika *ZBC* Redio na TV bahati nzuri Mhe. Simai Mohammed Said alizungumza kidogo, habari yoyote inataka *balance* kwamba ukifanya tukio likizungumzwa basi na yule mwengine nae atafutwe athibitishe ukweli wa habari. Wakati mwengine tunapitikiwa hatufanyi hivyo tunatoa habari za upande mmoja. Kwa bahati mbaya sana kama alivyosema Mawio kipindi ambacho wananchi wanakisikiliza na wananchi wengi wanasema shida zao. Sasa kama wananchi wamesema halafu Mheshimiwa asijibu asiseme maana yake nilivyomwambia kwamba unamfunga mdomo zisemwe habari za upande mmoja. Kwa hivyo, hili nafikiri Mhe. Waziri na yeye ni Mheshimiwa anajua wataliangalia

njia bora ya kufanya ili kuweka usawa katika utoaji wa habari. Wakati mwengine tunaona kwamba ni taasisi ya serikali hasa ukipigwa unavumilia tu lakini kuna mambo mengine wazi wazi unaona kwamba haya hukutendewa haki.

Lakini pia kuna baadhi ya waandishi na watangazaji kwa ubinaadam wanakosea wanaposoma habari au uandikaji wa habari. Tunamuomba basi Mhe. Waziri kupitia kwake hao waandishi wawe na utamaduni wa kuomba radhi sio umekosea halafu unafanya kama hukukosea unakwenda tu husemi suala la kuomba radhi ama vipi. Kwa hivyo, hili nalo lionekane kwamba ni changamoto ambayo imeikabili sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa bahati nzuri sana Mhe. Rais wetu amejitahidi sana taasisi hii iwe na studio bora na za kisasa, lakini matumizi ya studio hizi bado ni mjadala hata wasanii wetu bado hawapati fursa ya kufanya kazi zao katika studio hizi kwa kiwango kizuri. Sijui studio zetu ni za kufanyia hafla tu katika maeneo ya Wizara ya Habari au alikusudia jengo maana yake nini, ili wananchi wajue ili na wasanii wetu waweze kunufaika. Kwa hivyo, mimi nafikiri hilo nalo wapunguze masharti kwenye studio ili wasanii na watu wengine waweze kutumia studio zile kama zilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine na hili naiomba kamati chini ya Mhe. Ali Suleima Ali (Shihata) Mwenyezi Mungu akipenda tunatarajia awe tena Mwenyekiti wa Kamati hii ya Wanawake kipindi kijacho, basi namuomba sana Mheshimiwa waende wakatembelee minara ya studio Masingini waangalie hali ilivyo. Hali ya Masingini hairidhishi sana kwa hivyo namuomba Mhe. Shihata na timu yake waende kule waseme wao tunataka kwenda sehemu fulani sio wapangiwe waende wakaangalie eneo hili ili liweze

kuimarishwa. Pale kuna kikosi cha KMKM wanalinda kibanda kibovu Wizara hawajakitengeneza, kuna minara inataka kuangaliwa vizuri kwa hivyo lazima waende kule. Ukisoma humu katika ripoti yao wamezungumzia kwamba zipo taasisi binafsi zinalalamika zinakodishwa minara kwa bei kubwa, sasa lazima hili Mheshimiwa uende ukaliangalie kwa uhalisia ili tuweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka kuzungumzia vyombo binafsi vya habari, hivi vyombo navyo ni muhimu na wenzangu wamesema kwamba vyombo ya habari binafsi vimefanya kazi nzuri, mimi nakiri kweli wamefanya kazi nzuri na wanaendelea kufanya kazi nzuri. Lakini lipo tatizo wao wanaikosoa jamii wanaisaidia serikali, lakini watumishi wa sekta binafsi ya habari wanalipwa mshahara mdogo sana usiozidi hata laki mbili ya kiwango cha serikali kima cha chini haifiki. Tunaomba kamati nalo hili walione. Tumezungumza na wakuu wa vyombo vya habari binafsi hebu zungumzeni na wafanyakazi wa vyombo binafsi vya habari muone maslahi wanayolipwa, wanalipwa maslahi madogo sana. Mhe. Mwemyekiti, sisi tunataka sekta binafsi iweze kwenda mbele kwa hivyo na hawa wawezeshwe, wengine nasikia pale hawalipwi chochote wanakwenda wanafanyakazi lakini hulipwi ili ukipata kazi ndio ujilipe huko huko, hiyo haiwezekani lazima kuwe na utaratibu mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nizungumzie Shirika la Magazeti ya Serikali, limezungumzwa humu ndani kwamba sasa hakuna gazeti Bara la Zanzibar Leo na hili ni tatizo. Kwa sababu kama walivyosema wengine kwanza wenye makampuni ya matangazo mengi ni Bara, lakini na sisi tunapokwenda na wenzetu waliopo Bara wanataka kupata habari za Zanzibar. Mimi juzi siku ya Ijumaa nilitaka kuliangalia gazeti la Zanzibar Leo Dar es

Salaam nimeshindwa, Dodoma hakuna. Sasa hili kwa nini naomba tusaidiane hili gazeti liweze kuwini.

Lakini hapa utaona kwamba shirika hili linadai pesa nyingi, mimi nataka kujua hizi milioni 138.7 ambazo wanazidai watu binafsi uliwapa nini au huduma gani. Shirika lilitoa kwa taasisi binafsi mpaka likafikia deni la milioni 138 bila ya kulipwa. Tuseme serikali mlikuwa mkipeleka magazeti na huduma nyengine za matangazo. Hivi na huku pia kwenye matangazo watu binafsi walitoa milioni moja na bila ya kulipwa na kuendelea na kutoa huduma hii.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya utalii niwapongeze wamefanya kazi nzuri sasa hivi tuna watalii 4,034,000 karibu, lakini niombe tusibweteke kwa kiwango hiki cha watalii zipo nchi kama sisi za visiwa tena vidogo zaidi yetu sisi, kama Maldives na nyenginezo, Cuba huko wana watalii karibu milioni tatu kwa mwaka, hawa wenzetu wana laki saba kwa mwaka na kuelekea milioni moja. Sisi kama dhamira ya serikali ilikuwa laki tano 2020. Lakini kutokana na mfumko na fursa tulizozipata kutokana na majirani zetu wengine kuharibikiwa na utalii mimi nafikiri tungelijipangia tuwe na laki saba mpaka 2020 na tunaweza tukijitahidi kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Makumbusho itakuwa sehemu yangu ya mwisho pamoja na Idara ya Michezo. Idara ya Makumbusho kwa hakika imevurugika naweza kusema kama yamekufa na kwa sababu sijui ndio makumbusho au vipi, lakini karibu makumbusho yote yamekuwa magofu tu sasa mpaka lile jengo kuu la Beit el Ajaib nalo pia limekuwa hamna kitu. Sasa kama pale pameharibika je, huko Maruhubi, Kijichi na kule kwa Bikhole hamna kitu. Mimi nafikiri tatizo la idara hii labda serikali Mhe.

Waziri hamjaitilia maanani na ndio maana kwa miaka miwili na nusu haina Mkurugenzi. Sasa kama idara haina Mkurugenzi kuna Kaimu Mkurugenzi tu haya makumbusho yataishi kweli. Kwa muda wa miaka miwili hakuna mtu ambaye anaweza kufanya kazi hiyo ya makumbusho. Kwa hivyo naomba tu na hili kamati utatusaidia ili zipatiwe tija.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu michezo niwapongeze tumepata mafanikio ya *Zanzibar Heroes* wamefanya vizuri, lakini mimi namuomba Mhe. Waziri kwanza mafanikio ya timu ya taifa yanatokana na ligi nzuri ya ndani, kama huna ligi nzuri huwezi kuwa na timu ya taifa nzuri. Mimi naweza kusema tumepata timu ya taifa nzuri kwa sabbu wachezaji wetu pia wanacheza ligi kuu ya Bara kuwa wengi katika wale waliokwenda Kenya. Sasa tuwe na mambo mawili, kwanza tujitahidi tuwe na ligi bora ili wachezaji wetu tuwauze hata hapa hapa Tanzania, lakini la pili uondoe kidogo ubaguzi hatupendi sisi washabiki wa mpira kusikia *ZFA* Pemba na *ZFA* Unguja, Kamati Tendaji ya *ZFA* iwe moja tu na ligi iwe moja, isiwe na ligi Pemba na ligi Unguja, kuwe na Ligi Kuu moja ya Zanzibar. Lakini serikali tunao wajibu wa kusaidiana na *ZFA* kutafuta wafadhili na walimu, tufanye juu chini ligi yetu iwe na mdhamini, wenzetu huko Bara wanafanya hivyo na tunaona mpaka wafanyabiashara wenye asili ya Zanzibar kina Bakhresa wanadhamini wao ile Ligi Kuu inayoitwa *Azam Cup*.

Kwani tukimuomba na sisi hawezi kuja kufadhili Ligi Kuu ya Zanzibar ambayo hakuna masafa marefu ya usafiri wa timu, timu hazina gharama kubwa kama Bara, nafikiri tukifanya kazi vizuri tukiweka maslahi ya nchi mbele tunaweza kupata mfadhili na tukasaidiwa katika mambo haya. Lakini ombi jengine katika michezo kwamba Mwenyezi Mungu akipenda naiomba wizara yako Mhe. Waziri mwaka 2019 katika kuenzi mafanikio ya Timu

ya Taifa ya Zanzibar basi tuombe tuandae timu ya *Challenge Cup*, ili iwe kuelekea katika sherehe zetu za Mapinduzi au vipi lakini tuwe na *Senior Challenge Cup* kwa mwaka 2019. Nafikiri tukiwahi mapema tunaweza kupewa fursa hii, muda mwingi sana zaidi ya miaka kumi Zanzibar haijaandaa mashindano ya *challenge*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niingie katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na hapa nitazungumza kidogo tu. Nampongeza Mhe. Waziri na timu yake wamefanya kazi kwa bidii, wizara ni kubwa hii ina taasisi nyingi. Kwa hivyo, lazima tuwape moyo, mimi naomba tu wazidishe utoaji wa elimu katika uwezeshaji bado wananchi wetu katika majimbo yetu hawajui fursa hizi za uwezeshaji zinapatikana vipi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri awape elimu na ikiwezekana hata Waheshimiwa Wawakilishi mnaweza kuwapa semina ya uwezeshaji ili na wao waweze kwenda kuwasaidia wananchi wao. Kwa sababu kazi za wawakilishi ni za wananchi, kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba sana wakati wa bajeti ijayo fanya juu chini utuletee semina ya uwezeshaji mafanikio na changamoto zake zinazoikabili katika taasisi yake.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho udhalilishaji wa wanawake na watoto suala hili ni kubwa na janga kwa taifa na sote kwa umoja wetu tunalipinga. Lakini tuwaombe wazee na wananchi pamoja na sisi tuwe tayari kutoa ushirikiano kwa taasisi zetu, Baraza hili limepitisha miswada miwili ambayo itakuwa sheria muhimu sana. Kuna sheria ya adhabu na sheria ya mwenendo wa kesi za jinai. Kama tutatoa elimu na wananchi kuzielewa adhabu zake mle kwa masuala haya ya udhalilishaji wa wanawake na vijana wadogo wa kiume na kike bila ya shaka tutapata mafanikio zaidi katika kupambana nayo. Lakini adhabu kali peke yake haisaidii

isipokuwa na elimu yenyewe na utayari wa watu kuanzia wazazi, taasisi ya serikali kama mahkama, waendesha mashtaka, polisi, wizara na hospitali zetu, pamoja sisi wenyewe ambao tutakuwa tuna familia nazo ni msingi katika kupambana na maovu haya.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi maoni yangu yalikuwa hayo na naomba nipongeze kamati niwatakie mafanikio mema. Lakini kuna yale maeneo mengine nayo wajizamishe zaidi kupata uhalisia wa mambo, nafikiri tumefanya kazi nzuri. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono ripoti hii ya kamati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Machano Othman Said, sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Ali Kombo na atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwanza naikubali ripoti hii mia kwa mia sina mashaka nayo ukiacha kasoro ndogo ndogo tu ambazo nitazungumza. mimi ningeomba tu baadae Mhe. Waziri wakati ukifika akija zimetajwa takimu za ongezeko la wageni 3,076,342 hadi 4,033,126. Mimi ningeomba tu wakati ukifika na pesa pia atutajie ambazo zimeingia ikiwa ni dola, ikiwa ni pesa zetu, tusiwe tunapokea watu tu kubwa zaidi hapa tunataka pesa. Kwa hivyo, akija Mhe. Waziri hili naomba atwambie ni pesa ngapi hadi ngapi, au ngapi kutoa ngapi, la kwanza.

La pili Mhe. Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni, Utalii na Michezo, waandishi wake wa habari ningeomba sasa hivi iwawezeshe angalau zile habari zao zigeuke *tone*. Sasa hivi ukifungua redio tu kwenye Mawio ni udhalilishaji, nani kabaka, nani kafanya nini, si vibaya lakini sasa wapewe

uwezo angalau waende vijijini kuna kazi nyingi sana ambazo wananchi wanazifanya, kuna mifugo, kuna kilimo, kuna matatizo chungu nzima. Sisemi kwamba ubakaji si matatizo, lakini tena sasa angalau ripoti kidogo iwe inageuka geuka. Naomba kwa njia zenu ambazo mnaweza ukawawezesha basi Wizara tujitahidi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, namkumbusha tu Mhe. Waziri kuna fidia ya watu wa Bungi ambapo tumejenga minara ya redio, hii nakumbusha tufahamu kwamba tuna deni. Kuna jengine nadhani Mhe. Simai Mohammed Said alikumbusha lakini muhimu kwa wakala wetu wa watalii, muda ukifika si vibaya kwa mawakala kupewa vikaratasi kwa njia yoyote wakajua kwamba mwezi huu *culture* ya hapa ipo kadhaa, kwa hivyo kuna maeneo fulani yanafaa kufanya hivi. Namuomba Mhe. Waziri na hili dogo lakini tujitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Mhe. Waziri akija sasa hivi ni mwezi wa pili bajeti nyengine inaingia, viwanja vya michezo. Tumezungumzia sana, Mhe. Machano Othman Said kazungumzia sana mipira, tukenda mpaka *Zanzibar Heroes*, tukasema tutajenga viwanja, leo kwa kwetu Kusini au Kati tumebakia na Bungi tu, sasa viwanja navyo angalau viwepo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imejitahidi lakini imesahau baadhi ya mambo na bahati mbaya yalitangazwa kwenye vyombo vya habari na mimi sikutaka mambo haya tena niyazungumze, kichwa kinazidi kunizunguka Waheshimiwa Wawakilishi. Hapa kuna *document* hii Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alisahau kuweka kwenye *document* zake. Hii *document* inasema: “Taarifa ya mradi wa ujenzi wa dakhalia na skuli ya kusomesha mambo ya utalii katika nyumba ya serikali iliyopo Kigaeni na kiwanja Nam. 922 kilichopo Nganani Makunduchi Zanzibar. Imetayarishwa na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora”.

Hii Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri amesahau, lakini alipewa juzi katika safari zake. Hapa nasikitika kidogo, si vizuri serikali siku zote ukawa unauliza mambo haya haya au wananchi unawagonga gonga kwa kuwatenganisha. Mimi nimeuliza mara ya mwisho Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira (Salama bint Aboud) alinambia nyumba hii ni ya serikali, kauli ya serikali kwa sababu yupo hapa kwa niaba ya serikali. Lakini nyumba hii ndugu zangu Wawakilishi mpaka hivi karibuni inalala wageni na wanalipa dola sio za Zimbabwe ni dola za Kimarekani. Pesa hizi zinakokwenda hazijulikani, hii ni nyumba ya serikali.

Katika maswali yangu na *hansard* zipo, nyumba ile niliambiwa ni Chuo cha Kilimo na cha Utalii na wamesha-*graduate* na wameshaajiriwa. Nyumba hii pia kuna baadhi ya Mawaziri niliwauliza wakanambia wao hawajui chochote. Hii karatasi Mhe. Mwenyekiti, nitakupa humu kuna wizara kama nne zimeshirikishwa ni kwamba zinajua kila kitu juu ya ile nyumba. Sasa tufikeni pahala mimi naipenda sana serikali yangu hii tai hapa nimeiweka kwa sababu ya serikali na nimepata kwa sababu ya Chama cha Mapinduzi, lazima niiheshimu serikali hii na naipenda tena sio kwa mdomo wala kwa kubabaisha. Sasa hapa nachanganyikiwa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imehusikaje na nyumba hii na ripoti hii Mwenyekiti nadhani na wewe na Mhe. Waziri mje mtujibu. Ile nyumba inalala wageni, jamani hapa tunazungumzia pesa, kila wakati pesa, nchi inapotea, pesa zinakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, samahani nina-*declare* kwamba ni Mmakunduchi, ile Kamati iliyoambiwa ni ya Makunduchi inapata pesa ngapi katika pesa hizi. Je, hii ni halali. Tupo watu wazima ndugu zangu ifike pahala tujitambue kwamba sisi ni viongozi na jamii inatutizama. Maana hapa kinachoshangaza ni kwamba labda kila waziri anatumia *influence* yake kwa pale alipopewa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuna Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, zote zipo hapa, sasa kama kila waziri atakapokaa, Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo achukue TV, achukue mipira, Tawala za Mikoa achukue bunduki. Ah! Sasa hapa hapatakuwa na nchi tena. Naomba Mhe. Waziri na Mwenyekiti mkija mtupe jibu, hii nyumba mlitwambia dakhalia na hapa imeandikwa dakhalia, lakini inalala wageni na hailipwi, hii ni halali.

Tukumbuke kile kitabu cha kusadikika kinachosema kuna kiongozi mmoja anakunywa maji ya bahari tani tano na madau yake, lakini kila baada ya muda mfupi anasema ana njaa na kiu, hii ni hatari. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nakumbusha tu, tufike pahala serikali isiwe na matamshi ya *zigzag, hansard* zipo kule. Serikali ilitangaza hapa kunambia mimi na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania nyumba ile ni ya serikali. Lakini ukisoma hii ya Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na huku kuna michanganyiko mengine tunawa-*confuse* wananchi, tunaji-*confuse* na sisi wenyewe. Naomba tutulie katika *information* zetu na katika maamuzi yetu. Ahsante sana Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Abdalla Ali Kombo, sasa naomba nimwite Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na kama muda utaturuhusu basi Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi ili kuchangia Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ambayo inaongoza Wizara mbili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi ila nitachangia mambo machache katika ripoti hii. Niendelee kuwapongeza

wajumbe wenzangu ambao wametangulia kuchangia ripoti hii. Pia niwapongeze Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuanzia Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi ambazo wanazifanya za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wizara hizi zinafanya kazi kama wenzangu walivyotangulia kusema. Pia napenda sana niwapongeze Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kazi wanazozifanya kuanzia mwenyewe Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na viongozi wake wote wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Sekta ya Utalii niwapongeze kamati hii kwa kazi ambayo wameifanya katika kipindi chote hiki na hii leo kutuwasilishia Barazani na sisi kuweza kutoa maoni yetu. Katika Sekta ya Utalii nimeona mafanikio ambayo yamepatikana katika sekta hii, tumeona kuongezeka kwa wageni ambao wanaingia nchini kwetu na pia ujio wa ndege mpya na meli za kitalii. Sote ni mashahidi kwamba tunaona kila kukicha tukizunguka Zanzibar nzima Unguja na Pemba unawakuta wageni wa kitalii wameingia hapa kwetu Zanzibar. Hii inaonesha kwamba nchi yetu ni ya utulivu na yenye historia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba kamati imetembelea baadhi ya maeneo ya utalii na ikagundua changamoto ambazo wamezikuta. Katika changamoto hizo zikiwemo miundo mbinu. Wanasema kwamba kamati imegundua takriban mahoteli mengi ambayo yapo hapa Zanzibar kuna tatizo kubwa la miundo mbinu ikiwemo tatizo kubwa la barabara na maji safi pamoja na umeme ambao usio wa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba miundo mbinu hii kama haijatengenezwa au haijaondoka changamoto hizi kwa kweli wageni wetu wakati mwengine wanaweza wakatukimbia. Tukitengeneza miundo mbinu ambayo ipo, basi wageni wataweza

kuvutika kwa miundo mbinu ambayo ipo. Niungane na Wajumbe wa Kamati kwa mapendekezo au maagizo ambayo wameyatoa.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna kucheleweshwa kwa kupatiwa vitambulisho vya waongozaji na watembezaji watalii ambao changamoto hii wenzetu hawa wanapeleka fedha zao mapema idara husika, lakini wanacheleweshewa kupewa vitambulisho hivi. Naomba sana Kamisheni ya Utalii iwaharakishie watu hawa ili waweze kufanya kazi zao kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo ambalo kila mwaka linajitokeza kuhusiana na suala zima la takwimu. Kamati pia wamesema kwamba kuna kukosekana kwa takwimu sahihi za wageni wanaoingia nchi kwa shughuli za kitalii suala ambalo linachangia upotevu wa mapato. Suala hili kwa kweli kwa kuwa tumeona mafanikio ya Sekta ya Utalii yanakuwa siku hadi siku lakini pia tumeweza kugundua kwamba wageni wameongezeka. Naomba sana wizara husika ikishirikiana na Kamisheni ya Utalii basi iandae mfumo maalum ambao unaweza kufanikisha na kutambua takwimu halisi ya wageni wanaoingia na kutoka hapa nchini kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika maagizo ya kamati niungane na agizo hili kwamba kamisheni ihakikishe Sheria ya Utalii Nam. 7 ya mwaka 2012 inayoweka masharti ya kuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo wa Vijijini ambapo kila mwekezaji anapaswa kuchangia asilimia moja ya mapato yake inatekelezwa. Mimi kwa kweli naunga mkono kamati kwa kuliona suala hili kwamba ni tatizo na tuone mahoteli mengi au wawekezaji wengi wapo katika maeneo ya jamii na jamii nayo ifaidike na wawekezaji hawa ikiwemo masuala mazima ya barabara, maji safi na mambo mengine ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Nikija ukurasa wa 29 kuna mambo

ambayo kamati haikuridhika nayo kwani kuna changamoto katika Sekta ya Kazi. Niipongeze sana sekta hii kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaifanya katika maeneo yao ya kazi. Kwa kweli ndani ya kamati wameona kwamba kuna Maafisa wa Ukaguzi wa Kazi na Usalama wa Afya Kazini hawafuatilii majukumu yao hasa katika sekta binafsi ambayo hatua wameifanya kamati ya kufikia katika Kampuni ya Ujenzi, Kiponda mara mbili na kutoa maagizo kadhaa ambayo mpaka sasa hayajafuatiliwa. Tatizo hasa katika sekta hizi za binafsi kuna tatizo kubwa la mambo ya mikataba ya kazi. Suala hili ni sugu katika baadhi ya maeneo, mahoteli mengi na makampuni mengi inafika pahala inawaajiri watu na kuwatumia kwa muda mrefu lakini wanashindwa kupewa mikataba.

Masuala haya ukifuatilia zaidi kwa kweli wakaguzi hawa wanakwenda wanapofika pale wanazungumza na wenyewe waajiri lakini hatimaye yale mambo yanapotea kabisa na inafika pahala changamoto kubwa muajiri anawafukuza kiholela wafanyakazi na wafanyakazi wale wanashindwa kwenda kufuata sheria kwa sababu mikataba hawana. Naomba sana wizara husika kwa kushirikiana na Kitengo cha Sekta ya Kazi basi ishirikiane na ifuatilie yale makampuni yote ambayo wafanyakazi wake hawajapewa mikataba basi wapewe ili wafanye kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la wazalendo kukosa ajira, wenzangu wametangulia kusema Mhe. Nadir Abul-latif Yussuf pamoja na Mhe. Omar Seif Abeid suala zima la ajira binafsi kuwa na wageni wengi kuliko wazalendo wenyewe. Suala hili kila tunapoingia Barazani hapa inafika kipindi hata kipindi cha Bajeti tatizo hili tunalizungumzia sana. Inasikitisha hususan sisi Wawakilishi ambao tupo katika ukanda wa pwani ambao tuna wawekezaji wengi. Vijana wetu wanatulalamikia kwamba ajira hakuna basi hata katika Sekta ya Utalii. Ukitizama kwamba mahoteli yapo na kuna kazi ambazo sio lazima wawepo wasomi.

Kuna sekta ambazo hata mtu wa kawaida anaweza kufanya kazi katika sekta hizo za utalii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kupitia wizara husika basi iunde kamati ya kufuatilia wafanyakazi ambao wapo katika mahoteli au makampuni hayo na kuona wazalendo wangapi na wageni wangapi, ili tuone na tujue kwamba tatizo hili lipo kweli na kama lipo tutafute njia au mikakati ya kufanikisha liondoke.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Mfuko wa Uwezeshaji, niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuamua kwa makusudi kupitia Wizara hii ya Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kuandaa mfuko huu wa JK na AK kwa makusudi kwa ajili ya kuwaweshesha wanawake kiuchumi. Tumeambiwa kwamba mfuko huu tokea kuanzishwa ni miaka minne (4) sasa, lakini mikopo iliyotolewa ni 1,430 jumla ya shilingi bilioni mbili, milioni mia tano sabini na mbili elfu na sabini na tano iliyotolewa Unguja na Pemba ambapo wananchi 21,000 wamefaidika moja kwa moja na mikopo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu sote kuna malalamiko ya wananchi ambayo wanasema wanapofika katika eneo husika kwenda kutaka mikopo hii kwa kweli hawapati fursa ya kupata hii mikopo. Ninachokiomba kwa wizara husika kwamba izidi kutoa elimu kwa jamii hiyo na kuwafahamisha kwa kuwapa maelekezo ili waweze kunufaika na mkopo huo. Pia naomba tupewe mchanganuo huo mwezi wa sita tutakapokuja kupewa majibu, tupewe mchanganuo kwa kila mwaka tokea kuanza kwa mfuko huo mwaka 2013 mpaka 2018 ili tuone kila mwaka mikopo ilitolewa mingapi na imerejeshwa mingapi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati iliweza kuona changamoto ya kwamba hakuna takwimu sahihi ya idadi ya vyama au mtu ambaye amefaidika na fursa hizo. Naomba sana tujue ni sababu gani na tumeona kwamba pesa zimetumika kwa ajili ya

kuwakopesha wananchi lakini na wananchi hao tumetajiwa ni 21,000, basi tuone ile takwimu yenyewe halisi ambayo kwa wale watu waliofaidika. Hii ni changamoto kama walivyosema Wajumbe wa Kamati basi tunaomba siku hiyo ya kuletewa majibu katika Baraza hili tuone ule mchanganuo wenyewe wa takwimu halisi ya watu ambao wamefaidika na mkopo huu.

Lakini pia tumeona kwamba kuna urejeshwaji wa mikopo, kuna baadhi ya wakopaji kutokutaka kulipa mikopo yao bila ya sababu za msingi jambo ambalo hupelekea kuwanyima fursa wananchi ambao wengine wanahitaji kukopa mkopo huu. Naomba sana jamii husika ambao wamekopeshwa fedha hizi basi iundwe mikakati maalum ili kuhakikisha kwamba watu hao waliobakia wanarejesha mikopo hiyo kwa haraka ili na wananchi wengine wapate fursa ya kuweza kukopa.

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja kwenye suala zima la Sekta ya Wanawake na Watoto ambayo iko ndani ya ukurasa 34 na kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna mambo ambayo kamati haikuridhika nayo katika changamoto ya Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala hapa ambayo wameyaona waheshimiwa wajumbe wa kamati hii ukosefu wa usafiri. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunaomba sana Idara hii ya Maendeleo, Wanawake na Watoto wapewe usafiri ili waweze kufanya majukumu yao ya utendaji yakiwemo ufuatiliaji wa masuala ya kesi za udhalilishaji. Sote tunafahamu kama kutokuwa na usafiri watendaji wetu hawa hawatoweza kufuatilia kesi hizo za udhalilishaji maeneo yote.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine kukosekana kwa mfumo bora wa ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, endapo idara hii watapewa vitendea kazi wataweka

sawa hata huu mfumo wenyewe wa ufuatiliaji wa kesi hizi za udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna suala la waratibu wa shehia kukosa vitambulisho. Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba katika shehia zetu kuna Waratibu wa Wanawake na Watoto ambao wanajitolea kwa kufanya kazi zao kila siku asubuhi, mchana na usiku. Lakini waratibu hawa wanafanya kazi kubwa kweli kwasababu kabla ya kesi zote kwenda polisi basi mratibu lazima kwanza aitwe yeye na azifuatilie. Lakini inasikitisha kwamba waratibu hawa wanafanyakazi bila vitambulisho. Kwa sababu na mimi nilitokea huko kwenye Uratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia, basi naomba sana sana waratibu hawa wapatiwe vitambulisho, lakini pia wapewe posho angalau wapate japo nauli ya kwenda hata wakiitwa wilayani ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana kamati hii kwa mpango waliojipangia wamesema kwamba watashirikiana pamoja na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika maendeleo ya wanawake pamoja na mizunguko yote kwa mwaka huu. Ni jambo zuri kamati hii ikishirikiana pamoja na Afisi hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka basi itaweza kufahamu kwamba kesi ngapi ambazo zipo na ni kesi ngapi zinaweza kuchukuliwa hatua kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu sote kwa jumla changamoto za kesi za udhalilishaji ambazo zipo hapa Zanzibar na wenzetu hapa wameona kwamba kuna uwepo wa maombi mengi ya ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji kutoka kwa wana jamii. Hii inatokana na baadhi ya wahanga kuona kuwa hawana washtakiwa au uhusiano wa karibu na familia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli haya masuala yanasikitisha sana lakini utakuta pia kuna baadhi ya watendewa wa makosa ya udhalilishaji umri wao ni mdogo sana na wanashindwa kujieleza

polisi au kutoa ushahidi wa mahkamani. Suala hili kwa kweli ni sawa lakini wenzetu hawa wanaokwenda kuwafanyia watoto wadogo vile vitendo wanafanya kwa makusudi ili washindwe watoto wale kutoa ushahidi wa uhakika. Kwa kweli utakuta mtu anakwenda kumfanyia kitendo mtoto wa miezi miwili au mitatu ataweza kutoa ushahidi, au mtoto wa miaka minne anaweza kutoa ushahidi, mtoto anashindwa akimuona polisi anakimbia kweli leo anaweza kutoa ushahidi. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tumepitisha Sheria ya Adhabu pamoja na Sheria ya Makosa ya Jinai, basi naomba sana Mhe. Rais aweze kutia saini haraka ili ziweze kutekelezwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Asha Abdalla Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nikachangia machache kama walivyochangia wenzangu ili kufanikisha Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nianze kwa kamati kuwashukuru sana katika kufanya kazi yao na kuweza kuona changamoto nyingi zinazowakabili wizara hizi mbili na pia kuziandika ili kuweza kuzifahamu vilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niungane na wenzangu kutokana na makosa mengi yaliyoandikwa humu ndani ambayo kama wizara yapo mengi. Mimi naungana na wenzangu wale wote waliosema kama paundwe kamati ya kwenda kuchunguza au kuona yale yote

ambayo kamati wameyaona na wale kamati nyengine na wao waweze kutoa undani zaidi, maana yake watapata fursa zaidi ya kuonana na watendaji. Mimi naunga mkono kutokana na hali halisi ya kitabu walichokiandika, nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) nafikiri kwa hivyo wameandika mambo sana humu si rahisi kuyasoma.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la Pemba ambapo hakuna taarifa za habari zinazopatikana kule zinazokuja Unguja kwa wakati. Pemba bado nasema tena upande wa *ZBC* bado habari zake hazipatikani zilivyo. Mimi nakumbuka Pemba kulikuwa na Mawio Asha Pandu Mwinyi, Kauthar Is-haka, Suleiman Mawio na Masanja Mabula, lakini sasa hivi simsikii hata mmoja labda uone kwenye *clip*, sijui habari hizi wale waandishi wa habari wamekwenda wapi ambazo angalau asubuhi unapata taarifa zozote zilizoanguka kule Pemba. Hivi sasa labda urushiwe *clip* ya mtu ambayo kavuta, lakini waandishi wa habari na ninaamini watakuwa kama wamechoka hivi, maana yake mwandishi wa habari kama hapati habari zake kutolewa anakuwa hana haja ya kufanya kama anafanya *photocopy* ya uongo uongo, maana yake unamuona anakupiga picha anaandika habari halafu hazitoki.

Kwa hivyo ningeomba Mhe. Mwenyekiti, suala la habari Pemba likatizamwa upya, matangazo haya ya redio na TV waipe nafasi Pemba kipindi maalum ambacho na wao wanapata na wakati wa asubuhi Mawio. Simu zinapatikana kwa nini wawe habari zao hawapeani na Pemba ikatoka, wewe utasikia tu sijui wanaita wapi hapa katikati ndio unakuta Mawio yanapotoka. Kwa nini Pemba Mawio hayapatikani. Kwa hivyo, ningeomba sana tukapata zile habari za Mawio si kama habari mbaya tu, ni habari zozote ambazo zinatokea kuhusu kule. Kwa hivyo, hawa watu mimi ningeomba mkarudia nao mkawatafuta tena kama wapo au wapo wengine ili kuweza kuwarudisha katika fomu angalau tukapata habari.

Mhe. Mwenyekiti, habari ni kila kitu, habari ndio inayofanya mambo yote unayoyasikia katika ulimwengu ukayapata, wao ndio wanaoweza kufanya vitu vizuri au wakafanya vitu vibaya, lakini naamini waandishi wanapoandika mambo mengine huwa wanafanya kwa kuwapa habari jamii. Kwa hivyo, ningeomba sana kwa upande wa Kisiwa cha Pemba habari za *ZBC* na redio bado sana.

Mhe. Mwenyekiti, niliwahi kulifuatilia gazeti la Zanzibar Leo huwa naliona kuna sehemu nzuri ya Pemba zinaandikwa habari zake, kwa nini na hii TV na redio habari zake zisiandikwe. Kwa h hivyo, ningeliomba sana wakaangalia wale waandishi wa habari wanaochukua na wao siku ya pili yake au siku ile ile habari zao wakapata fursa zikatoka.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye gazeti tulilipigia kelele sana hapa kwamba lije lifanye kazi Zanzibar. Mheshimiwa gazeti lile la Zanzibar Leo kwa kufanya kazi Zanzibar halipati faida na humu tumeandikiwa mafanikio mengi yaliyoandikwa lakini fedha sijaziona zilizoandikwa kwamba tumepata faida gani toka kuleta kwetu. Sisi Wazanzibari tuliokuwepo hapa sote ni milioni moja laki tano, wanaosoma gazeti ni watu hamsini elfu kama wanafika au ishirini elfu au wangapi na magazeti yakigaiwa yapo kumi, kumi na tano Zanzibar Leo linasomwa na watu hamsini au arubaini litapata faida wapi.

Gazeti linakwenda kwa watu ambao wapo milioni arubaini, huko mikoani lipo kila pahala, gazeti tumelihamisha Bara tumelileta hapa tumeangalia faida na sasa tunaona kwamba halina faida tena. Sasa tunataka turudishe kule kule au linabaki hapa hapa, maana yake kwa hapa kwa kuchapisha habari magari kule yanaondoka alfajiri saa kumi, sita ya kwenda mikoani labda tukodi ndege lakini kwa gazeti hatuwezi kupata faida kwa kulianzisha hapa.

Gazeti lazima likitakiwa kusoma sisi tungepata nakala ndogo tu ya gazeti letu, ni mafanikio makubwa gazeti kulichapisha hapa. Lakini hata huo mtambo utakapokuwa kule Bara wakati ni wetu si tutachapisha vile vile. Mimi naona tu kwamba tuangalie sifikiri kama kwa faida ya Zanzibar kutoa gazeti hapa itapata faida.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Kamisheni ya Utalii, utalii sio kwamba kuna mahoteli tu au kuna kitu gani, utalii unahitaji ufuatiliwe sana, utalii wana uwezo hata kama mtu ana hoteli wa kwenda kumsaidia maarifa ili kupata mapato zaidi na wageni zaidi. Utalii wa kwenda kwenye njia wakakutana na Wizara bwana kuna hoteli kule, kuna mambo ya utalii kule, barabara hii tutaifanyaje tutachangiaje, tunafanya kila kitu. Lakini yeye atakwenda zake kwenye hoteli hata hama haipitiki ataruka juu atakwenda kule, mgeni atakwenda vipi. Kwa hivyo, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo barabara za kwenda kwenye mahoteli na kwenye sehemu za utalii nao zinawahusu, wao walitakiwa kuziangalia na kusaidia michango ili mtu afikie kule kwenye sehemu. Lakini wao wanaruka wanakwenda kule kwenye hoteli wanamalizana nae wanaruka tena atakwenda mgeni gani kule.

Kwa hivyo, nilikuwa nashauri nao wasione kuwa watu wa utalii kwamba kazi yao ni wazungu na dola na kila kitu, wana haki ya kutizama vitu gani ambavyo vinasaidia ili utalii ukue. Mheshimiwa utalii Pemba haujakua kabisa, mahoteli yanalala matupu, yanajengwa na sio faida ya mtu anatakiwa ajenge viwanja vimetolewa na serikali havijengeki hata ukijenga hakuna watalii na sababu mbili kubwa. Mheshimiwa kwanza Pemba usafiri wake haujakuwa *guarantee* na bei ni ghali sana utafikiri unakwenda nchi za nje. Wao watu wa utalii wanapanda ndege hapa laki moja na ishirini, kwa mzungu sijui anapanda dola mia mbili atakwenda kutalii wapi, dola mia mbili ana laki tano hapa aende zake Pemba akafanyie nini.

Mhe. Mwenyekiti, utalii meli hakuna, boti hakuna, meli moja hiyo imekaa kama hirizi tunaitizama hiyo hiyo tunapakiana kama makumbi maana yake sasa idadi haipo tena. Mimi ninachosema tunakwambia tena na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ananisikia ile meli siku ya kufanya hatari nayo tutakuja kukumbuka, meli sasa hivi inapakiwa na lazima ipakiwe hatuna usafiri mwengine. Serikali lazima nayo ichukue jitihada sasa hivi za makusudi kuhusu Kisiwa cha Pemba hatuna usafiri, hatuna usafiri wa Tanga, hatuna kabisa tumerudi kwenye maboti sasa sijui tunakwenda wapi. Lazima tukubaliane kwamba usafiri upatikane hata kama ni meli gani lakini tuweze kuziita zije, meli moja ile ni hatari hata ikimalizika ile ikipata ajali ya kwenda kuisaidia haipo. Kwa hiyo, ningeomba sana suala la usafiri likashughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ndege nazo halikadhalika imekuwa ndogo ndogo nyingi ambazo zinahitaji sasa hivi tuwe na ndege kubwa Pemba, watu wamekuwa wamehamasika kupanda ndege lakini ndege zenyewe ndogo. Sasa ningeomba sana pamoja na utalii na ninavyochangia nenda kwenye mashirika ya ndege kaangalie nani anayekusaidia, punguzeni masharti ili ndege zije kule Pemba kwa sababu unajua kama hakuna kwa kwenda tena ukifika Pemba ushafika mwisho. Kwa hiyo, lazima kule tuwe na usafiri wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, Pemba tatizo jengine matangazo hakuna, ukitizama TV unatizama watoto tu wanaimba nyimbo *ZBC*, hayaoneshwi mambo ya Pemba yalioko kwenye utalii, hakuna vipindi vya utalii, hapa wanatwambia tu lakini hakuna vipindi vya utalii, vipindi vya utalii kuonesha Pemba kuna nini, hakuna. Kule kuna mambo mengi, kuna watu wengine wanavutika na uganga tu na mambo mengine ya matambiko, vipo vitu waambie waje watu. Kuna huo msitu wa Ngezi nani anayeujua haujui mtu na wapo wadudu chungu nzima wa kuweza kutalii. Sisi mpaka sasa hivi tumeshindwa kufanya chochote kuwaunganisha baina ya tumbili

wale walioko Unguja na Pemba hawawezi wakazaana na tumbili mwengine. Ili mradi hatuwezi kuchanganya wanyama wala kitu gani sasa sisi tumekuwa sijui tunafikia wapi.

Kwa hivyo, ningeomba kule Pemba kwenye msitu wa Ngezi kuna mambo mengi, kuna maji kule yanayotoka yamekaa kama zamzam hakuna anayejua, kuna maji kule wengine wanasema ukiyanywa sijui unapata faida gani hakuna anayejua, wala hayaandikwi, wala hayatangazwi. Kwa mfano kwa Mhe. Bahati Khamis Kombo, Jimbo la Chambani kuna maji kama shaba au dhahabu yanaongeza mpaka nguvu za kiume, yana mambo chungu nzima hayatangazwi, ni vitu ambavyo watu tumevikalia. Wewe hata ukenda Pemba uliza nini wanasema karafuu, si karafuu tupu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Bado dakika tano? Mheshimiwa nina mambo mengi ya utalii huku lakini basi. Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mambo ya ajira, lengo na madhumuni ya serikali kila tunapofanya miundo mbinu ya kuweza kufanya viwanda na kuweza kujenga mahoteli jambo la kwanza ni kuwasaidia Wazanzibari kupata ajira. Leo kila mahoteli unayokwenda watu wanatoka huko nchi za nje wanakuja huku kutafuta kazi na sisi tupo hapo zamani tulikuwa hatusomi sasa hivi shule yetu ipo pale Maruhubi na wanatoa wanafunzi. Lakini mwanafunzi wa kizanzibari akitaka kazi hapati na ni kwa sababu eti ukienda kule wanakwambia eti wazanzibari mara harusi, mara wanakwenda mazikoni, mara sijui wanakwenda kumtizama bibi. Si kweli Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine tungeona tunawaajiri tukaona ndio kweli wanakwenda kuzika kila siku, wanakwenda harusini kila siku, lakini viwango vya elimu wanavyo, kazi wanaweza kufanya. Hizo kazi nyengine wanafanya nani, humu Baraza la Wawakilishi mna mtu mgeni mbona tunafanya wenyewe na tunaweza hata tushindwe huko kufanya kazi za hoteli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naungana na wenzangu twende tukakague wafanyakazi wangapi ambao kwenye mahoteli na serikali ilisema, wafanyakazi wangapi wa Zanzibar wawepo lazima wanaotoka hapa hata kama tutamuajiri mtu *specialist* mle fulani kwamba huyu kwa kazi hii awepo huyu. Lakini kazi za *local* mle ndani hata za kufyagia, kutandika kitanda, mbona watu wana maharusi tele wanafanya wanatandika vitanda washindwe kutandika vitanda hivyo, haiwezekani kazi ndogo ndogo tunaweza na kazi kubwa tunaziweza. Mheshimiwa ningeomba sana hilo liangaliwe kwa undani sana.

Mhe. Mwenyekiti, nasema Uwanja wa Gombani ulifanyiwa kazi ukatiwa taa hazijawashwa tena mpaka leo, umeme unatiwa *unit* tatu tu sijui taa zile zitawaka vipi, kesho na kesho kutwa kuna mechi za usiku zikianzishwa haziwaki tena taa zile na itabidi kazi kubwa ifanyike. Ningeomba wizara kila *weekend* ikawasha taa kule Pemba angalau ukajulikana ule uwanja. Mhe. Mwenyekiti, toka siku zilizotiwa taa mpaka leo haujawashwa tena na hizo taa zilisetiwa zikawa karibu na majumbani badala ya mle ndani. Sasa naomba sana Mheshimiwa taa za Gombani zikafanyiwe marekebisho ya *setting* na kila wiki ziwashwe Jumamosi na Jumapili watu wote watoke wakatizame taa. Watakwenda vijana usiku wakitizama mechi na sisi tujifunze, kuna wengine hawajui kucheza mpira usiku wakicheza wanaona mtu anakimbia kumbe kivuli. Sisi tunaanza kwenda kucheza watufundishe kucheza mpira usiku, unaona juzi hapa tulipata *Zanzibar Heroes* wangecheza usiku wangefungwa mpaka wakakimbia hawajui kucheza na taa usiku. Sisi kule Pemba tuna timu zetu Pemba *combine* nani watuchezeshe watuwashie taa za usiku.

Mhe. Mwenyekiti, jengine naomba sana hawa watu wa utalii wakafanya kazi yao ya utalii. Mheshimiwa katika miji mikubwa sheria sasa za utalii hazipo zipo kwa Mkuu wa Mkoa tu, sheria za utalii hazionekani, ngoma hujui ukapige wapi kila mmoja

mkubwa wala hujui ukakate kibali wapi, utalii bado hatujaujua na ngoma zote utalii na hata msewe, dumbaku, nini. Sasa tujue tu muongozo wa mjini ni upi na ngoma za harusi ni zipi ziwekwe wazi tujue vya kupiga, starehe ziko pahala.

Mhe. Mwenyekiti, Pemba kulikuwa na sinema tatu pale Chake Chake sasa hivi hakuna hata kipande cha sinema, ndio tumebakisha kubakana tu hakuna kwengine pakwenda. Hakuna ngoma hata inayopigwa kila mmoja ndani amejifunika atafanya nini, mawazo yote mabovu yanamjia

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nakuomba umalizie.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Duh! Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la wanawake na watoto, kwa kweli ni suala ambalo mimi upande mmoja nasema wanajitahidi sana ingawa mambo yametukabili sana, lakini mwenzangu hapa alizungumza. Hivyo, tuchukulie tutizame ukweli huyu mtu anayechukua mtoto wa miaka miwili na miaka mitatu, huyu anabaka au ni mwendawazimu, huyu ni nani? Maana yake hii wizara pamoja na Wizara ya Afya hawajatwambia hasa mtu kama huyu ni mwendawazimu au kabaka ana hamu au ana kitu gani. Mimi ninavyojua mtu anavutiwa na msosi ule, lakini mtoto wa miaka miwili yule ni muuwaji sio kubaka na sijui kakusudia nini. Kwa hivyo, lazima mheshimiwa hili litizamwe sana na tuangalie kweli kweli na hawa madaktari wawapime wale wakimkamata tu wapime na wamtizame huyu ni mwendawazimu au nini, hilo mheshimiwa naomba liendelee.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee kwenye hizi sehemu…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nakuomba umalizie muda wako umekwisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, basi niunge mkono hoja, maana buku kubwa sana hili, naunga mkono hoja mheshimiwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Suleiman Sarahan Said sasa mchangiaji wetu wa mwisho kwa muda huu atakuwa Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ambayo imewasilishwa na mheshimiwa makini kabisa, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza naiunga mkono hii ripoti kwa sababu wajumbe wetu kwa kweli wamefanya kazi kubwa, ripoti ni kubwa, wamefanya kazi ya ziada wamevuka wamekwenda mpaka Tanga. Kwa kweli kamati imefanya kazi lazima tuipongeze pamoja na wajumbe wote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze moja kwa moja kufuatilia ukurasa wa 7 ambao umezungumzia masuala ya *ZBC*. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nataka niwapongeze sana Shirika letu la Utangazaji la Zanzibar kwa upande wa redio pamoja na televisheni. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa, wanajitahidi na changamoto ni sehemu ya kazi, mimi nilikuwa tu nataka niwape moyo kuanzia Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi kwamba tusione tabu kupewa changamoto, kwa sababu changamoto sasa hivi dunia ya leo tunatakiwa tuzigeuze ziwe fursa. Kwa hiyo, tusikilize Waheshimiwa Wajumbe maoni yao basi watendaji wakirudi waende wakayafanyie kazi naamini taasisi zetu hizi zitazidi kuimarika kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho nilichokuwa nataka nikiseme kuanzia jengo letu la Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na

Michezo au jengo la Redio Zanzibar pale Rahaleo, nilikuwa naomba mjitahidi kulifanyia maboresho kwa sababu jengo zuri tumejengewa lakini katika hali ya usafi tunaomba kidogo mjitahidi. Kwa kweli kituo kile ndio kinachotupasha habari, kwa hiyo na watangazaji maisha yote wanatakiwa wawe watu nadhifu ambao walingane na jengo vile vile. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nawapongeza sana, isipokuwa hizi changamoto ndogo ndogo zilizoelezwa na kamati kuhusu suala la maslahi ya wafanyakazi wetu hawa wa redio pamoja na televisheni, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri ukae na timu yako muweze kulitatua, kwa sababu mtu akifanya kazi akiwa huku ana madai anasikitika, hata ule ubunifu na ufanisi unakuwa unapungua. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana tuangalie maslahi ya watumishi wetu hawa ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira *ZBC* tumelizungumza kwa muda mrefu sana tokea walipokuwa hawajabadilishwa jina, walipokuwa wanaitwa Redio Zanzibar pamoja na TVZ. Kuna suala la vijana wetu kujitolea kwa muda mrefu na unajua kijana anapojitolea kwa muda mrefu anaweza hata akamshinda yule mwenye elimu yake kwa sababu ile *experience* peke yake inasaidia. Sasa vijana wetu hawa wanapokuwa wanajitolea na kujitolea kwao kazi yao inaonekana kwa sababu mpaka ukaona wananchi wanapata taarifa basi ujue kuna watu wengi walijikusanya wakaweza kushirikiana mpaka taarifa zikawafikia wananchi. Leo inapofika pahala yanapokuja masuala ya ajira wanatoka watu nje kabisa, hatukatai kutoka watu nje kwa sababu kuna sehemu nyengine zinatakiwa na zile taaluma, lakini vile vile na zile kazi ambazo wao wenyewe wanazimudu kwa muda mrefu wameshazifanya basi ni vyema kujaribu kuwaangalia na wao kuweza kupata ajira, kwa kweli walikwisha kujitolea kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la malimbikizo ya wafanyakazi, kuna mfanyakazi mmoja hapa sina haja ya kumrejea kwa sababu

kamati ilimtaja. Nilikuwa naomba sana sana aweze kulipwa malipo yake ili aweze kufanya kazi kwa utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna moja nilikuwa nataka nilizungumze ambalo hili linahusu sana *ZBC Television*, naamini litakuwa linagusa kile kitengo chetu kinachokusanya kumbukumbu za habari.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu sana kuangalia inapofika sherehe za Mapinduzi kitu ambacho kinachonisikitisha kwamba *TBC* wanaonesha filamu za kale za Zanzibar tena unazikuta hata kabla ya Mapinduzi, lakini televisheni yetu hatuioni. Hili kwa kweli halileti afya nzuri, sisi siku zote tunazungumza kwamba kila siku Muungano anatajwa Mwalim Julius Kambarage Nyerere, Mzee Abeid Amani Karume hatajwi, sasa wewe utegemee kwamba Mzee Karume akatajwe upande wa pili baada ya Mzee Karume kumtaja sisi ili na wenzetu wakapokea. Lakini *TBC* wamejitahidi kwamba wao wanatangaza mpaka yale ma-*rickshaw* waliokuwa wanabebwa mabwanyenye kipindi hicho, leo *ZBC* hatuioni. Mimi kitu ambacho ninachokiomba kwa sababu najua kuna mashirikiano makubwa baina ya *ZBC* na *TBC* hebu kaeni pamoja muweze kuzipata zile filamu ili unapofika ule wakati wa sherehe za Mapinduzi na sisi tuweze kuonesha.

Mhe. Mwenyekiti, unajua ukiangalia rika la vijana wengi *manpower* kubwa sasa hivi wengi wao hawakuyaona Mapinduzi na ndio maana wanakuwa wanababaishwa babaishwa sana, mtu akija na maneno yake anababaishwa. Sasa wakiona zile kumbukumbu kwa kweli inatusaidia sana sana. Wafanyakazi wa *ZBC* sasa hivi wanapata nafasi mara kwa mara kwenda China kujifunza. Mnapokwenda China hebu waangalieni wenzenu, mnapokwenda kama utaikuta *studio*, basi *studio* ile inakuwa ya kisasa lakini kuna ile *studio* ya zamani kwenye miaka ya 40, miaka ya 50 unazikuta kule zile kumbu kumbu. Sasa na sisi tuige

mifano ile mizuri ili kuhakikisha kwamba tunaweza kufaidika na zile kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye ukurasa wa 9 hapa limezungumziwa suala la Gazeti la Zanzibar Leo. Wenzangu wamelizungumza suala hili na mimi vile vile nachangia katika hili kwa sababu gazeti ni mali yetu. Gazeti hili tumeliunda kwa shangwe tunalipongeza lakini lazima tufike pahala chombo hiki ni kweli chombo cha serikali, lakini hatujawakataza kufanya biashara na ndio maana tukaunda gazeti tukasema liuzwe.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri rudi ukakae na timu yako tuangalie mahesabu kama kuendelea kulichapisha gazeti Tanzania Bara linaleta tija si lazima kulichapisha Zanzibar tuna shughuli nyingi tu za kufanya. Mitambo yetu ya *Government Press* pale tuna shughuli nyingi za kufanya kwa sababu gazeti ni matangazo, chombo chochote cha habari biashara yake inakwenda na matangazo. Sasa utakuta Zanzibar ukiangalia udogo wetu na mazingira yetu na *population* vile vile inapelekea kwamba kuna uchache mkubwa wa matangazo. Kwa hiyo, tuangalie *marketing* kama gazeti kwamba tukilichapisha Bara linaleta tija, basi mimi nadhani wala tusione tabu kwa sababu kama walivyosma wenzangu zibakishwe kopi chache ambazo zitaweza kuuzwa Zanzibar ili kuweza kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, kama ingelikuwa tuna zile *frequent fly* hapa Zanzibar lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi viwanja vyetu vya ndege ikishafika saa mbili, saa tatu sana zile ndege kubwa zinazokwenda nje ya nchi ndio zinatembea saa tano mpaka na kuendelea. Kama ingekuwa kuna zile *charter frequent* mimi nafikiri tungeliweza kuchapisha magazeti yakafika Dar es Salaam ili yakaweza kusambazwa mikoani. Wenzangu wamezungumza pale kwamba mabasi yanaondoka alfajiri kubwa kwa hiyo inakuwa si rahisi kuweza kuyawahi. Kwa hiyo, naomba sana

mkae hii ni changamoto hatupendi kuona gazeti linakuja hapa linalalamika kwamba linakosa faida.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna huduma hapa ambazo zinatolewa na taasisi yetu hii, hapa tunaambiwa mambo ambayo haikuridhika kamati, inasema changamoto ya Shirika la Magazeti ya Serikali. Hapa kuna deni tumeambiwa kwenye kamati taasisi za serikali zinadaiwa shilingi milioni 184,000,000 na zile za binafsi ni milioni 138,000,000. Mhe. Machano Othman Said nilimsikia katika mchango wake aliuliza vizuri sana, tuambiwe taasisi gani za binafsi ambazo zimefika pahala mpaka zikawa zinalimbikiza madeni kiasi kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa serikali mimi nadhani hapa tutoe fatwa kwamba katika bajeti za wizara zote tunatenga mafungu, yaani katika yale mafungu ya *stationary*. Kwa hiyo, mimi nadhani tunampa changamoto Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, tunaomba kwa sababu hamkutulea orodha ya zile taasisi zinazodaiwa. Naomba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ukafanye kazi uletewe zile taasisi mpaka ikifika wakati wa mwezi Juni kama taasisi hizi hazijalipa tuje tuwakamate kwenye bajeti fedha hizi zitoke kwa lazima. Hatuwezi ikawa sisi kazi yetu kutaka habari tu lakini wakati wa kuchangia ili kupata zile habari tukawa tunaumizwa. Kwa hiyo, hili Mwenyekiti sisi tutakuwa pamoja na wewe na kamati kuhakikisha kwamba zile taasisi za serikali kwa sababu fedha zake tunapitisha kwenye bajeti ili ziweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, hili nitaliunganisha pamoja na taarifa nitakayokuja nayo na kamati yangu kuhusu suala la bili za maji na bili za umeme katika taasisi mbali mbali za serikali. Kwa hiyo, sasa hivi lazima tuhakikishe kwamba yale mafungu tunayoyapitisha yanatumika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu hapa ukurasa wa 13 imeelezwa Tume ya Utangazaji. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana tume hii lakini nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti pengine na waziri tunajua ataleta jawabu baadae, lakini kama kutakuwa na ufafanuzi Mwenyekiti labda pia na wewe utusaidie, kwa sababu Tume ya Utangazaji wao ndio wanao-*control* masuala yote ya vyombo vya habari. Hivi sasa kumeibuka televisheni nyingi ambazo ni *online TV*. Sasa Tume ya Utangazaji naomba kwanza ufunguaji na usajili wa hizi *online TV* kuna taratibu gani? Je, kuna kanuni ambayo inaongoza na inayosimamia?

Nasema hivi kwa sababu Zanzibar imekuwa kama mvua za vuli mara moja kuna wingu linatanda mvua inanyesha. Sasa hivi tupo katika hali ya amani na utulivu lakini katika miaka miwili tunayokwenda mbele tunakwenda kwenye wakati wa uchaguzi, tusije tukaona televisheni ambazo ziko *online* ambazo huwezi ukazikamata moja kwa moja wakaja wakaanza kutangaza vitu ambavyo viko kinyume na sheria. Sasa hili nilikuwa naomba sana Tume ya Utangazaji waje watwambie basi Mhe. Waziri siku atakayotuletea ripoti au kama kuna mambo mengine wanaweza wakayajibu bila ya kusubiri muda mrefu kwa sababu maana ya ripoti kutaka kujua.

Kwa hivyo, tunaomba sana yale ambayo wanaweza kutujibu katika kipindi hiki wanaweza wakatujibu, yale ambayo wanahisi ya kuyafanyia kazi watakuja kutujibu katika kipindi kijacho. Mimi hapa kitu ambacho nilikuwa nataka nijue kwamba je, ule utaratibu wa ku-*control* hizi *online TV* wana-*control* vipi kupitia Tume ya Utangazaji.

Vile vile suala la ajira wenzangu wamelizungumza katika vyombo vya habari binafsi ni kweli wanalalamika, kazi wanafanya nzuri lakini wanashindwa kufuata lile agizo la serikali la kuwalipa kima cha chini cha mshahara. Sasa hili nilikuwa naomba pia Tume ya

Utangazaji iweze kulishughulikia, lakini Mhe. Waziri na yeye kwa sababu ndiye msimamizi wa taasisi hii tunaomba vile vile aweze kulishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 16 wa hii ripoti…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma naomba umalizie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nimalizie, hee! Haya, acha nimalizie kwenye suala zima la utalii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napongeza jitihada za serikali kupitia wizara kuhusu kuutangaza utalii. Kwa kweli utalii sasa hivi unaimarika kama tunavyoona katika ripoti ya kamati watalii wanaongezeka, lakini kwa kweli serikali yetu na hili tunaomba sana, sana, serikali yetu tujaribu kulisimamia suala zima la kuhakikisha kwamba utalii wetu hauyumbi.

Sasa hivi kuna maagizo ya ghafla yanayokuja ambayo yanayumbisha kidogo uchumi wetu wa Zanzibar. Sasa hivi kuna mahoteli ambayo yamo katika *construction*, tayari vifaa vyao vya ujenzi vimekwama katika Bandari ya Mombasa. Kuna agizo la Kamishna wa *TRA* Tanzania kwamba makontena sasa hivi ambayo yanapitia Mombasa yasije Zanzibar moja kwa moja yapitie Tanzania Bara. Sasa hii utaona kwamba ni suala halihusu moja kwa moja wizara lakini linagusa kwa sababu mle mna vifaa vinavyotumika hoteli, kuna vyakula, samaki, vifaa vya usafi, lakini vile vile kuna vifaa vya ujenzi. Sasa hili mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali waweze kuhakikisha kwamba ili uchumi wetu na uwekezaji wetu usiyumbe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naendelea kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, pia pamoja na wizara zote ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, pamoja na Wizara

ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaakhirisha kikao naomba niwakumbushe kuwa ile semina kuhusu maradhi yasiyoambukiza itafanyika leo mara baada ya kuakhirishwa kikao hiki katika ukumbi wa juu. Nawashukuru sana naomba kuakhirisha kikao mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 72 ya Viwango vya Idadi ya Wajumbe katika Baraza, tunaendelea lakini nasema hata robo ya watendaji humu ndani hatujafika. Sasa tunatumikia wananchi na tumechukue *commitment.* Je, ni kweli tutakuwa tunawatendea haki kwamba tunakwenda kwenye kikao kama hiki cha kujadili ripoti kama hii, lakini ukiangalia uhalisia hata watu 25 hatujafika humu ndani. Naomba utaratibu wako Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe nakushukuru sana kwa *concern* yako ambayo unaielezea na ni kweli kwamba Wajumbe waliokuwemo humu ni wachache, lakini naona kwamba Wajumbe wengi wanaingia sasa hivi. Kwa hivyo, naomba tuendelee kwa sababu sasa hivi Wajumbe wanaingia ingia na itakuwa pia si busara kuacha hiki kikao halafu baadae wakiingia tukarudi tena, tunapoteza wakati vile vile. Kwa hivyo, nashukuru kwa utaratibu

lakini ni maamuzi yangu nahisi kwamba tuendelee. Ahsante Mhe. Mjumbe.

Waheshimiwa tunaendelea Mhe. Shehe Hamad Mattar na ajitayarishe Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ambayo leo ndio tunaijadili hapa.

Mhe. Naibu Spika, sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema na kuweza kufika hapa kwa wakati nikaweza kutoa yangu machache katika ripoti hii iliyo mbele yetu ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nianzie michango yangu katika ripoti iliyopo mbele yetu katika sehemu nzima ya Sekta ya Habari. Sekta ya Habari kama ilivyoelezwa katika ripoti hii kwa kweli ni sekta muhimu sana duniani kote na mimi nakubaliana nayo hiyo, kwamba kupitia habari inakuwa mtu unaona kama dunia ni kiganja kwamba utaweza kujua taarifa mbali mbali zilizokuzunguka katika dunia kupitia chombo hiki. Kwa hivyo, ni muhimu sana kuwepo katika nchi na kwa upande wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kweli nimpongeze sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kusimamia vyema kuona kwamba chombo hiki kinafanya kazi kama inavyostahiki na kupelekea kupata vifaa mbali mbali ambavyo vitawezesha kufanya shughuli zao. Kwa hivyo, na mimi niipongeze sana ripoti hii na naiunga mkono kwanza kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuiunga mkono ndani yake kuna mambo kidogo tunaweza kuchangia kama hivi ifuatavyo kwenye Sekta ya Habari.(*Makofi*).

Wizara hii mafanikio yaliyopatikana ni makubwa lakini bado yanahitajika zaidi. Kwa sababu ukiangalia vyombo vyetu vya habari kama televisheni na redio ndio vyombo vya mwanzo katika Zanzibar hii takriban Afrika Mashariki vinaongoza, lakini kuna mambo mengine bado hayajafikia. Niendelee kuiomba serikali nayo kuitupia jicho sana ili tusiwekwe nyuma kulinganisha na vyombo ambavyo vilikuja baadae vikaibuka vikawa vinatengeneza mambo yao katika mpangilio mzuri sana. Na sisi tunatakiwa tuwe ni walimu, wizara yetu wawe ni walimu wa zile taasisi ambazo zinaibuka siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala zima la ripoti hii katika Shirika la Utangazaji la *ZBC*. Hili ni shirika kwa sasa hivi baada ya kuunganika kama ilivyokuwa Sauti ya Tanzania Zanzibar na Redio, lakini kuna mambo ambayo mimi nimeyaona hayapendezi. Katika kufanya kazi kwao Shirika hili la Utangazaji halipendezi na ni pale inapotoa taarifa ambazo zinatoka kisiwa cha pili cha Pemba huona kwamba taarifa zile hasa kama vile Wawakilishi tunafanya shughuli zetu za maendeleo katika majimbo yetu au hata wakati mwengine na baadhi ya watu wengine, isipokuwa zile shughuli za viongozi wakuu tu wa serikali zinaweza zikafika siku ile ile kwa wananchi wakajua kuna nini.

Mhe. Naibu Spika, lakini inapofika kama Mwakilishi anafanya jambo muhimu sana la kitaifa katika maeneo yake habari ile wewe unaweza ukafika siku mbili ndio uweze kuiona, aidha kwenye mawio au kwenye taarifa ya habari katika televisheni moja kwa moja. Hili ni jambo sio zuri hasa ukizingatia mwandishi huyo wa habari humpati kirahisi kwa kwetu Pemba. Kwa sababu mwandishi wa habari anatakiwa atafute habari azilete, lakini sisi kule Pemba tunawatafuta wandishi wa habari tuwalishe habari na tena kwa gharama. Sasa haipendezi kuona kwamba leo mwandishi wa habari unamgharamia, unamchukua unamlipia gharama zake zile na leo unakaa kwenye chombo kama hiki unasikiliza taarifa zako uzione, unaona siku inapita. Naomba sana waziri

anayehusika aliangalie hili, tutafute namna gani ambayo taarifa kama hizi nazo kwa watu ambao kama sisi na wengine watatoa habari zao pale au matukio yao yaweze kuonekana moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, ni wakati uliopita tu nilikuwa nikiona bahari zinafika moja kwa moja alipokuwa Marehemu aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkoani. Yule ilikuwa taarifa zake siku zote zinaonekana, akiwa anakwenda kutembelea shamba la mikarafuu au anakwenda kwenye sehemu yoyote ile siku ile ile inaonekana sijui alikuwa anafanya nini, lakini kwa nyengine zote zinaweza zikafika siku mbili. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Naibu Spka, suala hili Waziri aliangalie na atafuta namna gani bora ambayo itaweza kuwa habari zetu za kutoka Kisiwa cha Pemba ziweze kufika moja kwa moja bila ya matatizo.

Jengine ni kuhusu watangazaji. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo tunaitegemea kupitia Shirika letu la Utangazaji kuona kwamba Kiswahili ndio kinatangazwa vizuri, kinazungumzwa vizuri, kwa sababu Zanzibar inajulikina kwamba ndio chimbuko la Kiswahili hapa duniani kote. Karibuni tumeweza kufanya kongamano la Baraza la Kiswahili la Kimataifa kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwa leo huwa ninashangaa sana, waaandishi wao wa habari walikuweko kule kwenye kongamano kama lile, lakini wakati wanapotekeleza mambo yao naona ni kinyumenyume katika kukilinda Kiswahili chetu kisiweze kupotoshwa. Kama pale unapoona kwamba mwandishi wa habari anazungumza lugha hata vile vina havifanani yale maneno.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano anapotangaza matangazo ya vifo, sijui kama ni Kiswahili sahihi, husema kwamba 'anasikitika kutangaza kifo cha mjomba yao'. Hiki ni Kiswahili sijui kama ni Kishwahili sahihi. Kwa hivyo, watu kama hawa wao Wizara ya

Habari wanatakiwa watafute maneno ambayo watoto wetu watakuwa wanayaiga yakiwa ndio maneno halisi, hili ni jambo ambalo nimeligundua na mengineyo.

Jambo jengine kinachonikera katika chombo chetu hiki ni pale tunapozunguma kwamba kulinda mila zetu. Mila zetu za Kizanzibari, utamaduni wetu hasa katika vipindi vinavyorushwa na *ZBC* baadhi ya wakati. Kuna vipindi kwa kweli unaviangalia huwezi kuvitizama ukiwa uko na mtu maharimu wako. Hata juzi kitendo kama hicho nilikiona mara narudi hapa Barazani kufika saa nane nikakuta vinarushwa vipindi wanatuletea mambo ambayo kuyatizama sio wakati wake. Kama vile alivyosema Mhe. Rais wetu wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwamba, wanatuonesha viungo ambavyo kwa wakati ule si wakati wake kuviangalia wanatulazimisha na wakati mwengine mazingira ni mabaya. Naomba sana wanaochuja vipindi hivi na kuangalia kwamba vinarushwa vipi, waviangalie na kama zipo kanda kama zile waziondoe mara moja ili tuweze kulinda zile mila zetu na tabia ya Kizanzibari, tusizungumze kwa maneno tu, tutekeleze kwa vitendo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika masuala ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika sekta nzima ya kazi. Mhe. Naibu Spika, katika sekta ya kazi sehemu ya Kamisheni ya Kazi kwa mujibu wa ripoti hii na ndio ilivyo iliundwa kisheria kwa Sheria Nam. 11 ya mwaka 2005. Katika ripoti hii imetueleza kwamba iliweza kutekeleza majukumu yake ambayo ni kufanya ukaguzi, kusuluhisha migogoro ya kikazi pamoja na kukuza mahusiano mema kazini, haya ni miongoni tu mwa majukumu ya kamisheni hii. Pia katika ripoti hii imetueleza kwamba wameweza kutembelea taasisi 260 kwa Unguja na Pemba lakini kwa bahati mbaya Kamisheni hii haikueleza kwamba ni ngapi ambazo zimetekeleza yale majukumu yake yaliyopangiwa au yaliyoagizwa na serikali ya kuhusu kutekeleza kima cha chini cha shilingi 300,000 kwa mfanyakazi wa kima cha

chini. Hili hawakulieleza hapa ni taasisi ngapi ambazo zimeweza kutekeleza katika hizo 260. Naomba watakapofika kutoa majibu ya ripoti hii basi watueleze kwamba ni taasisi ngapi hadi sasa zimeweza kutekeleza agizo hili na kama halitekelezeki basi tuone taratibu nyengine, kwa sababu inakuwa ni kikwazo lakini si vizuri kuona kwamba mpaka leo serikali ilisema hivyo kwa sababu anapozungumza Waziri ni serikali haijatekelezwa.

Kwa mfano, leo tunayo hapa taasisi ambayo ni kubwa kwa Zanzibar ambayo ni *Global Hospital.* Mhe. Naibu Spika, katika utafiti wangu hospitali hii ni kubwa ninavyoiona na ndivyo ilivyo hata malipo yake ukienda pale ni makubwa, lakini bado kima cha chini kinalipwa shilingi 170,000 mpaka leo hii sijui kwa nini, tusingetegemea wafanyakazi kama wa pale waweze kufanyiwa mambo kama hayo.

Mhe. Naibu Spika, kama hiyo haitoshi pia vile vile Kamisheni hii ya Kazi ina wajibu kuangalia maslahi ya wafanyakazi yanakwenda vipi na mahusiano kama ilivyoelezwa. Leo pale pana ubaguzi wa kimapato na kiutendaji. Kwa mfano, watu ambao wana sifa moja ya udaktari pale kama ni *nurses* au madaktari wanapishana kimishahara, wale wageni wana mishahara yao na wazalendo wana mishahara yao, kwa nini iwe hivyo. Sekta ambayo inahitaji mashirikiano ya juu kabisa haipaswi kwamba kila mmoja amtupie mwenziwe. Leo kama ni daktari anajiona kwamba mimi ndio nina sifa ya *degree* au *diploma* kwa nini Watanzania Bara alipwe mshahara mwengine mimi wa Zanzibar nipangiwe mshahara mwengine. Hapa tutakuwa tunafanya kazi ambayo tunatengeneza migongano, kitu ambacho si kizuri katika sekta kama ile ya afya.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana hii Kamisheni ya Kazi ifike pale ikaangalie hili jambo linafanyika. Kwa sababu ubaguzi ni tendo baya sana, hata Rais wetu Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikemea sana jambo hili akasema, naomba ninukuu

kwamba: "Ubaguzi ni dhambi kubwa sana, tuichukie kwa nguvu zote na tukianza dhambi ya ubaguzi tutaendelea kufanya dhambi hii kama vile kuendelea kufanya dhambi ya kula nyama ya mtu utaendelea tu". Nakumbuka maneno haya. Kwa hivyo, na sisi tuiangalie dhambi hii ya ubaguzi haipatikani pale, kama ni madaktari wote wana sifa moja kwa nini waweze kubaguliwa hawajisikii vizuri.

Mhe. Naibu Spika, itafikia wakati kwamba daktari pale ana mgonjwa anapata matatizo badala ya mwenzake kumsaidia anatafuta chumba chengine kujiweka na akamwambia shauri lake ni lake mwenyewe kama atakufa au atapona, anayeumia ni mwananchi aliyefika pale. Kwa hivyo, tuliangalie sana suala hili la ubaguzi katika sekta zetu kama wenzangu walivyozungumza hapa leo utakuta hoteli ina wafanyakazi wengi wa kigeni wazalendo hawapo maslahi yao pia vile vile ni madogo kwa wale wazalendo. Kwa nini iwe hivyo, punda wetu wenyewe tupandishwe mkiani?

Mhe. Naibu Spika, suala zima la mahusiano mazuri katika sehemu za kazi. Ni vyema sekta kama hii kukagua kwamba je, hawa viongozi wanao utaratibu wa kukaa na wafanyakazi wao. Kwa sababu katika taasisi za serikali na tunawaona Mawaziri wanafika katika wizara kuna wakati wanakutana na viogozi, lakini kuna wakati wanakusanya wafanyakazi wote kuwasikiliza kero zao na shida zao na baadae wakaweza kuzifanyia kazi. Naomba sana na hizi taasisi za binafsi waelekezwe jinsi gani ya kuweza kukaa na wafanyakazi wao wasiwe wao ni watu wa kushusha amri tu, lakini kuna wale wafanyakazi wa chini wanaweza kutoa mawazo ambayo na wao wanayaona yanaweza kupeleka mbele taasisi ile wasiyadharau, lakini leo ni jambo la ajabu sana na nadra sana kusikia taasisi ya binafsi inakaa na wafanyakazi wake.

Mhe. Naibu Spika, hiki ni kilio tayari nimekipata katika wafanyakazi taasisi kama hizo za binafsi ambazo zinafanya

mambo kama hayo. Naomba sana tufanye marekebisho na wao wajisikie ni sehemu ya kuchangia katika taasisi ambayo wanaifanyia kazi, ili wakifanya hivyo kila mmoja atajisikia kufanya kazi kwa raha kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika upande wangu naunga mkono kwa asilimia mia moja ripoti hii na niwapongeze sana waliyoyaona humu ni kweli nayaunga mkono kwa asilimia mia moja ahsante kwa kunipa fursa hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Rashid Makame Shamsi, baadae atachangia Mhe. Jaku Hashim hayupo. Kwa hivyo, atafuata Mhe. Hassan Khamis naye hayupo, kwa hivyo atafuata Mhe. Said Omar Said.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa michango yangu katika ripoti hii inayohusiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza mawaziri wa wizara zote mbili pamoja na watendaji wake juu ya majukumu yao na utendaji wao katika kufanikisha malengo ya mipango ambayo wameipanga. Vile vile niipongeze Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa ripoti yao nzuri, iliyopangika, iliyosheheni mambo mbali mbali ya mafanikio lakini na changamoto. Nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Suleiman Ali kwa uwasilishaji wake makini, pia niwapongeze wajumbe wenzangu wote ambao wametangulia katika kuifanyia haki ripoti hii kwa kuchangia ile michango yenye nia ya kuweza kuleta maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaelekea katika mambo matatu kwa leo, najua mambo mengi yameshachangiwa lakini na mimi niweze

kuweka msisitizo katika baadhi ya mambo. Lakini niseme tu kwamba changamoto ni sehemu ya maendeleo. Kwa hivyo watendaji wa wizara hizi tunaowajadili katika ripoti hii wasivunjike moyo pale ambapo tunachangia changamoto mbali mbali. Kwa sababu tutakapokuwa tunafanikiwa katika kupunguza changamoto ndio tunapelekea sekta hizi kuweza kuendelea zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nije ukurasa wa 19 katika suala zima ambalo wenzetu wameliona, wameliibua, tatizo la ukosefu wa mafuta ya petroli ambalo limeweza kuathiri harakati katika sekta ya utalii katika mwezi Disemba mwaka jana.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wameweza kubaini hii na ni dhahiri kwamba kuadimika kwa mafuta kuliweza kuathiri na kuleta usumbufu mkubwa kwa baadhi ya watalii wetu. Hii ni moja kati ya sekta ambayo tunaitegemea kuweza kupata pato kubwa sana la fedha za kigeni kuliko sekta nyengine. Sasa kunahitaji sana juhudi za makusudi kuweza kuona kwamba tunapunguza changamoto mbali mbali ambazo niseme kwamba hazina ulazima kama tutakuwa tumejipanga vizuri.

Suala la ukosefu wa mafuta sio tu linaathiri sekta ya utalii, lakini linapotokea linaathiri karibu sekta zote. Kwa sababu mafuta ndio usafiri na unapoathiri shughuli za usafiri katika nchi maana yake shughuli za wananchi za maisha ya kila siku zinaathirika……

Kwa hiyo, taasisi inayohusika *ZURA* kwa kushirikiana na wizara basi tuiombe sana ijipange vizuri katika kuona tunapungukiwa na matatizo ya mara kwa mara, hivi tunavyozungumza vituo vingi vya petrol vina foleni. Maana yake tumekuwa na upungufu Disemba tuna upungufu wa mafuta Febuari. Sasa *trend* ya namna hii ikiendelea maana yake kule tunakotaka kwenda kiuchumi hatuwezi kufika. Kwa hiyo, tuwaombe sana wenzetu hii hali wakati mwengine inatia aibu wageni wanapokuja nchini na wakaona watu wako katika foleni za mafuta. Tuiombe sana *ZURA*

kwa kushirikiana na wizara kujipanga vizuri ili kuweza kuepuka matatizo ya namna hii ambayo yanaweza yakaathiri sekta mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka katika sekta hii ya utalii jinsi gani inavyoathiriwa na mambo mbali mbali yakiwemo uhaba wa mafuta. Nije sasa katika ukurasa wa 21. Katika ukurasa wa 21 wenzetu walizungumzia kwenye Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu pamoja na Utamaduni. Mhe. Naibu Spika, katika sekta hizi wenzetu hawakuridhika na baadhi ya mambo ambayo wameyataja hapa. Moja wapo ni matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili na wamesema kwamba hivi sasa kumekuwa na matumizi ya maneno kadhaa ya Kiswahili ambayo siyo sahihi huku katika sehemu mbali mbali ikiwemo vyombo vya habari, huku Baraza la Kiswahili likifumbia macho makosa haya.

Mhe. Naibu Spika, kwanza hapa niwatetee Baraza la Kiswahili. Baraza la Kiswahili mimi naona hawayafumbii macho matatizo ya matumizi sahihi ya Kiswahili. Baraza la Kiswahili linajitahidi sana katika kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi. Baraza la Kiswahili linafanya makongamo mbali mbali hata mwaka huu wamefanya kongamano. Baraza la Kiswahili linatumia vipindi vya redio na *TV* katika kuelimisha matumizi sahihi ya Kiswahili. Lakini Baraza hilo hili la Kiswahili linajitahidi sana katika kuandika makala kuandika vitabu kuandika makamusi mbali mbali ya lugha ya Kiswahili ikiwemo ya Lahaja zote zinazozungumzwa Zanzibar.(*Makofi*).

Kwa hiyo, wenzetu hawa lazima tuwapongeze na nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Rais jinsi gani anavyosisitiza matumizi sahihi ya Kiswahili. Tatizo Mhe. Naibu Spika, lipo katika hawa waelimshwaji au sisi tunaoelimishwa na tunaosisitizwa juu ya matumizi sahihi ya Kiswahili, sisi ndio tuno matatizo. Sasa mfano juzi tu kwamba Baraza la Kiswahili limethubutu kuweza kusambaza Kamusi za lugha fasaha kwa vyombo vya habari vyote

vya binafsi na vya Serikali. Hii ni juhudi moja ya Baraza la Kiswahili, kuweza kuona hata hivi vyombo vya habari viwe vya binafsi au vya Serikali vinatumia matumizi sahihi ya Kiswahili Fasaha. (*Makofi*)
Sasa wenzetu lazima tuwapongeze lakini tuwalaumu hawa wanaosisitizwa.

Sasa ikiwa vyombo vya habari vinatumia lugha ya Kiswahili isivyo fasaha, hapa ni tatizo na hususan kama itakuwa ni chombo cha serikali. Lakini ni ukweli usiofichika kwamba vyombo vingi vya binafsi ukivisikiliza vipindi vyao, basi lugha inayotumika mimi miweze kusema sijui lugha ya mitaani zaidi au ya kihuni zaidi. Sasa hapa lazima Baraza la Kiswahili linasaidia lakini na zile taasisi ambazo ndio muhimili wa kuweza kutoa habari ikiwemo Tume ya Utanganzaji basi ziweze kufanya wajibu wake, ili kuweza kuona kwamba vyombo vya habari basi vinazungumza au zinatamka maneno ya Kiswahili kwa ufasaha kabisa.

Lakini katika hilo Mhe. Naibu Spika, niende sasa katika suala zima la sensa ya filamu. Wenzetu wamebaini hapa kwamba kuna filamu zisizo na maadili, wamesema baadhi ya filamu zenye maudhui na taswira isiyokubalika katika maadili yetu huoneshwa katika vituo vyetu au kuzagaa katika maduka ya kanda za *video*.

Mhe. Naibu Spika, tuwapongeze wenzetu sana kwa kuweza kuibua hili. Hili Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ni tatizo, ni tatizo na linachangia mmong'onyoko wa maadili katika visiwa vyetu ya Tanzania kwa ujumla. Nimpongeze sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuliona hilo. Kuna filamu Mhe. Naibu Spika, huwezi ukazitizama ukiwa na watoto wako na nyengine zinarushwa na vyombo vyetu vya habari vya taifa ukiacha vile vya binafsi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba filamu ambazo zinaoneshwa zinafanya vijana wetu waweze kupungukiwa na

maadili ambayo sisi tumeyazoea. Lakini hata baadhi ya wazazi wanashabikia hili. Sasa tuombe sana sensa ya filamu iweze kutekeleza majuku yake. Lakini vile vile vyombo vya habari viweze kuchuja hivi vipindi ambavyo au filamu ambazo zikioneshwa inakuwa ni karaha kwa jamii.

Ukweli usiofichika Mhe. Naibu Spika, tumefikia pabaya sana utakuja waigizaji, wanenguaji wakinengua nusu uchi katika muziki mbali mbali na filamu mbali mbali, hii ni hatari kwa taifa letu na haya wakati mwengine ndiyo yanayochochea vijana wetu kuingia katika mambo mbali mbali yakiwemo ya kubaka. Kwa hivyo, tuweze kuziona *factors* hizi ambazo zinachochea katika athari nyengine za udhalilishaji ili tuweze kuzizuia mapema hatujachelewa, lakini tukiamua nafikiri tunaweza. Kwa hivyo vyombo vya habari vichukuwe nafasi yake katika kuona kwamba vipindi vinavyooneshwa pamoja na filamu na michezo mbali mbali basi vinaendana na maadili ya Zanzibar na maadili ya Mtanzania kwa ujumla.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuondoka katika suala zima la utamaduni nielekee sasa katika ukurasa wa 24 kuzungumzia au kuchangia kidogo suala zima la sekta ya michezo. Tuwapongeze sana wenzetu wanakamati kwa kazi kubwa sana walioifanya katika kukusanya taarifa hizi kuhusiana na sekta hii ya michezo. Lakini kabla sijenda mbali sana nimpongeze sana Mhe. Rais kwa juhudi anazochukuwa katika kuimarisha michezo na kuwapa moyo wachezaji wetu wa timu mbali mbali, inatia moyo kuweza kuona kwamba Rais wa nchi yuko pamoja sana na wanamichezo.

Mhe. Naibu Spika, ripoti ya mwaka jana ya aina hii tulizungumzia changamoto ya ufinyu wa bajeti ambayo na mara hii imeweza kujitokeza. Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kuendeleza michezo kwa bajeti ambayo inapangwa. Nilieleza mwaka jana mwaka 2016 katika ripoti za bajeti inaonesha kwamba Baraza la Michezo la Taifa, bajeti yake ilikuwa ni shilingi thamanini na nne milioni.

Katika mwaka 2017/18 bajeti yake imeshuka mpaka shilingi sabini milioni na 2018/19 imepanda kidogo kwa asilimia nne.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii kwa kweli kama tunataka kwa udhati kabisa kuweza kuendeleza michezo katika fani mbali mbali, sio mchezo wa *football* tu pamoja na michezo mengine ambayo nayo kwa kweli inatupatia sifa. Kwa mfano juzi juzi tu mchezo mpya huu unaoitwa *beach soccer* ambayo ilishiriki mashindano ya *Copa Beach Soccer* ilipata ushindi ambayo hii kwa kweli ni sifa kubwa sana kwa taifa, ukiacha ile *Zanzibar Heroes* iliyopata nafasi ya pili. Tuwapongeze sana timu hizi kwa uhodari wao na juhudi yao. (*Makofi*)

Lakini tuna nafasi kubwa ya kuweza kuzikuza hata timu nyengine hivi sasa tumo katika maadilizi ya Timu ya *Karume Boys*. Ningependa sana tuoneshe juhudi zetu sisi Wawakilishi mapema kabla ya kuona kwamba wenzetu wako katika mashindano. Nafikiri juhudi zianze katika mazoezi. Lakini na chombo kinachohusika Wizara ya Habari pamoja na juhudi zake basi kuisimamia uzuri timu hii ya *Karume Boys* ili nayo iweze kuleta sifa katika taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari na Michezo inajitahidi sana katika hili na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi anayochukuwa, lakini kwa kweli bado changamoto zipo na inahitaji msaada mkubwa. Tujitahidi sana katika kutafuta wadhamini kama wenzangu walivyochangia ili kuweza kuona kwamba suala la michezo linakuwa na msukumo wa aina yake ili kuendelea kuipatia sifa Zanzibar na vijana wetu kupata fursa ya kuweza kupata ajira kupitia suala la michezo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya michango hiyo, mimi niipongeze sana kamati kwa kuwasilisha ripoti hii lakini niendelee kuwapongeza Mawaziri kwa juhudi wanazochukuwa katika

kuendeleza yale majukumu yao waliyopangiwa. Lakini niwaombe na wenzangu waendelee kuchangia na kuiunga mkono ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana nashukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi. Mchangiaji anaefuata ni Mhe. Said Omar Said baadae atakuja Mhe. Suleiman Makame Ali. Mhe. Suleiman hayupo.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuhudhuria katika .....

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa endelea atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub sawa. Eendelea Mheshimiwa.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii kuhudhuria katika kikao hichi nikiwa katika hali ya uzima.

Lakini pia nichukuwe nafasi hii kukushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Ripoti ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Nataka nichukuwe nafasi hii kwanza kuishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake kwa kazi kubwa waliyoifanya na kutudhihirishia hapa mbele yetu chini ya Mwenyekiti Mahiri Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Naibu Spika, kipindi kilichopita tulipata bahati kwenda katika ziara katika kamati yetu tulipata nafasi ya kwenda Tanzania Bara. Basi baada ya kufuata wiki ya pili iko siku tulikosa vyombo vya habari kule. Sasa tukajiuliza watu wa habari wako wapi, tukaambiwa kuwa leo yupo Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), nikasema loo kumekucha! Kwa hivyo, hatukufanikiwa kupata vyombo hivyo

alivitawala Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) kwa umahiri wake, hongera sana nakushukuru sana (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, neende moja kwa moja kutokana na wakati nianze na ukurasa wa 7. Nataka niende kwenye mafanikio ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC)*. Nataka nichukuwe nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Habari kwa umakini wake ndani ya Baraza hili, kwa umakini wake na nje ya Baraza hili. Nimponge kwa kuitumikia wizara hii vilivyo na kila mmoja kumpa haki yake kwa jitihada yake, nimpongeze sana. Mtu anapofiliwa na mtoto wake hupewa pole na huhaniwa, lakini anapopata mtoto hupewa hongera. Kwa hivyo, nimpe hongera Mhe. Waziri kwa kufanikiwa kupata mitambo mipya na ya kisasa pia kwa ukarabati wa *studio* zetu (*Makofi*).

Lakini pia kwa umakini wa kupata kuweka kumbukumbu za hotuba za viongozi wetu na kuweka kumbukumbu za nyimbo za zamani. Lakini hapa Mhe. Naibu Spika, ningependa na mimi nijaze moja pia kuweka kumbukumbu za Mashekhe wa zamani. Mhe. Naibu Spika, hotuba za viongozi wetu wa zamani ndio dira ya viongozi wetu wa sasa. Hotuba ya viongozi wetu wa sasa ndio dira ya viongozi wetu wa kesho. Hivyo hivyo na miongozo wa Mashekhe waliopita ndio dira ya Mashekhe waliopo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, linapotokea tatizo dogo la kisiasa kwa mfano ikawekwa kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, nchi hutulia ikawa kimya, inapowekwa kumbukumbu ya Marehemu Mzee Abeid Aman Karume nchi yote hutulia kimya. Hii ni kutokana na umuhimu mkubwa wa kumbukumbu na kumbukumbu ya zamani inaongoza leo, kumbukumbu ya leo itaongoza kesho. Mimi nitoa pongezi sana kwa kupata kifaa ambacho kitatuwezesha kuweka kumbukumbu hizi tulizozitaja.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nichukuwe nafasi hii niishauri kwamba kwa kuwa Zanzibar leo hii tuna redio nyingi tafauti na tulikotoka. Sasa ningependekeza kwamba hizo hotuba za viongozi wetu zisikike katika redio zote zilizokuwepo Zanzibar, ziingizwe huu ndio utamaduni tunaotaka tuujenge kwa sababu utamaduni wetu kama alivyotangulia kusema Mhe. Mwenyekiti katika mchango wake kwamba hatuna ubaguzi, tuliufuta ubaguzi zamani.

Lakini la kushangaa utakuta kuna baadhi ya redio baadhi ya Mashekhe wetu waliopita hatujawasikia hata siku moja. Hii ni kinyume hasa na hata na sheria yetu hiyo ya Dini. Zipo redio hujasikia kutajwa kwa mfano Shekhe Mkuu Marehemu Hemed bin Jumaa bin Hemed hatujasikia ambao wale ndio wa wakuigwa, ndio wakufuatwa miongozo yao, linapotokea tatizo aingizwe yule pale aweze kujibu masuala. Lakini utashangaa baadhi ya redio hujasikia hilo, utasikia wengine. Kwa hivyo, ningependekeza redio zote wawekwe hawa ambao wataisaidia na wana lengo la kuisaidia Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye changamoto baada ya mafanikio ni changamoto. Mimi nataka nikubaliane na kamati kwamba tunazo changamoto katika wafanyakazi wetu tulionao humu ambao ni wa *ZBC* ambao tunawaona hawa. Kwa kweli kamati iliona moja ya changamoto ni kutolipwa posho zao stahiki wafanyakazi wa *ZBC* ambao wanaofanyakazi ndani ya Baraza hili la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi hawa tukubali kwamba wanafanyakazi ngumu na wanafanyakazi kwa muda mrefu. Kama sisi hapa tutabakia mpaka asubuhi basi na wao watabakia mpaka asubuhi hapa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mcheza kwao hutunzwa au huangaliwa. Sasa kwa nini tusiwaangalie hawa na wanafanyakazi mbele yetu tunawaona kwa macho hawa, serikali yote ipo hapa inawaona kwa macho. Mhe. Naibu Spika, wapo wafanyakazi

ambao hatuwaoni wanapofanyakazi, lakini sisi tunapokea taarifa tu bilioni 400 zimetumika kwa moja, mbili, tatu na tumewasafirisha hawa na hawa, tumetoa mafunzo haya na haya wala hatujaona kitu hatuko kwenye kazi zao hatujaziangalia kazi zao, hao wanalipwa posho zinazokimu. Je, leo hawa wanaofanyakazi mbele yetu tunaona, serikali yote ipo hapa inashuhudia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niwafananishe wafanyakazi hawa ni sawa na mtu anayepika chai ya maziwa. Mtu anayepika chai ya maziwa haondoki, akiondoka yanafufurika, hawaondoki hawa wanaogopa kufufurika tunao saa zote. Kwa hivyo lazima waangaliwe na wapewe kile ambacho wameahidiwa wapewe na wameshaahidiwa kwa nini wasipewe na kazi wanaifanya.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Sekta ya Utamaduni. Kwa kuwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ina dhima ya kuhifadhi na kulinda mila zetu, desturi zetu na utamaduni wetu wa Zanzibar, bado ina jukumu kubwa na ina kazi kubwa sana wizara hii, inahitaji msaada. Pamoja na kuwa na viongozi mahiri, makini na wenye kujituma lakini bado hii kazi ni kubwa mno. Mhe. Naibu Spika, kurejesha mila za Wazanzibari leo kuna kazi kubwa, kazi ambayo lazima serikali yenyewe iingilie kati. Utamaduni kidogo kuna tofauti na mila, utamaduni ni mitindo linakuja hili mara linaondoka linakuja hili, lakini mila haibadiliki na ikibadilika mila ni mtihani, ikibadilika mila ni mgao kwa jamii.

Kwa mfano, tunapotaja mila yapo mambo mengi ya mila. Mhe. Naibu Spika, tuseme mazishi ni mambo ambayo hayabadiliki na yakibadilika ni mtihani hayo. Ndoa ni mambo ambayo hayabadiliki, matanga hayabadiliki hayo ni lazima yashikiliwe yasibadilike. Lakini leo Mhe. Naibu Spika, yote yameshabadilika, hayo matatu yameshabadilika, kivipi.

Kwa mfano, amekufa mtu fulani katika familia, yule ameacha ndugu wane. Katika ndugu wale wanne wawili hawaendi kaburini si ndugu zake hawafiki kule, kwa sababu gani, utasikia aah! yule aliyekufa ni kaka yangu lakini ana msimamo wa kusoma talakini, unaona kwa hivyo sisi hatuendi kule, ndugu yake anakosa kumzika ambapo ndio mila zetu. Pengine huyo kwenye jamvi lile la matanga hayupo, atasema hawa wanataka matanga na matanga ni haramu. Je, hatujaibagua jamii.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda wangu umeshafika, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii, niseme tu na mimi naikubali na naipongeza na kuiunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wingwi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Said Omar Said. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atafuatia Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza ni- *declare interest,* mimi ni mjumbe wa kamati hii na mengi nimeyasema huko na sitokuwa na mchango mkubwa, lakini nitakuwa sitowafanyia haki wale wananchi wangu ambapo mimi ni mtumishi wao, kwa kuwa kuna kadhia imewagusa humu wananchi wa Jimbo la Paje karibu mwaka wa tisa huu, nitakuwa sijawafanyia haki na unapoambiwa jambo ukaliona ni ovu tumia mdomo wako, mkono wako mwisho ulimi wako ambao ni imani dhaifu.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Paje wana kilio cha miaka tisa. Katika ukurasa wa 18. Mgogoro wa wananchi wa Paje na warusha vishada vya michezo ya baharini kai. Kamati ilifanya ziara maalum ya kuwatembelea wananchi wa kijiji cha Paje ambao wanalalamika kutopata sehemu ya malipo kutokana na shughuli za urushaji wa vishada vya baharini vinavyofanywa na

wawekezaji na wanamichezo wa mchezo huo, hali hii inatokana na kuwa wananchi wa Paje wameacha kufanya shughuli zao za kiuchumi walizokuwa wakizifanya baharini, ikiwemo kusokota kamba, vyau, ufutaji wa pweza, kwachi na upandaji mwani ili kupisha mchezo huo kwa kutegemea kupatikana kitu. Lakini kwa huzuni na unyonge mkubwa mpaka leo hii karibu mwaka wa tisa wameacha nafasi zao kuwapisha watu kwa kutegemea kitu, hata Mwenyezi Mungu hayupo radhi. Mhe. Naibu Spika, wamekwenda wakilalamika na kupanda ngazi na kushuka wakati mwengine wanafanya mazoezi bila kutaka wenyewe kwa hiyari yao, ni usumbufu wa muda mrefu.

Kwa hivyo, niiombe serikali na nafikiri wizara hii sasa hivi imempata mkurugenzi ambaye sina mashaka na yeye Dkt. Lila nimpongeze kwa dhati kabisa. Dkt. Lila ni mtu mwenye mapenzi makubwa sana na wananchi, wananchi wale wamepisha mradi huu uendelee kwa kutegemea kitu lakini mwaka wa tisa huu wananchi wa Paje wamekuwa na kilio hicho, kwa kweli ni kitu kinachosikitisha. Mhe. Naibu Spika, watu wanapata karibu Dola 40, kutoa dola 5 sio kitu kizuri wala hakipendezi, wanaoneemeka ni wageni lakini wananchi wa pale imekuwa kitendawili. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri hii hapa ndio ajira yangu nilipotokea na mimi ni mtumishi, unaambiwa uchunge unga wako kabla haujaingia maji. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri, nakuamini sina mashaka na wewe lakini huu mwaka wa tisa karibu. Niipongeze sana kamati chini ya mwenyekiti wake makini Mwakilishi mzoefu Mhe. Ali Suleiman Ali kufanya ziara ile na wakaiona hali ilivyo, aliwakuta watu wanasikitika wengine karibu ya kulia, kitu hiki hakipendezi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nichukuwe fursa hii kuwapongeza waandishi wa habari wote kwa kazi wanayoifanya ya kuelimisha jamii. Waandishi wa habari wamekuwa kioo kwa kueneza habari, vyenginevyo habari zetu zingetoka zikaonekana, kwa hilo nipongeze kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kidogo kwenye ripoti hii sikuona kuhusu Uwanja wa Mao Tse Tung. Nimpongeze Mhe. Rais kwa ujenzi ule ambapo sasa hivi mazingira ya Uwanja ule yamebadilika na tumeona na mwelekeo wake. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri amshauri Mhe. Rais afanye kama alivyofanya Mhe. Rais Jakaya Kikwete Lumumba pale Dar es Salaam , uwanja ule ukatumika usiku mchana kwa kutiwa mataa. Hata timu ya Bunge ilipiga kambi pale. Kwa hivyo niombe sana na nafikiri Mhe. Rais suala hili hawezi kulikataa, litasaidia afya na kama tunavyojua michezo ni ajira na ni afya. Kwa hivyo uwanja ule utumike usiku na mchana, ili vijana wale pale wende waliokuwa hawapati nafasi asubuhi, wende usiku, wasiopata nafasi jioni wende usiku kwenda kujitoa jasho. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri umshauri Mhe. Rais ili patumike pale na kama serikali haijali hasara kwa wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, tumeona pale Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete Rais Mstaafu alitengeneza kitu cha kileo kabisa, hilo nikuombe mheshimiwa. Lakini vile vile niipongeze kamati kwa kutembelea baadhi ya maeneo kule Pemba na ikawa redio ya Micheweni Mkoani, niwapongeze sana hasa watu wa Micheweni redio yao kule kazi wanayoifanya tumeiona. Mhe. Naibu Spika, wana kilio tu Mhe. Waziri, nafikiri Mhe. Naibu Waziri tulikwenda naye kule kilio chao sio kikubwa kwa kweli watu wanataka kupongezwa wa Micheweni, kazi kubwa wamefanya ya kuwaelimisha jamii. Mhe. Naibu Spika, kulitokea maradhi ya mripuko kule basi redio ile ikafanyakazi, ikaelimisha wananchi wa pale, yakapungua, unajua mawaidha ni kitu tosha.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika tatizo la ukosefu wa mafuta, alizungumza ndugu yangu Mhe. Mwakilishi wa Magomeni. Siku zote husema humu ndani hebu tujaribu, mbuzi anakula majani kutokana na urefu wa kamba yake, tusitake kuiga Tanzania Bara hapa hatujawa tayari. Sasa *formula* hii mliotuletea

imekuwa kizungumkuti, siku zote mafuta yanaadimika, hakuna mafuta kuadimika katika Sherehe za Mapinduzi, kabla ya wiki mafuta hayaonekani wiki mbili au moja, mafuta ndio *engine* ya nchi na ndio nuru ya nchi, lakini tunafanya kitu ambacho hakielekei.

Mhe. Naibu Spika, tumemtafuta mwekezaji mmoja sijui njia gani iliyotumika pale au vigezo gani vilivyotumika pale, tulitegemea itakuwa ndio suluhu au ndio muarubaini hakuna kitu. Narudia tena mbuzi anakula majani kutokana na uwezo wa kamba yake. Tuwe tayari kujipanga kwanza, miundombinu tunayo ya kutosha. Mimi juzi nilipata wakati mgumu sana Mhe. Naibu Spika, na swali ninalo hapa Bungeni kwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, katika moja ya kero za Muungano.

Mhe. Naibu Spika, mafuta yanakwenda Burundi, Rwanda, Zambia na Zaire yanalipishwa Dola 3 mpaka Dola 4. Niliuliza swali Bungeni kwamba Zanzibar wanalipishwa Dola 10 ni kitu cha aibu na ubaya wenyewe serikali kule Tanzania Bara walikiri, swali ninalo hapa, ni kitu cha aibu haielekei. Kwa vyovyote mafuta Zanzibar yatakuwa ghali kuliko Tanzania Bara. Ndipo niliposema wakati mwengine huu Muungano wa upande mmoja tu. Leo mtu pua na mdomo taa huwashi nje kwanza unawasha ndani ya nyumba, ni kigezo gani kilichotumika kulipa Dola 10 sisi. Ukitaka swali lipo hili hapa na bahati nzuri ninalo. Malipo kuhusu utaratibu wa kuingiza mafuta nchini unaosimamiwa na *Petroleum Bulk Procurement Agency* (*PBPA)* kwa mfumo wa *Bulk Procurement System*, Wakala wa Kukusanya Mitaji kutoka Makampuni ya Ndani na Nje, kwa mshangao mkubwa makampuni hayo yote, aliyenijibu Naibu Waziri vizuri wenyewe kaja kakiri, nimfanye nini. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa moja katika kero mafuta ndio *engine* ya nchi. Wenzetu wale ambao hawako karibu wanalipishwa Dola 3 mpaka Dola 4 na *wharfage*, sisi tunalipishwa Dola 10, sio kitu kizuri. Mhe. Naibu Spika, mafuta Dar es Salaam sasa hivi au Tanzania Bara ni rahisi kuliko

Zanzibar. Kwa hivyo serikali hapa kikao iangalie vizuri nini cha kufanya au nini cha kufikiria.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije kidogo kwenye wizara ya mama yangu Mhe. Maudline Castico Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza yeye na watendaji wake. Nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba yule anayekukosoa ujuwe anakupenda, wala usitake kumuhukumu kuwa ana kitu ndani ya roho yako, ujue yule anayekukosoa anakupenda na yule anayekuja kusema pembeni muongo yule, lakini yule anayekuambia uso kwa uso ujue anakutakia mema. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, elimu imekuwa ndogo inayotoka au wanayoipata Wizara ya Afya nafikiri au na Polisi katika kuchunguza kesi za kubaka, elimu imekuwa ndogo. Mhe. Waziri liandike hilo mtafute njia ya kutoa elimu, elimu imekuwa ndogo katika ubakaji. Nilichokiona wakati kamati hii ilipofanya kazi, kitu cha mwanzo mtoto akibakwa utafikiri gari inapelekwa *garage*, inafunguliwa *bonnet* tu kwanza, haijaguswa pahali popote gari inafunguliwa *bonnet*. Kuangalia yale mazingira ya mtoto kabakwa kama kabakwa tumbo, kama kichwa kaangushwa chini, uangalie ule upelelezi uko vipi, pengine tunaweza tukaja kumtia mtu kwenye hatia ambayo haielekei na hizo kesi zimeshatokea, daktari mtu atamvua nguo tu kwanza aangalie, Polisi halikadhalika vile vile. Kwa hivyo elimu itolewe tusije tukahukumu tu, hivi vyeo ni dhamana hata kwa Mwenyezi Mungu tutakwenda kuulizwa tumesimamia vipi dhamana zetu. Tusifukuzie tu kuvua nguo na tuangalie yale mazingira. Je, kaangushwa chini au utakuta michubuko, kakamatwa tumbo utakuta pana japo alama za vidole, tusivukuzie tu kama gari kufungua *bonnet* moja kwa moja bila ya kwenda *garage*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nije katika maadili ya malezi. Malezi yanazidi kupungua tofauti na tulivyokuwa tukilelewa nyumbani. Mtoto wa

jirani ukimpiga leo umekuwa mtihani, ambapo mtoto wa Mhe. Abdalla Ali Kombo mimi nilikuwa wakati wowote ule nilikuwa naweza kumpiga na wangu akampiga na kumfundisha malezi. Lakini elimu inataka kutolewa.

Mhe. Naibu Spika, pia madisko yamekuwa mengi mno uangaliwe utaratibu wa kutolewa vibali. Hivi sasa Paje watu hawalali, Bwejuu, Jambiani ngoma zilikuwa zikipigwa *weekend*, lakini sasa hivi mfululizo, maadili *total* yataporomoka tu. Kwa hivyo, tuangalie utaratibu wa kutoa vibali, wananchi wana haki yao katika nchi yao, ngoma zimekuwa nyingi. Ndio unakuta sasa hivi wala unga wamekuwa wengi, ubakaji unazidi. Leo *disco* linakwenda kupigwa katikati ya wananchi unategemea nini, ukipanda shokishoki huwezi kuvuna pera utavuna shokishoki na ukipanda doriani huwezi kuvuna chooko ulichokipanda ndio utakivuna.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tutafute utaratibu. Mhe. Naibu Spika, hapa aliyekuwa Waziri Mhe. Said Ali Mbarouk alitoka saa nane za usiku akawaita watendaji wake ofisini kwake Kikwajuni hawakujua wanapelekwa wapi, walivaa bukta na yeye mwenyewe akavaa bukta yake wakaingia Paje wakaona hali ilivyo, akazuwia ngoma zile. Lakini nimshukuru sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini mpya, kazi anayoifanya ni kubwa ya kupigiwa mfano. Kwa hivyo, bado kule changamoto zimekuwa kubwa mno. Bado Mhe. Waziri, Bwejuu, Jambiani na Paje ngoma zimekuwa nyingi sana tena sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nije nyumba ya kulelea watoto Mazizini. Hivi juzi nilizungumza kuna kadhia imetokea na niliomba Serikali Naibu Spika, na wewe mwenyewe ulikuwa ni shahidi lakini sijapata majibu na nafikiri ndio itakuwa imeshatoka tena. Mtoto miezi sita au minane unampeleka skuli unategemea nini, anafahamu nini, anapata nini. Nyumba ya kulelea watoto kazi yake kulea watoto, ndio jukumu lake na inalipwa na

wafanyakazi wanalipwa. Kitu cha kinyonge kabisa kila Mhe. Naibu Spika, na kinatia huruma. Hebu angalieni utaratibu…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, lakini utaratibu gani.

La mwisho watoto wale waliopo pale wanaolelewa siku ya siku kuu wamekwenda kuvishwa suruali. Nililipigia kelele, sasa unategemea nini ndio ile iliyosemwa ukipanda shoki shoki huwezi kuvuna doriani. Sasa maadili kama Wizara yenyewe inaharibu unategemea nini. Wizara yenyewe inaharibu maadili unategemea nini. Utamaduni wetu Mhe. Waziri sisi si kuvaa suruali kabisa, sio utamaduni wetu kuvaa suluali na walipinga kwanza kamati yenyewe ikajiridhisha, walipinga walikuwa wakali kwanza, nikawaambia tulieni baadae wenyewe tu wakajisuta. Sasa Wizara yenyewe inafanya makosa unategemea nini, maadili yetu yanatukataza.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baada ya hapo ni Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari, Utalii. Kabla ya kuchangia kwanza niwapongeze sana sana Wajumbe wa Kamati akiwemo Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mwenyekiti Mahiri maarufu mjomba kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ili

kuhakikisha kwamba kila changamoto na kila lililo baya wanaligundua na kutuletea, ili kulipatia maoni na kutoa ushauri wetu.

Mhe. Naibu Spika, badala ya shukurani hizo niende moja kwa moja ukurasa wa 9. Ukurasa huu unasema mambo ambayo Kamati hayakuridhika nayo changamoto za Shirika la Magazeti ya Serikali. Mhe. Naibu Spika, hapa ni kweli hata mimi nimeliona kwenye tatizo la usafiri walisema kwamba kuna gari nne na vespa ya tangu mwaka 1992. Mimi sioni vibaya kutaja umri wangu. Hii vespa nadhani mimi na yeye hatukupitana kwa miaka mingi sana. Vespa mpaka sasa ina miaka ishirini, nilishangaa nilimwambia Mhe. Bihindi hapa kwamba hatukupitana kwa umri na vespa hii, cha kushangaza vespa hii hata kama iwe ni ya nani kati ya sisi tuliomo ndani Barazani humu basi itakuwa si vespa tena itakuwa ni kachara hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwamba hawa wafikiriwe na changamoto hii ya vespa, vespa ina gharama kiasi gani hata kwamba vespa tokea mwaka 1992 mpaka hii leo. Katika changamoto moja inayowakabili hawa ni usafiri, kwa hivyo naiomba sana Wizara husika kuhakikisha kwamba tatizo hili la vespa moja au kupata usafiri wa uhakika waweze kulifanyia kazi. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tulipitisha bajeti hapa na akaunga mkono hakuna aliyezuia bajeti na haitotokezea hivyo. Kwa hivyo naishauri sana Wizara na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba sekta hii inapatiwa usafiri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, chengine cha kusikitisha ni suala la madeni walisema kwamba hadi sasa Shirika linadai shilingi milioni 323.2. Gazeti mpaka leo wanadai pesa hiyo ambayo Serikali inadaiwa pesa hiyo hapo shilingi milioni 184 na taasisi

binafsi zinadaiwa shilingi milioni 138. Mhe. Naibu Spika, hapa tutegemee kukua au tutegemee kuporomoka kama mpaka Gazeti wanadai pesa hiyo mpaka leo hii inafikia kwamba pesa hiyo inakuwa kidogo ni vikwazo kupata pesa hiyo. Mhe. Spika, kwa hivyo nawaomba sana kwamba wote wale ambao wana madeni na wanajijua basi wafanye haraka ili kuwapatia pesa hizi angalau kutafuta hiyo vespa, kwa sababu vespa tokea mwaka 1992 nina imani wangepata pesa hizi wangetafuta wangefanya mipango pango wakaziba ziba wakatafuta vespa angalau ya kuweza kuwasukuma sukuma wakiwa na safari zao.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye vyombo vya habari ukurasa wa 14. Kwenye vyombo vya habari hapa wamesema kwamba vyombo vya habari vya binafsi vipo juu zaidi kulikoni kile cha Serikali na hapa Mhe. Naibu Spika, nimejiuliza kwamba vyombo vya habari binafsi vinajitia Serikali, tatizo nini kwamba hawa binafsi wanalipia Serikali, lakini Serikali waliandika kwamba huenda wasikilizaji wasisikilize. Tatizo lipo wapi kwamba vipindi sio vizuri au tatizo kuna nini. Kwa sababu hivi vyombo vya habari vya *private* wanailipia Serikali. Sasa cha kushangaza kwamba hichi cha Serikali ndio mama ndio baba ndio cha kuvua kuwashinda hao ambao kwamba wanategemea sehemu nyengine, lakini wao *private sector* wanalipia Serikali. Sasa lakini tatizo hili Mhe. Naibu Spika, naliomba pia lakini Mhe. Waziri kwa alivyo makini na nina imani nalo hili litapata ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende moja kwamoja ukurasa wa 19 Mhe. Jaku alizungumza kuhusu ukosefu wa mafuta na wengi wamesema suala la ukosefu wa mafuta mara kwa mara. Hii Zanzibar yetu ni visiwa vya kitalii, bila ya mafuta watalii wakifika hapo *Airport* watakwenda kuchukuliwa na nini. Maana yale mambo ya ubwanyenye yameondoka zamani kubebwa kwa

machela sijui kwa nini ile yamekwisha zamani yale. Sasa Mhe. Naibu Spika, suala hili la mafuta ni suala la kupewa kipaumbele, kuna tatizo gani haya mafuta haya ikabidi kwamba yanaadimika mara kwa mara. Mhe. Naibu Spika, hata leo hii mafuta ni tabu, tatizo kipo wapi. Kwa hivyo naomba sana Serikali kujidhatiti kwenye hili kuhakikisha kwamba mafuta yanapatikana mara kwa mara, kwa sababu tuna tegemea sana utalii. Sasa watalii wakija hapa wakiona wanasumbuka kwa mafuta itakuwa tayari kwa sababu wanakwenda kusambaza kule kwao kwamba Zanzibar usiende ukienda itakuwa usumbufu hivi na hivi na ni kweli kwa sababu wakija wanashudia hilo.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naiomba sana Serikali kwa sababu sisi Zanzibar tunategemea sana utalii basi kuhakikisha suala hili la mafuta ni kuhakikisha kama mtu ilivyokuwa ndani mwake asikose kijio ndani mwake, basi tuhakikishe kwamba mafuta kwa sababu ndio safari na ndio kila kitu. Naiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba mafuta yanapatikana muda wowote.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Wizara ya Uwezeshaji ya mama yangu hapo Mhe. Castico. Kwenye suala la urejeshaji wa mikopo, juzi nilitoa mfano hapa nikakwambia kwamba kuna mwalimu alisomesha darasani akaandika hisabati akawaandikia wanafunzi baba yako amekopa shilingi elfu mbili, elfu moja kakopa benki, elfu moja kakopa kwa jirani. Je, baba anatakiwa alipwe shilingi ngapi. Mwanafunzi akajibu baba yangu halipi, mwalimu akawa mkali akamwambia nakwambia hivyo kusudi kwa sababu baba yangu akikopeshwa halipi.

Mhe. Naibu Spika, sasa cha kushangaza hawa watu hawalipi, kwa nini hawafanyi utafiti hawa wanaoturudisha nyuma, maana hizi pesa sio pesa za sadaka hizi ni pesa za Serikali, Serikali imetoa

kwa nia njema kuwakopesha wananchi wake. Kwa hivyo waliokuwa hawakopesheki wasikopeshwe, lakini leo cha kushangaza kuna yale Mabaraza yetu ya Vijana yaliyoundwa kisheria pesa hizi nina imani hawanufaiki nazo kabisa, katika jimbo langu Mabaraza hayo yapo na sifikirii na nina uhakika kama walinufaika nazo hizi. Lakini nina uhakika kwamba kuna wananchi ambao wamekwenda kuchukua mkopo huu lengo la kuhakikisha kwamba wanadhorotesha maendeleo ya wananchi wengine hadi leo hii wana miaka mitano sita saba hawajalipa mkopo huu, kuna tatizo gani wahakikishe wale waliokuwa hawakopesheki wasiwakopeshe na suala hili linakuwa litaka kumjua kwamba mkopeshaji wako unayetaka kumkopesha mfuatilie mpaka kule anakokaa, ikiwa Sheha kamtilia saini basi Sheha aanze kuwajibika yeye kwa sababu yeye Sheha anawajua.

Mhe. Naibu Spika, leo mtu anakwenda kuchukua pesa milioni mbili, tatu mpaka tano Wizara ya Uwezeshaji wanatoa pesa hizo mtu halipi, halafu inakuja hapa inafika miaka mitano pesa hizo hazilipwi, tunakwenda wapi hatufiki mbele. Kwa hivyo naiomba sana wizara ichukue hatua kali za kuhakikisha kwamba wale wote wanaodaiwa au wadaiwa sugu miaka mitano na kuendea mbele kwa sababu naona mikopo hii ya uwezeshaji haina masharti makubwa hata hivyo, unachukua shilingi milioni moja, mwaka mzima inategemea na biashara yako.

Mhe. Naibu Spika, sasa naiomba sana Wizara kuwachukulia hatua, sio kwamba maneno tu hawalipi hawalipi bila ya kumchukulia hatua hawezi kulipa. Lakini mimi nina uhakika kwamba alipochukua ule mkopo kuna mkataba ndani yake walijazwa iwapo kashindwa kulipa mkopo ule, sasa sisi kila siku tunapitisha bajeti hapa milioni mia sita bajeti ya mara ile na mara hii mia sita wanapewa watu wanazilia changu hawarejeshi na

kuna watu wanazitaka hizi pesa hususan vijana, wanazitaka hizi pesa kuzifanyia kazi ili kuzizungushia wao hawazipati.

Kwa hivyo naiomba sana sana Wizara kuhakikisha hili limefanyiwa kazi na hizi pesa zimepatikana itakapokuja bajeti hapa tujue kwamba wangapi wamekopa na wangapi wamelipa na wadaiwa sugu tuwaone, kama mimi jimboni kwangu nikitaka kuwajua Wizarani Chake Chake, kwa sababu hawa ni watu wanaorudisha maendeleo. Leo pesa hii ya Serikali Rais ameweka kwa nia njema, leo mtu anachukua mkopo harejeshi inakuwa ni hadithi ya alinacha halipi, afuatiliwe kwa sababu hii pesa si yake.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye sekta ya vijana. Kwenye sekta ya vijana nilimwambia Mhe. Bihindi Hamad hapa kwamba hii sekta ya vijana nitaigusia kidogo ni huko huko kwenye masuala hayo hayo ya mikopo. Vijana ndio taifa na ndio nguvu ya taifa. Mhe. Naibu Spika, vijana mimi nilimgusa Mhe. Bihindi nikamwambia hata ile mikarafuu imani yangu kwamba wangeambiwa wale vijana wakachuma kwa kibarua tu basi hiyo pesa ya mikarafuu ingepatikana, kwa sababu yale Mabaraza ya Vijana yapo kisheria na yapo kwenye taratibu nzuri. Kwa hivyo naomba sana vijana wajaliwe, wathaminiwe wahakikishwe kwamba wanawekwa vizuri wanatunzwa ili kuondokana na mambo maovu na kuacha mambo ambayo kwamba hayana maana.

Kwa hivyo inshaalla Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Suleimana Makame Ali mchangiaji anayefuata ni Mhe. Dkt. Makame Ussi, baada ya Dkt. Makame atachangia Mhe. Bipanya Ali Abdalla.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante saana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kwenye mada hii tunayoijadili hivi sasa. Kwanza kabisa napenda sana kuipongeza kamati hii Kamati ya Wanawake na mambo mengine yaliyomo kwenye kamati kwa ufasaha wake wa kuripoti na kueleza mambo yote ambayo kwa kweli yatasaidia sana kurekebisha yasilete kasoro ziliopo. Nampongeza tena Mwenyekiti wa kamati hii ndugu Ali Suleiman Ali Shihata na ni Shihata kweli, maana kakagua kwenye sehemu inayohusika, akataka na huku alikokagua hawa wahusika akenda akakagua huko akapata mengi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiingia kwenye kitabu Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya pili hapa kuna malengo yametajwa hapa. Kwa kweli nimevutiwa na malengo haya wanasema malengo makuu ya Wizara hii ni kuwa na maendeleo ya habari, utalii na utamaduni na michezo nchini kwa kuhakikisha mambo yafuatayo:-

1. Wananchi wanapata taarifa za kutosha na za usahihi kwa wakati muafaka.
2. Wananchi wanashiriki katika kutangaza utamaduni wa Zanzibar.
3. Wananchi wanashiriki katika kazi za sanaa.
4. Kuhakikisha kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi bora katika ukanda wa bahari ya Hindi.
5. Kuhakikisha kwamba wananchi wanashiriki katika michezo kwa kushinda na kujenga afya.

Mhe. Naibu Spika, haya kwa kweli ni malengo mazuri lakini sasa mimi nilitaka kuongeza tu hapa ingekuwa ni vizuri kila lengo lililosemwa hapa kwa mfano wananchi wanapata taarifa basi wangetueleza kimefanyika nini kuhakikisha kwamba hizi taarifa kweli wanazipata wananchi, hivyo hivyo wananchi wanashiriki wangetueleza pia utaratibu wa wananchi kushiriki kwa sababu na sisi tunataka tuhamasishe wenzetu kule majimboni kwetu washiriki na wao waweze kufaidika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapo sasa nakwenda moja kwa moja kwenye Shirika la Magazeti ya Serikali. Kwa kweli Shirika hili ni muhimu kwani linaweza kuelimisha kwa njia ya magazeti, linaweza kusomesha kwa njia ya magazeti na mambo mengi ya kimaendeleo yanaweza kufanywa. Lakini inasemakana kwamba lengo la kuchapisha kopi elfu tatu halijafikiwa kwa sababu ya vifaa na mambo mengine mengine.

Mimi ningeshauri sana kwa umuhimu wa Gazeti hili basi ni vyema zikachapishwa kopi za kutosha na sisi tukaweza kuuza ndani ya nchi hapa na nyengine tukaziuza nje ili tuweze kupata fadia ya kuendesha hili shirika, kwani shirika maana yake ni chombo kinachojitegemea. Likichapisha magazeti megi maana yake kitaweza kupata mapato makubwa na Shirika hili litakua.

Mhe. Naibu Spika, hapa pia wameainisha mambo ambayo kamati haikuridhika na changamoto walizoziona. Kwanza walikuta kuna tatizo la usafiri. Shirika limerithi gari nne, gari nne hizo tangu mwaka 1992. Sasa gari hizi taaban ni kwamba zimeshakuwa chakavu sana haziwezi kufanya kazi na habari za magazeti zinataka kutafutwa, zitafutwe mashamba na kila pahala ili ziweze kuandikwa, wakikosa usafiri hawawezi kufanya kazi. Nashauri watafutiwe usafiri tena wa uhakika ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi.

Kuna tatizo la madeni wanadai sana. Sasa Shirika kama halilipwi litakwenda vipi. Kwa hivyo pia nashauri Wizara husika isimamie haya madeni yalipwe ili hili shirika liweze kujiendesha vizuri zaidi. Kuna mambo ya mitaji wametaja hapa, kuna kutokuwa na uhakika za nakala za uchapaji, yote haya kwa kweli yanahitaji marekebisho tunashauri Wizara husika zikae pamoja zirekebishe matatizo haya.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja sasa niende kwenye umuhimu wa kupata kutangaza habari. Kwa kweli hapa imeainishwa kwamba sekta ya habari ni moja kati ya sekta muhimu sana katika jamii yoyote duniani, kwani hutumika kuhabarisha umma kuhusu mambo mbali mbali yanaoendelea yakiwemo kisiasa, kiafya, kielimu na hata kiuchumi. Aidha sekta hii hutumika kuibua, kueleza na kufafanua na hata kuburudisha katika jamii. Hili ndio lengo kubwa la habari. Sasa habari kwa kweli hiyo moja kwa moja wametaja kurekebisha matatizo mbali mbali kupendekeza mambo mema mazuri ya kuendesha nchi. Aidha habari hupotosha na hili ndio jambo la muhimu sana habari zikiandikwa vibaya zinapotosha zinaweza zikazaa cheche, cheche za matatizo ukaja ukazuka moto mkali sana hapa watu wasielewane hapa kabisa kabisa. Kwa hivyo habari lazima zisipotoshwe ziende vile zilivyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa kutokana haya mimi nitapendekeza tu baadhi ya mambo ambayo kwa kweli waandishi wanaweza wakayapata wao wanayajua zaidi lakini yale ambayo wanayaona mwenyewe. Kwanza waangalie sana thamani ya habari hiyo na thamani yenyewe basi ihusiane itakuwa na thamani, habari itakuwa na thamani kama itahusiana na hali halisi iliyopo na hali halisi hiyo iwe ya kimaendeleo, isiwe hali halisi ya kupigana watu kwa kunyang'anyana, iwe ni hali halisi ya maendeleo wanafundishwa watu maendeleo hayo, Iwe ina umuhimu wake kwamba inapendeza kwa wasikilizaji na inakidhi haja ya maendeleo ya nchi.(*Makofi*).

Halafu jengine pia habari ili habari ziwe nzuri zaidi lazima zihamasishe ziwe na hamasa ziawafanye watu wawe na hamasa kufanya mambo kufanya kwa ushindani na pia zishirikishe, ziwafanye watu washiriki katika mambo ya maendeleo. Ubaniaji wa habari mtu anaweza kuwa anajua habari au anaifahamu lakini kaibania, hii itakuwa hafati zile *ethics* za uandishi wa habari, lazima habari anazozipata azitoe kwa uwazi na zifahamike vizuri.

Halafu mwenye habari, pia anayetoa habari ahakikishe kwamba hiyo habari ni yake kwa hivyo kama akiipotosha yeye ndiye anayefuatwa kwa makosa aliyoyafanya. Kwa hivyo ni vizuri awe na uhakika kwamba anatoa habari yenye maana, habari inayoongoza vizuri na sio habari ya kupotosha ikiwa na kupotosha itabidi afuatiliwe na asema kaipata wapi habari, ikiwa ya kuzusha au kupata chochote.

Habari iangalie pia nguvu za siasa, hapa sisi Chama chetu ni Chama cha CCM na tunaendesha mambo yetu kufuata Ilani za CCM. Kwa hivyo wanapoandika waandike kwa muijibu wa Ilani za Chama cha CCM, wakiandika vyenginevyo akifuata mambo pengine ya upinzani ambayo ya kupotosha watakuwa hawakitendei haki Chama Tawala.(*Makofi*).

Jengeni ni elimu, kwa kweli sisi tumezoea kuwaona waandishi wa habari kwamba huyo huyo mwandishi wa habari wa uchumi, huyo huyo ataandika habari za afya, huyo huyo akaandike habari nyengine. Ni vizuri sana kuwa na waandishi wa habari ambao wame-*specialize* kwenye mambo fulani fulani kama wa uchumi basi afanye habari za uchumi, kama ni afya basi awe ni mwandishi wa habari za afya na kadhalika na kadhalika. Tukifikia huko nadhani tutaweza kuandika habari nzuri na za zenye manufaa zaidi kwa sekta husika.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Wanawake na Watoto. Kwa kweli

katika Wizara hii niwapongeze wanajitahidi sana, mikopo nakumbuka tangu yupo Mhe. Haroun Ali Suleiman, ilitoka mikopo mingi sana nakumbuka Kaskazini tulipata mikopo, sikumbuki ni kiasi gani lakini tulipata fedha nyingi na vikundi vingi vilifaidika. Lakini naona utaratibu ule sasa hivi kama umepungua kidogo, sijui labda tukielimishwa zaidi tutajua. Tuna wananchi wengi sana wamejiunga na vikundi vya ushirika hawapati nyenzo za uwezeshaji, hawapati mikopo.

Mimi nakumbuka kuna vikundi vyangu si chini ya 12 ninavyo vimeomba mikopo, vimeomba msaada tangu nafikiri miaka mitatu au miwili nyuma hawajafanikiwa, tunaomba sana watu hawa waliojiunga kiushirika wasaidiwe ili waweze kuondoa umaskini. Kwa sababu tumepiga kampeni za kutosha, tumeeleza vya kutosha, wananchi wamefahamu wamejiunga kiushirika vikundi vimekuwa vingi, si ajabu kwangu mimi nadhani vipo 200, vile vya *registered* na vile ambavyo *unregistered,* karibu 200, vyote hivi vinataka misaada. Sasa uwezeshaji kami misaada yenyewe inasuasua namna hii nadhani tutawavunja moyo sana wananchi wetu.

Halafu kuna wananchi sasa wanyonge wa Mungu, mmoja mmoja anauza maandazi, anauza badia na kadhalika hawa wanakosa usaidizi mara nyingi sana, wanalalamika na hawa ni wengi. Naomba serikali iwaangalie na hawa maskini pengine hawawezi kujiunga na ushirika hawataki au wafanye nini, lakini na wao wanaweza wakafanya kitu cha kujiendesha wakapata kitu cha kuendesha maisha yao. Naomba sana na hawa tuwafikirie, tuwasaidie misaada japo shs.20,000/= hata shs.10,000/-. Kuna wengine Wallahi ukimsaidia elfu kumi anakwenda kununua unga wa ngano anakuja kutengeneza chapati, tumeshawaona hao wapo. Kwa hivyo tunaomba sana na hawa na wao tuwaangalie wapate misaada ili waweze kumudu maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, naingia tena sasa kwenye Kamisheni ya Kazi, mambo mengi yameelezwa hapa kwamba Kamisheni ya Kazi tangu kuundwa kwake hapa ikaelezwa kwa mujibu wa taarifa za Kamisheni hadi mwisho wa mwaka wa Disemba 2017, jumla ya taasisi 2060 za Unguja na Pemba zilikaguliwa ili kufatilia ulipaji wa kima kipya cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi. Hizi sehemu ambazo zilifatiliwa zimetajwa 2060 sawa sawa, lakini katika ngapi au tunafanya tu, hapana tunakwenda tu, hatujui tuna lengo gani. Ingekuwa ni vizuri sana tunataja ni sekta zinazotaka kukaguliwa ni 1000 hizo ndizo zetu sisi tunazotaka kuzikagua. Kwa hivyo tumepata 2060. Hapa kuna 260 zilizokaguliwa sasa ngapi nazijakaguliwa na kwa nini, hatuwezi kupata sababu hapa tukaweza kuhoji tukaweza kutoa mapendekezo yetu ya kurekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ajira nje, ajira za nje zimetajwa hapa kuna vijana hawapungui 620 wamepatiwa kazi nchi za Arabuni huko, kama Maldives, Bakhrain, Oman, Qatar, Saudi Arabia na kwengineko. Sasa hapa zimetajwa nchi za Kiarabu lakini tunao wenzetu wanatafuta kazi Ulaya wapo Uingereza, wengine wapo Marekani, hazikutajwa hizi, hawa hawawezi kuingia kuingia kwenye Wizara yetu hii na wao tukawajua, tukawabaini watu hawa wanaofanya kazi hii, tukawaorodhesha kama wenzao hawa tuliowaorodhesha hapa, Uingereza na sehemu nyengine. Kwa hivyo tunaomba na sehemu nyengine kama tunazishughulikia au kama hatuzishulikii basi tuziingize kwenye kuzishughulikia na humu tutafute ajira watu wetu waende ili….

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Dakika mbili, ahsante sana nitajitahidi nizitumie vizuri sana ili dakika mbili zisizidi.

Sasa nimalizie tu kwa sababu ndiyo nimeshaambiwa dakika mbili sasa namalizia tu kwamba sekta ya uwezeshaji nimeshasema

kwamba kwa kweli tunahitaji tuweke mkazo zaidi tuwezeshe watu wetu ili waweze kufanya shughuli zao za kiushirika na za kibinafsi ili umaskini uweze kuondoka. Kwa hivyo tunaiyomba sana Wizara ijitahidi sana mje tushirikiane, kwangu mimi nitakuonyesheni orodha ya vikundi hivyo 200 ambapo karibu 50 vimeshasajiliwa na vyengine tunaendelea kuvisaidia kusajiliwa. Sasa mje mvione hivi vikundi tuvisaidie kwa pamoja, pamoja na watu binafsi ili tuweze kupiga vita umaskini.

Baada ya kumaliza hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Panya Ali Abdalla na ajitayarishe Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu (SW) ambaye ametujaalia jioni hii kukutana mahala hapa tukiendelea na majukumu yetu. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe na mimi kuweza kunipa nafasi niweze kusema machache katika Wizara zetu hizi.

Kwanza kabisa nianze kwa kupongeza Mawaziri wa Wizara zetu zote mbili hizi kwa kazi kubwa na za umakini kabisa ambazo wanaweza kuzifanya ili kusaidia jamii yetu. Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata au Mjomba). Nimpongeze sana kwa usomaji wake ambao umekuwa mzuri na ufafanuzi mzuri kwa kila alilotuletea. Nimpongeze yeye pamoja na wenzake wote ambao waliyokuwemo katika kamati hii, kwa kazi kubwa na mashirikiano makubwa waliyompatia Mwenyekiti wakaweza kufanya kazi hii. Bila ya kuwasahau watendaji wote wa wizara

hizi mbili kwa kazi kubwa za kushirikiana na Mawaziri wao ili ufanisi ukaweza kupatikana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika sekta ya habari ambapo hapa ukurasa wa 5 imeeleza ni moja kati ya sekta muhimu sana katika jamii yoyote duniani, kwani hutumika kwa kuhabarisha umma kuhusu mambo mbali mbali yanayoendelea yakiwemo ya kisiasa, kiafya na kielimu na hata kiuchumi. Aidha sekta hii hutumika kuibua, kueleza, kufafanua na hata kuburudisha katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nishukuru sana na niseme nakubaliana kabisa na usemi huu kwamba sekta ya habari ni sekta muhimu sana. Kwa umuhimu huo wa habari pia hapa imeelezwa kwamba taifa lenye kupata habari sahihi na kwa wakati sahihi linakuwa ni vizuri katika nyanja mbali mbali kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii. Naunga na maneo hayao kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika, habari ni jambo zuri na muhimu ambalo tunahitajiwa kulipata hasa ile ikiwa kwa wakati sahihi. Mimi nina suali hapa niulize kwa nini kipindi kile cha Mawio. Mawio tunayazungumza leo lakini yanatoka keshokutwa. Sasa hapa hatupati zile habari kwa wakati na usahihi, maana raha ya jambo likisimwa leo basi kama kesho unalipata au leo kama kuna kipindi basi kinaweza kikakatishwa tupata habari moto moto, jambo liko moto moto tukaweza kulipata, hiyo ndiyo habari yenye usahihi.(*Makofi*).

Mimi bado naendelea kuiomba serikali zile habari za haraka na usahihi ni muhimu sana kuzipata hasa ukiangalia ndani ya kipindi hichi ambapo kuna ushindani sana wa kibiashara. Sasa hivi tunamashirika mbali mbali na mimi bila ya kigugumizi niseme Shirika hili la Habari la *ZBC* ndilo shirika muhimu ambalo Wazanzibari wote tunalitegemea kwa asilimia mia moja. Ndipo tunakotegemea sisi kupata habari zenye usahihi, zenye uhakika na

zenye kueleweka. Naomba bado jitihada hii serikali ichukue na iendeleze ili *ZBC* iweze kung'ara katika kutuhabarisha habari zilizo njema na sahihi kuliko zile nyengine zinakuwa za upotoshaji.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini pia hapa Kamati katika mizunguuko yake imeeleza kwamba bado kuna changamoto ambayo inawakumba sana wafanyakazi katika utendaji wa kazi zao. Tuiombe sana Wizara na tunaendelea kuomba kila wakati kwamba wenzetu wanaofanya kazi katika Shirika hili kwanza niseme nawasifu na nawapongeza ni wazalendo, ni vijana wanajituma ni wazalendo, hawachoki, kama Mhe. Said Omar Said alisema hapa kama tutakaa mpaka usiku basi na wao watakuwepo mpaka usiku, kama tutafika asubuhi na wao watakuwepo mpaka asubuhi. Kwa hivyo tuone juhudi kubwa wanayoifanya na kazi yao ile ni ngumu, lazima tukubaliane na hayo. Hivyo lazima stahiki zao na wao wazipate kwa wakati muwafaka.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika Shirika la Utangazaji lenyewe *ZBC* ambalo linaelezewa hapa majukumu makuu ya Shirika hili ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Mimi niseme bado tunataka *ZBC* ijikite katika kuweka wataalamu wazuri zaidi katika mambo ya utangazaji, lazima *tune* yetu ile lafidhi ya lugha yetu ya Kiswahili sahihi iweze kupatikana katika chombo hichi. Kwa sababu sisi hapa katika mwaka 1930 lugha yetu ya Kiswahili cha Unguja Mjini ndiyo iliyoteuliwa kwa Afrika Mashariki. Kwa hivyo ni lazima hichi kipaji tukitumie kwa sababu sisi ndio, sijui inakuwaje mpaka ikawa tunahodhiwa, lakini sisi ndio wenye Kiswahili fasaha, sanifu chenye lahaja tofauti, Kiswahili ambacho mtu akikusikiliza anataka uendelee kuzungumza tu. Hivyo heshima hii bado tuiendeleze katika kuona watangazaji tunaowaweka, hatukatazwi mtu kuajiriwa, tukiona lafudhi yake haipo vizuri basi tunaweza tukampangia sehemu nyengine lakini katika hiyo hiyo *ZBC* lakini akapangiwa jambo jengine, lakini wale watangazaji tulitaka waweze kuwa na lafidhi nzuri ya

utangazaji jambo ambao lingeweza kukikuza zaidi na kukiuza sana Kiswahili chetu cha Zanzibar Mjini.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, naomba sana na heshima hiyo pia imeletea kuletewa sisi Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ipo hapa kwetu Zanzibar. Hiyo ni heshima kubwa na lazima tuweze kuithamini na lazima tuweze kuilea na kupembejea kwa heshima yote, hali ambayo tunajua ni tija na inaweza kutuletea ajira kubwa zaidi ya tulizonazo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu huu niende katika ukurasa wa saba ambao kuna mafanikio hapa ya *ZBC* lakini pia kuna changamoto zake. Imeelezwa katika changamoto kuna usafi, Kamati haikuridhika kabisa na hali ya usafi na utunzaji wa vifaa. Hili tunaomba sana kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake kwa dhati na moyo ambao anaonyesha kuitumikia nchi yake hii kwa dhati kabisa, kwa kuona alipoona *ZBC* ipo katika hali mbaya Mheshimiwa amejitoa muhanga akajitolea kupeleka kila aina ya vitu pale. Kwa hivyo tunapokuwa hatuvitunzi na kuvithamini tunaweza tukarudisha nyuma juhudi hizi. Naiomba sana serikali iweze kuchukua juhudi na wale ambao wamepangiwa kusimamia majukumu haya naomba sana wachukue majukumu yao haya ili jambo hili liweze kuwa na ufanisi mzuri tuweze kumuunga mkono Mhe. Rais wetu kwa juhudi zake ambazo anazichukua.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pia katika Wizara hii niseme kunakuwa kuna jambo na tunalisemea sana kila mara, kuna wafanyakazi ambao wanajitolea muda mrefu sana. Hili tumekuwa tukilisema tangu Baraza lile lililopita. Mheshimiwa kujitolea basi kuwa na kiwango chake, lakini la kusikitisha wale wanaojitolea zinapokuja ajira wanakuwa wao hawafai, wanaajiriwa wengine wapya. Mimi niombe ndani ya kujitolea mngekuwa mnachuja kabisa kuona mfanyakazi huyu itakapotokea ajira anatufaa na huyu hatufai, ili

tuweze kumtoa matumaini mapema akatafute shughuli nyengine afanye. Mtu miaka kumi na ngapi yupo anajitolea tu, jamani tuone huruma, kuzitumia nguvu zake zote hizi na baadae mtu huyu ikashindikana kuajiriwa katika kazi anaaminiwa na anafanya, lakini katika ajira haaminiwi. Hivi ni vitu ambavyo visingewezekana. Tunayeona anaweza basi tumpe uhakika huyu anaweza na ikitokea ajira tuweze kumuajiri kwa sababu tumeshazitumia nguvu zake muda mwingi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika hii hii *ZBC* kuomba sana lazima tujikite katika kuwapatia mafunzo wafanyakazi wetu. Kama tunavyoelewa sasa sio kama zamani, sasa mambo yanakuwa siku hadi siku, vyombo hivi ni vingi. Kwa hivyo na sisi lazima tuendane na ushindani ya kibiashara tuweze kuwapatia elimu wafanyakazi wetu na wao waweze kwenda na wakati ili pahali popote wanapotakiwa na wao waweze ku-*fit* kama walivyo wenzao.

Mhe. Naibu Spika, pia niseme sana kuhusu habari, habari jamani vyombo vya usafiri ni muhimu, sana katika habari kama tuna mapungufu basi tuweze kuzingatia kuwatafutia wenzetu habari bila ya usafiri hapo hakuna habari haipatikani, kwa sababu utapigiwa simu mahali fulani kuna tokeo fulani, wewe huna usafiri wa kwendea habari hiyo itakuwa imekupita. Naomba sana vyombo hivi vya usafiri viweza kupatikana ili ile habari iweze kupatikana ili ile habari tuweze kuipata kama ambavyo tunaitarajia.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 21 kwenye sekta ya utamaduni.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Haya, Mhe. Naibu Spika, utamaduni wa nchi yetu ni jambo muhimu sana, utamaduni wetu unaanzia

katika mavazi, mavazi ndiyo yanayotujulisha sisi kama Wazanzibari, mtu akikuona tu anajua huyu Mzanzibari. Kwa hivyo kuna mapungufu katika Sheria ile ya Mavazi na tuliyomba muda mwingi iletwe hapa Barazani tuifanyie marekebisho ili tuendani na utamaduni ulio sahihi wa mavazi yetu. Hivyo bado mimi naomba na nasisitiza Sheria ile iletwe ili tuweze kuifanyia hapa marekebisho na lazima tuendane na utamaduni wetu wa mavazi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pia kumezungumziwa filamu ambazo zisizo na maadili, ni kweli Baraza hili la Sanaa lina kazi sana ya kuchekecha filamu, lazima filamu zetu hizi zichekechwe ili ziweze kuonekana sahihi katika vyombo vyetu uweze kuangalia wakati wowote bila ya woga. Lakini leo inaoneshwa sanaa mbele ya mtoto wako unashindwa kukaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niombe sana kwamba hizi lazima zirekebishwe halafu ndio ziletwe.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wizara ya Wanawake na Watoto ambapo imeeleza mambo ambayo kamati haikurishwa nayo katika ukurusa wa 29 ni Maafisa wa Ukaguzi na Usalama wa Afya kazini, yaani kuna ubadhirifu wa baadhi ya watendaji wa waukaguzi wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili ni lazima tupambane nalo kwa sababu lazima watu wetu tusiwaadhibu sisi kwa sababu sisi kama hatukuwafanyia ukaguzi tukaona watu wetu wanafanya vipi kazi na wanathaminiwa vipi, hasa hizi sekta binafsi lazima tuoneshe uvivu tukazikague ili tuone wafanyakazi wetu wanafanya kazi lakini katika njia ya salama na amani ili wasinyanyasike, kweli sisi wanyonge lakini tusinyanyasike, lazima tuwague na tuone lakini hapo hapo mishahara ambayo Mhe. Rais ameshaagiza kima cha chini ni laki tatu bado wafanyakazi hawa wa sekta binafsi wanawalipa wanavyotaka. Kama hili ni kosa hawa wanaofanya

makosa haya adhabu ichukuliwe ili waweze kuwapatia mishahara yao sahihi kama inavyohitajika.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende tena katika utowaji wa mikopo na urejeshaji wa mikopo...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizi muda hatuna malizia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mheshimiwa Mfuko wa Uwezeshaji umewezesha wananchi 21,629 mimi nilitaka kujua hawa wanapatikana katika Wilaya gani, Shehia gani ili tuweze kujua kwa sababu sisi tunapoambiwa wamepewa lakini hatujui wametoka Shehia gani, Mkoani gani inakuwa na sisi hatujui sasa tukujua Shehia fulani, Mkoa fulani, Wilaya fulani wamepewa tutaweza kuisaidia serikali ili na sisi kuweze kusimamia...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Nashukuru mheshimiwa baada ya hayo machache naunga mkono kwa asilimia mia moja ripoti hii ya Kamati na Mwenyezi Mungu atupe nguvu na uwezo tuweze kufanya kazi zetu kwa usahihi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe nina orodha ya majina ya watu wengine zaidi ya watatu wamenileta majina. Sasa muda wetu ukitizama kuna muda ambao itabidi tuwape Manaibu Waziri pamoja na Mawaziri kwa ajili ya kujibu baadhi ya hoja.

Kwa hivyo, akimaliza Mhe. Ahmada Yahya atachangia kwa dakika kumi, akimaliza nampa Mhe. Said Soud na yeye achangie muda mdogo sana mchache, halafu nitawapa Manaibu Waziri, wale wote ambao sijawapa nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza, naomba wamepeleke michango yangu kwa maandishi ahsanteni. Sasa Mhe. Ahmada naomba sana uangalie wakati.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii mimi nitakwenda chini ya dakika kumi ulizonipa ili kusudi labda hizi nne nikopeshe kwa Mhe. Hassan Khamis Hafidh nimemuona pale anaomba nafasi kwa mbali.

Mheshimiwa mimi naipongeza sana na naikubali mia chini ya mia ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Katika mchango wangu wa ripoti hii Mhe. Naibu Spika, kwanza naipongeza timu nzima ya wizara kupitia Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi wote pamoja na Katibu Mkuu na wengine wote ambao wamefanya juhudi kubwa sana sekta hii kuikuza na mawaziri ambao wanahusika na sekta zote za ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, lakini shukrani zangu zaidi pamoja na sifa zaidi zinakwenda kwa mwenyekiti wa kamati hii ambaye ni Mwakilishi makini, mzoefu na asiye na papara mwenye kujua mambo Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), amefanya kazi nzuri sana kuongoza kamati hizi na kutuletea ripoti hii mbele yetu. Mchango wangu unakwenda kwanza kuipongeza wizara inayohusiana na michezo ikiongozwa na Komredi Rashid kwa kuondoa migogoro ya michezo kwa kipindi hiki. Jambo ambalo limeletza faraja kubwa timu yetu ya michezo kukua. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukishuhudia miaka ya nyuma mara nyingi migogoro ikienda Mahakamani ya michezo. Lakini sasa naona suala lile limepungua na hata Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein aliwahi kuzungumza haya migogoro inaviza juhudi zetu za michezo, lakini sasa tunasikia hakuna mambo yanayokwenda Mahakani, leo kashitakiwa huyu, leo pingamizi hili. Kwa hivyo jambo hilo sasa hivi linakuza michezo na sasa hivi timu zinafanya vizuri zinaleta sifa katika nchi yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa upande huu wa michezo nachangia sana kuhusu michezo ya maskulini. Mimi nalijua hili jambo katika 1967 na 1968 kulikuwa na michezo ikichezwa ya riadha maskulini ambazo skuli zifuatazo zilikuwa zinaongozwa hapa mjini. Skuli ya Kindongochekundu ikiitwa KC, Skuli ya Kiembesamaki ikiitwa KS, Skuli ya *Gulioni Primary School* ikiitwa *GPS*, *Darajani Primary School* ikiitwa *DPS* na *Bububu Primary School* BPS.

Mhe. Naibu Spika, mimi namshauri sana anzishe michezo ya maskulini ya riadha na mpira kama ilivyokuwa katika miaka 1960 iliibua vipaji vingi sina haja ya kuvisema, lakini mpaka leo vimeweka rekodi na picha zao zipo, akiwepo Dkt. Jidawy na mimi pia nilikimbia Gulioni na wengineo kwa hiyo. Hii imesaidia kwanza kuleta mashamushamu ya michezo nchini na vijana walikuwa hawakai vijiweni kuzungumza mambo yasiyofaa. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nashuhudia kwamba vijana wa Gulioni na Makadara wanatoka wanakuja mpaka kukiitwa Kaburi Msasa jioni mazoezi wanafanya, wana-*troty* wanakuja Mwembeladu wanazunguka wanapita Michenzani. Kwa hivyo lile lilikuwa ni vuguvugu zuri, nahisi angepokea ushauri huo mashindano ya maskulini yale yakaanzishwa na ya riadha kusudi tukazidi kupata vipaji vizuri zaidi katika masuala haya. Hili la pili.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutimiza dakika ambazo nilizoomba ni kwamba nakuja upande wa deni la Gazeti la Zanzibar Leo. Kwa nia safi Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein amefanya matengenezo nyumba ya Kikwajuni wapate ofisi Gazeti lile na kwa muda mfupi wakala wa majengo kazi ile ameifanya kwa kipindi kifupi sana. Kwa hivyo haya ni maendeleo. Hivyo deni la shilingi milioni mia tatu nukta halikuwa *satisfied,* yaani halikuchambuliwa, liko *lump sum of figure* kwamba ni deni la shilingi milioni mia tatu, lakini nani na nani halikutajwa na kama kwa mdeni humjuwi ngapi unamdai, kamati na wizara husika utamjua huyu nimfatilie wapi. Kwa hivyo nadhani ripoti kidogo

ingeweka sawa, wizara hii kiasi gani inadaiwa. Kwa hivyo kwa kushirikiana na serikali pia na Waziri wa Fedha deni lile likalipwa, kusudi shirika hili likawa lina-*move* na linaleta tija kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache mchango wangu ni huo tukumbuke zamani namna mchezo tukicheza, deni lilipwe na migogoro imepungua. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi naikubali asilimia mia moja ripoti hii. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ahmada. Sasa nitampa nafasi Mhe. Said Soud Said naomba uangalie muda.

Waheshimiwa Mawaziri nimepata *note* hapa mkutano huu kikao hichi sio cha kujibu hoja zilizotolewa, naomba sana muelewe musijitayarishe kwa majibu marefu, mujitayarishe kwa majibu mafupi na kukubali kwamba mumepokea mwezi wa Disemba ndio utakuwa ni mwezi wa kuleta taarifa zenu. Mhe. Said Soud Said karibu.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu juu ya hoja hii na kwa nini natoa mchango wangu juu ya hoja hii. Kwa sababu tu Katiba ya Zanzibar Ibara ya 18 imetoa fursa kwa watu wa Zanzibar kupata habari na kutoa habari, kwa maana hiyo habari ni chakula. Sasa kwa sababu habari ni chakula anastahiki kila mtu kupata habari hasa juu ya nchi yake na mambo yanayotendeka.

Mhe. Naibu Spika, lazima tukubali kwamba serikali inajitahidi sana katika kuboresha suala la habari na nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema hoja hii ya habari. Halikadhalika nampongeza Waziri wa Habari mwenyewe kutokana na jitihada zake za kuhakikisha kwamba Wazanzibari wanapata habari na kweli

Wazanzibari wanapata habari, kipindi cha Mawio inafanya kazi, *ZBC* inafanya kazi na mengine yanafanya kazi. Katika mazingira hayo sisi kama Wazanzibari tunafurahi.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile niseme kwamba suala la michezo pia limepewa nafasi kubwa sana katika serikali na Rais mwenyewe amesimamia hoja hii ya michezo mpaka tumeona jinsi gani alivyochukua hatua ya kuweza kukaa pamoja na wachezaji wa *Zanzibar Heroes* mpaka akaweza kula nao chakula na hatimaye kutoa takrima zilizokuwa katika Afrika Mashariki na Kati hazijapatwa kufanywa, kazifanya yeye Rais wetu kwa wachezaji na kwa maana hiyo mimi naweza kusema inatosha, Alhamdulillah pamoja na kwamba kuna watu au Wajumbe wanataka tukae nao tule pamoja, lakini kama kiongozi wa nchi kishafanya hayo sisi tunasema tumpongeza sana Rais kwa kuweze kupokea hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, pia ningetaka niseme kwamba Wazanzibari tunayo haki ya kulinda utalii na watalii katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Kwa sababu utalii umeweza kuboresha maisha ya Wazanzibari sana hasa katika sekta ya kilimo, sekta ya ufugaji, sekta ya uvuvi watu wanauza bidhaa zao na ukitaka kuona saa 11 alfajiri ukienda shimoni pale magari yaliopo pale ambayo yanaleta bidhaa na yanaondosha bidhaa kupeleka mahoteli ya kitalii, unaweza ukasema kwamba Zanzibar imepiga hatua sana katika sekta ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, sasa iko haja Wazanzibari kulinda utalii na kuwalinda watalii na hatimaye kuweza kujipanga kwamba hii ni sekta muhimu katika nchi yetu. Vile vile mimi nashauri kwamba wizara isione tabu kutoa vitambulisho katika mazingira kwa wale watu ambao wanatembeza watalii wakajulikana na wale ambao ni ma-*paparazzi* ambao wanawatembeza watalii na hatimaye hawana sifa, wanawaadhibu, wanawakashifu, wanawafanyia fujo basi si vibaya kukamatwa na wakapelekwa ndani na hatimaye kupata

viboko kumi na mbili kwa ishirini na nne kama vile vya 1964 ambavyo vilikuwa vikitumika, ili wakome ule utaratibu ule, wakipata viboko kumi na mbili vya kuingia na kumi na mbili vya kutoka, mimi naamini watalii watatembezwa na watu wenye heshima.(*Makofi*).

Lakini hawezi leo mtembezaji utalii hajulikani hapa juu ana nywele au ameweka misumari, hafahamiki kama ni Mzanzibari, hafahamiki ana desturi au ana utaratibu gani, ikawa sasa anawakera wazungu ambao sisi wanatupatia pesa za kigeni katika nchi yetu na Zanzibar imepiga hatua kubwa sasa kiutalii, kwa vile lazima sekta hii tuilinde kwa gharama zote ili tuone kwamba inatupatiza faida.

Mhe. Naibu Spika, ningesema kwamba kuna haja ya Wazanzibari kurudi kwenye mila na desturi na ngoma za zamani. Kwa kweli sasa hivi inasitisha sana kuona kwamba harusi sasa zimekuwa zikifanywa sana na marusha roho, zikifanywa sana na madufu lakini ile misondo iliyokuwa ikipigwa sasa haipingwi tena misondo. Sasa na ile misondo ilikuwa ina maana nyingi sana na nyimbo zilikuwa zikitoka kwenye misondo zilikuwa zinaelimisha watu wengi sana, lakini leo harusi sasa zinapigwa madufu, marusha roho ile mila na desturi yetu inaporomoka na kwa nini inaporomoka kwa sababu sisi wenyewe hatuko tayari kuisimamia. Sasa nawashauri Wazanzibari kwamba ipo haja ya sasa kurudi kwenye utamaduni wetu wa asili ili kuboresha mila na desturi za nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nakushukuru sana kwa kutunza muda. Waheshimiwa niliwaeleza Waheshimiwa Mawaziri nikasema mwezi wa Disemba nafikiri ulimi umeteleza ni Septemba. *(Makofi)*

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Ame Haji Ali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake wa kutukutanisha hapa katika kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji katika hotuba hii.

1. Katika kukuza Sekta ya Utalii wizara iendelee kufuatilia suala zima la mapapasi kwenye fukwe zetu hawa bado wanawasumbua wageni.

2. Wizara ishirikiane na taasisi nyengine kupunguza baadhi ya makero kwa wawakezaji wetu hasa wazalendo.
   a) Nazungumzia kero za upatikanaji wa maji safi na salama.
   b) Suala zima la barabara za ndani ambazo nyingi zao ndizo wanazotumia watalii hasa kule kwenye jimbo langu.

3. Sekta ya Michezo bado wizara ifanye juhudi za makusudi ili kutafuta wafadhili. Michezo bila ufadhili bado nchi yetu itaendelea kudumaa katika sekta hii. Wananchi wetu wengi ni wapenzi wa michezo, lakini ukweli ni kwamba hawawezi kupiga hatua kwa kuendesha michezo kwa kuchanga shilingi elfu kumi kumi au kusubiri mtu aendeshe timu.

Bado kazi kubwa inahitajika kufuatilia kwenye mahoteli yaliyo mengi wananchi wetu wananyanyasika katika maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni mchago wangu mfupi. Baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Mohamed Mgaza Jecha: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa maandishi hasa Sekta ya Michezo. Mimi katika

Jimbo langu la Mtambile nitakuwa ni mmoja wapo kwa kujenga kiwanja cha mpira kwa mwaka huu. Kwa hivyo, naomba nisisahaulike katika kijiji changu cha Kangani.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze mawaziri wa wizara hizi mbili kwa utendaji wao. Pili, niwapongeze kamati kwa uwasilishaji wa ripoti ya kamati.

Tatu, *ZBC TV* na Redio, nimpongeze Mhe. Rais kwa kuwapatia *ZBC TV* na Redio vifaa vipya na vya kisasa.

Nne, pia kwa kurusha matangazo ya live katika matumio muhimu hasa ya maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi kutimia miaka 54.

Tano, tunashauri *ZBC* ifanye malipo kwa wakati kwa wafanyakazi ambao wanarusha matangazo moja kwa moja.

Sita, kuwaajiri vijana ambao wamejitolea na kuwapa kipaumbele. Saba, kiimarishwe kitengo cha *ZBC* Dar es Salaam, ili tuweze kupata taarifa kutoka Tanzania Bara. Ahsante naomba kuwasilisha.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nianze Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

1. Naomba wizara iandae vijana chini ya umri wa miaka 17 kwa ajili ya kuimarisha michezo kwa kupata timu ya taifa iliyo bora kama *Zanzibar Heroes*.

Halafu nije Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

2. Naiomba wizara iunde kamati ya kuwashughulikia watoto wenye mazingira magumu, wanaozurura mitaani na kushindwa kuendelea na masomo na kuwarudisha maskuli na kuwapatia

bajeti maalum itakayowasaidia kupata sare za shule na viatu, ili na wao waweze kupata elimu iliyo bora.

3. Naomba wizara wapatiwe usafiri wa gari kisiwani Pemba, kwa ajili ya kufuatilia shughuli zao za kazi hasa panapokuwa na msafara wa viongozi, ili wapate kuandika habari zao haraka na kuzitoa katika vyombo vya habari kwa haraka sana. Ahsante.

Mhe. Shaib Said Ali: Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani kwa wizara mbili na mwenyekiti wa kamati na wajumbe wake, naomba kuchangia yafuatayo.

1) Ukurasa wa 7, Ujenzi wa jengo jipya la *ZBC* Kisiwani Pemba. Naomba wizara iangalie na kufanya utafiti zaidi juu ya jengo hilo, kwani liko karibu sana na njia jambo ambalo linaweza likaleta athari baadae.

2) **Shirika la Magazeti**

Ni vyema sana uchapaji ufanyike Bara, ili gazeti lipate kusomwa na wengi na kupata fedha zaidi.

3) Ukurasa wa 27 Kamisheni ya Kazi

2.1.1 Suala hili ni vyema kuundwa tume, kwani ajira kwa wazalendo ni haba sana hata katika sekta za watu binafsi, kazi ambazo nyengine lazima utaalamu ufanyike.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza mawaziri wote wawili pamoja na watendaji wao. Pia niipongeze kamati hii chini ya mwenyekiti wake Mhe. Ali Salum Ali Shihata.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii imesheheni ushauri kwa wizara hizi, ushauri ambao lengo lake kubwa ni kusaidia ufanisi. Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, lakini ieleweke Zanzibar ina utamaduni wake wa asili, utamaduni wa lugha na silka. Tatizo

linaloikumba nchi zetu nyingi hususan za kiafrika ikiwemo Zanzibar "Ni kuingiliwa kwa tamaduni zetu za asili kwa kuingizwa tamaduni za kigeni, hususan kwa kuingizwa mitandao ya mawasiliano kupitia matumizi ya simu za mikononi.

Mitandao hii inawafanya wananchi wetu, hususan watoto kuiga matendo mbali mbali katika mitandao hiyo. Ndio maana hata hili wimbi la ubakaji kuwa ni jingi sana kutokana na kuiga ndani ya mitandao.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Uandishi wa Habari, naishauri wizara kuwa na utaratibu wa kuwafunza vijana wetu kuwa waandishi wa habari, kwa taaluma maalum na kwa mwananchi anayehusika na afya tu, kilimo tu, elimu tu, mazingira tu au siasa tu.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa kazi kubwa walioifanya na kuitendea haki na kuzifanyia kazi wizara zote mbili ambazo wanazisimamia na wanazifatilia kwa hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, nazipongeza wizara zote mbili hasa Wizara ya Habari na Utalii kwa kuendeleza kazi zake na kuwatendea haki wananchi na wafanyakazi wake. Naipongeza pia Wizara ya Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na wananchi katika kufatilia kesi za udhalilishaji na haki za wanawake na watoto pia.

Niwaambie tu wanakamati poleni sana kwa kazi ambayo mnakabiliana nayo, pia kwa changamoto kubwa mnazokabiliana nazo wakati wa kazi za kamati mpaka kufikia kutoka machozi kwa jinsi ya hali ilivyo juu ya suala la udhalilishaji.

Niwapongeze pia na hongereni mnajitahidi, Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi nichangie kwa maandishi Ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Wizara ya Habari kwa kupitia Tume ya Utangazaji kwa mafanikio mazuri ya kuboresha habari kwa wananchi wetu, ili kuweza kuchukuwa, kusikiliza, kitu chochote cha redio na televisheni kwa lengo la kupata kuangalia au kusikiliza matukio mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya mawimbi ni changamoto kubwa sana na hasa kwa kuzingatia kuwa habari ndio moyo wa nchi yetu. Ukosefu wa mawasiliano au habari kunaweza kuiletea matatizo makubwa nchi yetu. Hivyo niiombe serikali kuliangalia kwa kima tatizo hili hatimae lipatiwe ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, mfuko wa Uwezeshaji Wanawake na Makundi Maalum. Lakini cha kusikitisha kuwa katika uwezeshaji huo Makundi maalum hayamo hasa watu wenye ulemavu.

Nimuombe sana Mkurugenzi pamoja na Maafisa wake wa Wilaya na Mkoa kupitia wizara hii kujipanga vizuri kwa kutoa elimu ya kuhamasisha na kuwashirikisha vikundi vya watu wenye ulemavu bila ya kuwabagua.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya wizi tunaiomba serikali iliangalie kwani mwizi akiingia ndani haachi kitu akikosa kitu anaweza akadhuru hata mtu na ukizingatia mle ni kituo cha kulelea watoto na wengine hawajiwezi kwa udogo wao.

Naiomba serikali kuwapatia ulinzi wa askari hasa nyakati za usiku.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mwenyekiti kwa taarifa yake aliyoitoa.

Napenda kuchangia kwenye Sekta ya Uwezeshaji kifungu (c) Vyama vya Ushirika. Kama unavyoelewa katika maeneo yetu kuna wananchi wengi ambao wamejikusanya na kuunda vikundi vya Ushirika lakini vikundi hivyo vinakufa baada ya muda kutokana na matatizo yanayojitokeza hapa na pale kama vile:-

- Ukosefu wa Elimu
- Ukosefu wa Mtaji
- Ukosefu wa Soko kwa ajili ya bidhaa zao

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aje anijibu atafanya utaratibu gani ili vikundi vile vizidi kuimarika katika maeno yetu.

Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto:

Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni suala ambalo limeenea katika maeneo yetu hasa Mkoa wetu wa Kaskazini Unguja, udhalilishaji umekithiri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna aina nyingi za udhalilishaji kama vile:-

- Upakaji
- Kuwalawiti watoto wa Kiume
- Kumwacha mwanamke na mimba bila ya huduma yoyote
- Kuwatelekeza watoto.

Mhe. Mwenyekiti, hayo yote ni miongoni mwa mambo yote ya suala la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya yalikithiri kwa watoto wetu na kama nilivyoeleza hapo mwanzo kuwa Mkoa wetu umezidi.

Juzi tu katika Vyombo vya Habari kuna vijana watatu wamebakwa na mtu mmoja kwa kuwapa pipi.

Mhe. Mwenyekiti, huo ni udhalilishaji mkubwa kuwa hadi leo mtu yule yupo nje anadunda mitaani na kujisifu.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri suala lile alifanyie kazi na hatiame atupe majibu kwa nini muhalifu yule hadi leo yuko nje na sheria zipo.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, mimi naomba kuchangia Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

(1) **Sekta ya Wanawake na Watoto:**

Mhe. Spika, nashauri kuundwe kikundi maalum katika sheria kusimamia wale wote watakaozalilishwa na kupekeka taarifa kwa sababu baadhi ya wazee hawafaidiki na habari zinazotokea.

(2) **Maagizo ya Kamati:**

Mhe. Mwenyekiti, wadau wote wanaotoa huduma za utalii wanalipa leseni za uwekezaji kwa wakati na kiwango sahihi. Naunga mkono ripoti hii Mhe. Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar:

(1) Niipongeze serikali yangu pamoja na Mheshimiwa Jemedari wake Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Ali Mohd Shein kwa juhudi za makusudi

anazochukuwa kuona kwamba wananchi wake wanapata huduma za afya ndani kote karibu na bila usumbufu.

(2) Pia katika mambo ya elimu hayako nyuma niwapongeze pamoja na mawaziri na watendaji lakini hasa walimu.

(3) Naipongeza kamati kwa kazi kubwa iliyofanya ya kufatilia mambo yote na baadae kuleta katika Baraza la Wawakilishi.

(4) Sasa niziombe wizara zote mbili kwa mashirikiano na serikali kuu kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa kamati na Wajumbe wa Baraza.

(5) Kuhusu madaktari kupelekwa vituoni mote ambao imeonekana kuna upungufu mkubwa kwani vituoni bila ya madaktari ni sawa na kutokuwepo.

(6) Vile vile Wizara ya Elimu ifatilie mfumo wa masomo unaendelea hasa kwa vijana wetu ambao wako karibu na kupanga mitihani juu ya usomaji wao,

- Vijana hawa mara nyingi wanasoma kwa kupasi mtihani tu kwa njia ya *past paper* baada ya kufahamu masomo yenyewe.

- Tuangalie ili ubora wa elimu kwa vijana wetu na nchi yetu upatikane.

Naomba sana changamoto na maoni pia ushauri ufanyiwe kazi.

Vile vile kuhusu Ajira ya Nje ya Nchi, naipongeza sana serikali yetu kupitia Wizara ya kazi kwa mashirikiano makubwa na wawakala wa Ajira za nje hadi kufauli wa kupata ajira kwa vijana

wetu wa Zanzibar wasiopungua 620, kwa kipindi kin achoishia Disemba 2017, katika nchi mbali mbali duniani.

Mhe. Waziri atakapofanya majibu yake atujuilishe ni wakala Binafsi wangapi waliopo hapa Zanzibar.

Pia Wakala hawa wanatuhudumia vipi na mawasiliano yao yako vipi na wateja wao wakiwa katika kutekeleza majukumu yao huko nje, dhidi ya matatizo ya unyanyasaji, uvunjaji wa ovyo ovyo wa mikataba yao ya kazi. Pamoja na kupata stahili zao pale wanapofika wakati wa malipo kwa sababu kuna taarifa ya uvumi wa dharau na uvunjaji wa haki za binaadamu katika sehemu zao za kazi.

Mkuhusu Idara ya Usalama na Afya Kazini.

- Idara hii ipo kisheria.
- Je, ni vipi Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto inasimamia katika sekta za Binafsi na sekta za Umma kwa suala zima la kuwakatia Bima ya Afya kwa wafanyakazi wao ili kulinda afya zao na kuwa bora ili waweze kushiriki vyema kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Zaina Abdalla Salum:

(i) Mhe. Mwenyekiti, niipongeze kamati kwa kazi nzuri ya ukaguzi. Pia uwasilishaji wa ripoti ni mzuri nimpongeze Mhe. Mwenyekiti.

(ii) Ukaguzi wa kamati ulikuwa una lengo la kuhakiki utekelezaji wa bajeti katika wizara hizi mbili kwa sekta zake mbali mbali kuona kwamba unatekelezwa.

(iii) Mhe. Mwenyekiti, niiombe kamati kwamba pale tu wanapofanya ukaguzi wanatakiwa kujua pia huduma za watu wenye ulemavu zinaimarishwa.

(iv) Kuwe na mbinu gani zinazotumika kutoa msaada kwa watu hao ni vipaombele gani vilivyowekwa katika kituo cha Afya au kuhakikisha au vyuo ambavyo vinatumika kuhakikisha mtu mwenye ulemavu anapatiwa huduma husika.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii na Michezo pamoja na jitihada zao zote wanazofanya kuwasaidia vijana katika suala la Michezo nashauri angalau wajengewe viwanja kwa kila Wilaya ili vijana waweze kuendeleza na kutunza vipaji vyao.

Pili, kwako Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wako watetee Waandishi wa Habari ambao hushiriki Vikao vyote vya Baraza la Wawakilishi ni vyema wapatiwe malipo yao mapema kama taasisi nyengine zote zinavyolipwa kwani kumekuwa na malalamiko kutoka kwao wanacheleweshewa sana malipo yao. Naunga mkono hotuba yenu ya kamati na nawapongeza nyote kwa jumla.

Kwa hivyo Waheshimiwa sasa nimpe nafasi Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo Mhe. Naibu Waziri karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo, Wanawake, Habari na Utalii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kukushuru wewe binafsi pamoja na uongozi wako wakiwemo watendaji pia wa Baraza letu tukufu.

Mhe. Naibu Spika, pili napenda pia nichukuwe fursa hii kuishukuru Kamati ya Wanawake, Habari na Utalii, kamati hii imekuwa ikitupa miongozo mbali mbali, imekuwa ikitupa maelekezo mbali mbali na ndio maana leo tumefikia hatua mbayo tumefikia ya maendeleo kwa wizara yetu.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, shukrani za pekee zimuendee Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye naye amekuwa akitushauri na kutupa miongozo yake, lakini pia tunamshukuru sana kwa kutupatia vifaa ambavyo vimeondoa kero za wananchi wetu hasa kuhusu vyombo vya habari, televisheni na redio, hili tunampongeza sana Mhe. Rais kwa kutupatia vyombo hivi na sisi tukaweza kufanya kazi.(*Makofi*)

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, napenda pia niwashukuru watendaji wote wa wizara kwa kutupatia mashirikiano ya pamoja na kusimama nao kwa pamoja na kuendeleza kazi zetu ambazo pia nazo zimeonyesha tija kwa wananchi lakini pia na kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba niwashukuru sana wachangiaji wote na Wajumbe ambao wamechangia ripoti yetu au ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo, Habari na Wanawake na kutoa changamoto zile ambazo wameziona katika ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, naahidi kwamba kwa kuwa sisi ni wasikivu sana pamoja na watendaji wetu kwa yake ambayo yemejitokeza changamoto ambazo zimejitokeza katika sehemu mbali mbali za taasisi zetu, tunaahidi kwamba tunazipokea na bado tutaendelea kuzifanyia kazi ili kuona kwamba zile kero ambazo zimejitokea katika ripoti hii zimeondoka na hatimaye kupata ufanisi bora kwa wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa leo hii sisi hatutakiwa kujibu ni kupokea tu hii ripoti na pia na kuifanyia kazi, niseme tu kwamba naunga mkono ripoti hii asilimia mia moja na yale ambayo yote mapungufu, baadhi ya mapungufu ambayo yamo katika ripoti hii. tunaahidi kwamba tutaifanyia kazi na kuona kwamba tunaipatia tija serikali yetu lakini na wananchi wake kwa jumla.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri sasa nitampa nafasi Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Shadya karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kumalizia muda huu wa kuweza kuchangia machache katika ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari, Utalii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kama ulivyotangulia kusema kwamba sisi leo hatutakiwi kujibu bali maelekezo yote ambayo kamati wamependekeza na sisi tunaahidi kwamba tutayachukua na kuweza kuyafanyia kazi itakapofika mwezi wa tisa Inshaallah nina hakika kwamba kwa umakini wa watendaji wangu nitaweza kuleta majibu sahihi ambayo kwa kila mjumbe ameweza kuchangia na yeye anaweza kufurahia majibu haya.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, japo kwamba umesema kwamba hatutakiwi kujibu hoja lakini naomba kwa ruhusa yako naomba niruhusu kidogo niweze kumuweka sawa Mhe. Shehe Hamad Mattar wa Jimbo la Mgogoni aliyetaka kujua kwamba katika taasisi za binafsi ambazo tuliweza kutembea na kuweza na ambao wameweza kuitikia huu wito wa kuweza kulipa mishahara ambayo kima cha chini serikali imeagiza taasisi ambazo tuliweza kuzitembelea ni taasisi 317 waliotekeleza ni 225 sawa na asilimia

71. Baada ya kusema hayo machache Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi nichukue fursa hii ya kuunga mkono ripoti hii ya kamati, nakushukuru sana Mhe. Spika. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Michezo, Utamaduni na Utalii: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii ya dakika isiyozidi moja kutoa pongezi zangu za dhati tu hususan kwa mwenyekiti na wajumbe wake wa kamati. Lakini vile vile nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye usimamizi wake umeipelekea ripoti hii leo kuonekana kama inavyoonekana. Baada ya hayo kama tulivyosema majibu ya masuala haya, michango, maoni uhondo wake utakuwa mwezi wa Septemba, 2018. Kwa hiyo, basi niwashukuru Wajumbe wako wote wa Baraza la Wawakilishi kwa dhati kabisa wamechangia kwa nia moja, wamechangia kwa undani michango yao yote tumeichukua, tumeithamini, tumeiandika kwa urefu kabisa na majibu yao inshaallah watayapata kwa kutumia sera, kanuni, sheria zile ambazo zinaongoza ndani ya wizara yetu.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana wewe na Mhe. Spika na Baraza lako kwa jinsi unavyoliongoza na kwa umakini ulioliongoza katika kipindi hiki cha Baraza la Tisa na huu ni Mkutano wa Tisa. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. Ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia zoe mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa nafasi ya kuweza kuwepo kwa siku ya leo na hasa kusikiliza Kamati yetu ambayo imekuwa ikiongozwa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), pamoja na wajumbe wote kwa ujumla ambao wamekuwa pamoja na sisi. Tunashukuru sana kwamba tangu tumeanza mpaka sasa hivi tunaendelea vizuri kwa sababu

wamekuwa karibu sana na sisi na kuendelea kutusaidia na kutupitia tunashukuru sana. Lakini pia nimshukuru sana Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi anazofanya kila wakati kutushauri na pale tunapojisahau yuko tayari kutukumbusha na kutuelekeza. Nipongeze sana mheshimiwa ofisi yako ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Spika pamoja na wewe na watendaji wote pamoja wamekuwa ni watu wanaoshiriki kikamilifu na wanafanya kazi kila tunapowaomba kutaka kuelekeza wanatuelekeza.

Aidha, nipende kuwapongeza wajumbe wote walioweza kutoa mawazo waliyotushauri, wengine wamesema ni maagizo lakini sio maagizo ni kwamba wanatushauri ili tukaweze kutekeleza kazi tutafanyia utafiti na kuyaweka wazi hata yale niliyopongezwa namshukuru sana Mwenyezi Mungu na yale pia ambayo tumeambiwa kwamba tuyaweke vizuri na tuyalete katika mwezi wa Septemba tutayaleta. Naomba mnivumilie kidogo kuwataja wajumbe mlioko hapa maana yake wengine watadhani kwamba hamko Barazani inawezekana hamuonekani huko. Niwashukuru viongozi wote waliochangia katika nafassi zote.

Kwanza napenda nimshukuru sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Abdalla Ali Kombo, Mhe. Asha Abdalla Mussa…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri naomba ushukuru na upokee na hao ambao ni wachangiaji watatajwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ndiye ambaye mwenye madaraka ya kutaja waliochangia, yeye ndiye mwenye hoja. Kwa hiyo, naomba hao uwaache labda kuna jengine ambalo ulikuwa unataka kidogo kulielezea naweza nikakupa muda, lakini kwa majina anayetakiwa ni Mhe. Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikiwashukuru wote kwa ujumla na nakushukuru sana na nawapongeza.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote tuliokuwemo humu kufikia malengo ambayo kuanzia asubuhi hadi usiku huu tulikuwa tunachangia ripoti ya wizara zetu mbili au Ripoti ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

Mhe. Naibu Spika, lakini niseme kwa dhati kabisa niwapongeze waheshimiwa wote waliochangia na waliokuwa hawakubahatika kuchangia kwa sababu kama ulivyosema mheshimiwa laiti kama muda ungepatikana basi tungekuwa na wachangiaji wengi sana, lakini hata hivyo naamini walikuwa hawakubahatika pia wataridhika kwa hawa waliochangia.

Mhe. Naibu Spika, katika wachangiaji wote tuliowapata katika kamati yetu hii ni wachangiaji 38, wachangiaji 21 wamechangia moja kwa moja na 17 wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba wachangiaji walikuwa wengi na naomba niwataje wakae kwenye hansard.

1. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Omar Seif Abeid
4. Mhe. Machano Othman Said
5. Mhe. Abdalla Ali Kombo
6. Mhe. Asha Abdalla Mussa
7. Mhe. Suleiman Sarahan Said
8. Mhe. Hamza Hassan Juma
9. Mhe. Shehe Hamad Mattar

10. Mhe. Rashid Makame Shamsi
11. Mhe. Said Omar Said
12. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
13. Mhe. Suleiman Makame Ali
14. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
15. Mhe. Panya Ali Abdalla
16. Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil
17. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
18. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
19. Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
20. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
21. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, mengi waliyoeleza wajumbe hao tumeyasikia lakini pamoja na hayo tuwataje na wenzetu ambao wamechangia kwa maandishi. Mhe. Naibu Spika, wachangiaji waliochangia kwa maandishi naomba na wao niwataje ili wabakie katika *hansard* zetu. Lakini kubwa katika michango yao ilikuwa ni michango ya kusisitiza mambo mbali mbali.

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
2. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha
3. Mhe. Bahati Khamis Kombo
4. Mhe. Zaina Abdalla Salum
5. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
6. Mhe. Ali Khamis Bakar
7. Mhe. Ussi Yahya Haji
8. Mhe. Hamida Abdalla Issa
9. Mhe. Mgeni Hassan Juma
10. Mhe. Hidaya Ali Makame
11. Mhe. Ame Haji Ali

12. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
13. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
14. Mhe. Mussa Ali Mussa
15. Mhe. Miraji Khamis Mussa
16. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Spika, haya yalikuja mwisho mwisho katika kupapatua kuweka sawa, lakini mmoja niliyekuwa sikumtaja atanisamehe atajitaja aingie katika *hansard*.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla niseme tu kwamba kwanza nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote, nawapongeza Manaibu Waziri, nawapongeza Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wote wa wizara pia na watendaji wao wote kwa jumla. Aidha, mheshimiwa nachukua fursa hii kusema kwa dhati kabisa katika kamati yetu kazi tulizoziendea nyingi tulizozipata baada ya kutoa taarifa ya ripoti yetu, Waheshimiwa Wajumbe wengi wameipokea vizuri na maagizo mbali mbali ambayo wameyatoa Mhe. Waziri wakija kipindi cha Septemba watatoa majibu sahihi. Katika changamoto moja au mbili niziseme kwa ufupi sana.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nawashukuru wajumbe wameifahamu ripoti yetu, kadhia kubwa iliyozungumzwa hapa juu ya watendaji wetu wa *ZBC* waangaliwe kwa makini sana, hasa tukiangalia ushindani wa maendeleo katika vyombo mbali mbali tulivyokuwa navyo. Kubwa jengine ambalo limezungumzwa hapa ni suala la utendaji wa kazi kwa bidii. Mhe. Naibu Spika, tuna matatizo katika sehemu mbali mbali tulizotembelea tunaomba zichukuliwe hatua ili kuondoa kero na ubabaishaji kwa baadhi ya maeneo. Sehemu ya utendaji katika sekta ya utalii na miundombinu ni jambo muhimu lisingojee Septemba barabara zitengenezwe.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna changamoto nilizozipata nyengine kubwa kwa usalama wa watalii wetu, hakuna jambo zuri kuliko ulinzi kwa watalii wetu na sisi wenyewe kwa ujumla. Tunaiomba serikali kwa jumla suala la ulinzi katika mahoteli yetu, suala la ulinzi katika maeneo yetu tunayoishi wananchi wote liangaliwe kwa usalama uliokuwepo. Kwa bahati mbaya Mhe. Naibu Spika, baada ya kusoma taarifa hii na kuiandika yaliyotokea katika nchi yetu tumeyapata, hali ya usalama kwa watoto wetu haipo, udhalilishaji umezidi, unatisha, watoto wanatekwa sasa hivi. Mhe. Naibu Spika, hii tunaisema kama hali halisi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, leo mimi kwa masikio yangu na macho yangu nimemuona katika televisheni, ingawa msemaji kafichwa lakini nilishuhudia mchana mtoto jinsi alivyokamatwa akatekwa kwenye gari akachukuliwa kupelekwa pahala pasipojuulikana na vitendo viovu alivyofanyiwa. Naiomba serikali tuangalie kwa usalama wa watoto wetu na sisi wenyewe kwa jumla pana nini hapa nchini. Mhe. Naibu Spika, hofu yangu pana mtandao umeandaliwa kwa makusudi na watu waliokuwa hawajitambui. Kwa hivyo, serikali ili tuhakikishe tunaliweka sawa hili tusikae tukafikiri hili suala ni dogo, ni suala la aibu na suala kubwa katika nchi yetu. Mtoto mwanamke anaitwa fulani anaitikia naam, anakwenda kwa heshima kabisa anafika pale watu wanafungua mlango wanamtia ndani gari wanamchukua wanampeleka pahala pasipojuulikana. Ah!

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa endelea, naomba mumletee maji ya kunywa mheshimiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Naomba uje utoe hoja mheshimiwa.

Wajumbe: Ameshatoa hoja

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sikumsikia mnapiga hizo meza sana.

Waheshimiwa Wajumbe Mwenyekiti wa Kamati ameshatoa hoja wale wanaokubaliana na hoja yake wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nichukue fursa hii adhimu kwanza kukushukuruni nyote kwa utulivu wenu lakini kwa michango mizuri ambayo mmechangia kutokana na taarifa ambayo imetolewa na kamati. Pia nichukue fursa hii vile vile kuwashukuru kwa utulivu lakini kwa michango ambayo mmetoa. Vile vile niwashukuru Mawaziri na Manaibu Waziri ambao nao pia wameweza kupokea ripoti hii pamoja na michango iliyotolewa na kuahidi kwamba watakuja kuyafanyia kazi na kuleta majibu mwezi wa Septemba. Vile vile nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ambaye alitoa taarifa hii lakini pamoja na hayo kutoa majumuisho ya ripoti ambayo ameitoa.

Waheshimiwa Wajumbe, tuna kazi kubwa katika jamii yetu lakini tuna kazi kubwa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kazi hizi na wajibu huu tunaufanya kwa pamoja, nichukue tena fursa kuwashukuru sana na sasa naakhirisha kikao hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:16 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 20/02/2018 saa 3:00 asubuhi)

/